BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR 2016 - 2020

1.	**Mhe.**	**Zubeir Ali Maulid**	**-**	**SPIKA**
2.	**Mhe.**	**Mgeni Hassan Juma**	**-**	**Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake**
3.	**Mhe.**	**Shehe Hamad Mattar**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni**
4.	**Mhe.**	**Mwanaasha Khamis Juma**	**-**	**Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani**
5.	**Mhe.**	**Balozi Seif Ali Iddi**	**-**	**MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda**
6.	**Mhe.**	**Issa Haji Ussi Gavu**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka**
7.	**Mhe.**	**Haji Omar Kheri**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu**
8.	**Mhe.**	**Haroun Ali Suleiman**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi**
9.	**Mhe.**	**Mohammed Aboud Mohammed**	**-**	**MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Uteuzi wa Rais**
10.	**Mhe.**	**Dkt. Khalid Salum Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge**
11.	**Mhe.**	**Mahmoud Thabit Kombo**	**-**	**MBM/Waziri wa Habari, Utalii, na Mambo ya Kale/Jimbo la Kiembesamaki**
12.	**Mhe.**	**Riziki Pembe Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake**
13.	**Mhe.**	**Balozi Amina Salum Ali**	**-**	**MBM/Waziri wa Biashara,**

			na Viwanda / Uteuzi wa Rais
14.	**Mhe. Balozi Ali Abeid Karume**	**-**	**MBM/Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Uteuzi wa Rais**
15.	**Mhe. Rashid Ali Juma**	**-**	**MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Amani**
16.	**Mhe. Hamad Rashid Mohamed**	**-**	**MBM/Waziri wa Afya / Uteuzi wa Rais**
17.	**Mhe. Maudline Cyrus Castico**	**-**	**MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais**
18.	**Mhe. Salama Aboud Talib**	**-**	**MBM/Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati / Nafasi za Wanawake**
19.	**Mhe. Sira Ubwa Mamboya**	**-**	**MBM/ Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais**
20.	**Mhe. Juma Ali Khatib**	**-**	**MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
21.	**Mhe. Said Soud Said**	**-**	**MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Uteuzi wa Rais**
22.	**Mhe. Khamis Juma Mwalim**	**-**	**Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe**
23.	**Mhe. Mihayo Juma N'hunga**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais /Jimbo la Mwera**
24.	**Mhe. Shamata Shaame Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Micheweni**
25.	**Mhe. Harusi Said Suleiman**	**-**	**Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete**
26.	**Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri**	**-**	**Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani**
27.	**Mhe. Mohamed Ahmada Salum**	**-**	**Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/Jimbo la Malindi**
28.	**Mhe. Chum Kombo Khamis**	**-**	**Naibu Waziri wa Habari,**

			Utalii na Mambo ya Kale/ Nafasi za Wanawake
29.	**Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Uwezeshaji,**	**-**	**Naibu Waziri wa Wazee, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake**
30.	**Mhe. Lulu Msham Abdalla**	**-**	**Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo/ Nafasi za Wanawake**
31.	**Mhe. Juma Makungu Juma**	**-**	**Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba , Maji na Nishati / Jimbo la Kijini**
32.	**Mhe. Hassan Khamis Hafidh**	**-**	**Naibu Waziri wa Biashara, na Viwanda /Jimbo la Welezo**
33.	**Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi**	**-**	**Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mtopepo**
34.	**Mhe. Abdalla Ali Kombo**	**-**	**Jimbo la Mwanakwerekwe**
35.	**Mhe. Abdalla Maulid Diwani**	**-**	**Jimbo la Jang'ombe**
36.	**Mhe. Ali Khamis Bakar**	**-**	**Jimbo la Tumbe**
37.	**Mhe. Ali Salum Haji**	**-**	**Jimbo la Kwahani**
38.	**Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)**	**-**	**Jimbo la Kijitoupele**
39.	**Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil**	**-**	**Uteuzi wa Rais**
40.	**Mhe. Ame Haji Ali**	**-**	**Jimbo la Nungwi**
41.	**Mhe. Amina Iddi Mabrouk**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
42.	**Mhe. Asha Abdalla Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwengwa**
43.	**Mhe. Bahati Khamis Kombo**	**-**	**Jimbo la Chambani**
44.	**Mhe. Bihindi Hamad Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
45.	**Mhe. Hamad Abdalla Rashid**	**-**	**Jimbo la Wawi**
46.	**Mhe. Hamida Abdalla Issa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
47.	**Mhe. Hamza Hassan Juma**	**-**	**Jimbo la Shaurimoyo**
48.	**Mhe. Hidaya Ali Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
49.	**Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)**	**-**	**Jimbo la Mtoni**
50.	**Mhe. Jaku Hashim Ayoub**	**-**	**Jimbo la Paje**
51.	**Mhe. Khadija Omar Kibano**	**-**	**Jimbo la Mtambwe**
52.	**Mhe. Machano Othman Said**	**-**	**Jimbo la Mfenesini**
53.	**Mhe. Makame Said Juma**	**-**	**Jimbo la Kojani**
54.	**Mhe. Maryam Thani Juma**	**-**	**Jimbo la Gando**
55.	**Mhe. Masoud Abrahman Masoud**	**-**	**Jimbo la Bububu**
56.	**Mhe. Miraji Khamis Mussa**	**-**	**Jimbo la Chumbuni**
57.	**Mhe. Moh'd Mgaza Jecha**	**-**	**Jimbo la Mtambile**
58.	**Mhe. Mohamed Said Mohamed**	**-**	**Jimbo la Mpendae**
59.	**Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali**	**-**	**Jimbo la Uzini**
60.	**Mhe. Mtumwa Peya Yussuf**	**-**	**Jimbo la Bumbwini**
61.	**Mhe. Mtumwa Suleiman Makame**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
62.	**Mhe. Mussa Ali Mussa**	**-**	**Jimbo la Ole**
63.	**Mhe. Mussa Foum Mussa**	**-**	**Jimbo la Kiwani**

64.	**Mhe.**	**Mwanaidi Kassim Mussa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
65.	**Mhe.**	**Mwantatu Mbaraka Khamis**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
66.	**Mhe.**	**Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini**	**-**	**Jimbo la Dimani**
67.	**Mhe.**	**Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy**	**-**	**Jimbo la Chaani**
68.	**Mhe.**	**Nassor Salim Ali**	**-**	**Jimbo la Kikwajuni**
69.	**Mhe.**	**Omar Seif Abeid**	**-**	**Jimbo la Konde**
70.	**Mhe.**	**Panya Ali Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
71.	**Mhe.**	**Rashid Makame Shamsi**	**-**	**Jimbo la Magomeni**
72.	**Mhe.**	**Saada Ramadhan Mwendwa**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
73.	**Mhe.**	**Said Omar Said**	**-**	**Jimbo la Wingwi**
74.	**Mhe.**	**Said Hassan Said**	**-**	**Mwanasheria Mkuu**
75.	**Mhe.**	**Salha Mohamed Mwinjuma**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
76.	**Mhe.**	**Salma Mussa Bilal**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
77.	**Mhe.**	**Shaib Said Ali**	**-**	**Jimbo la Chonga**
78.	**Mhe.**	**Simai Mohammed Said**	**-**	**Jimbo la Tunguu**
79.	**Mhe.**	**Suleiman Makame Ali**	**-**	**Jimbo la Ziwani**
80.	**Mhe.**	**Suleiman Sarahan Said**	**-**	**Jimbo la Chakechake**
81.	**Mhe.**	**Tatu Mohamed Ussi**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
82.	**Mhe.**	**Ussi Yahya Haji**	**-**	**Jimbo la Mkwajuni**
83.	**Mhe.**	**Viwe Khamis Abdalla**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
84.	**Mhe.**	**Wanu Hafidh Ameir**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
85.	**Mhe.**	**Yussuf Hassan Iddi**	**-**	**Jimbo la Fuoni**
86.	**Mhe.**	**Zaina Abdalla Salum**	**-**	**Nafasi za Wanawake**
87.	**Mhe.**	**Zulfa Mmaka Omar**	**-**	**Nafasi za Wanawake**

Ndg. Raya Issa Msellem - Katibu

Kikao cha Kumi na Sita – Tarehe 30 Mei, 2018

(Kikao Kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 74

Hali Mbaya ya Soko la Samaki Darajani

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Kwa muda mrefu sasa soko la samaki la Darajani limekuwa katika hali mbaya ya kimazingira kutokana na uchakavu na mazingira yasiyo salama kwa kitoweo kinachouzwa hapo.

(a) Je, kwa kuwa wafanyabiashara wanalipa fedha zao Baraza la Manispaa kwanini fedha hizo hazitumiki kufanyia ukarabati na kuweka mazingira mazuri ya kufanyia biashara ya kitoweo.

(b) Kuliacha soko hilo kuendelea kuwa katika hali mbaya kama ile si kuhatarisha afya za walaji wa kitoweo kinachouzwa sokoni hapo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, siko hadhiri kidogo lakini naomba kabla ya kuuliza swali langu niagize tu au niombe Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pana toleo hapa kaweka katika Gazeti la Zanzibar Leo, niombe Mawaziri na Manaibu Manaibu watakapoingia kwanza waangalie hapa ki-*board* chetu alivyoagiza la Julai 4 kwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri watujibu hoja zetu za Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba ueleze tena sija kuelewa.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, ninachokiomba tu Mawaziri na Manaibu Mawaziri watapojibu maswali kidogo wakapita njia hii pana Gazeti hapa la Zanzibar Leo lilitolewa 2014 aliloagiza Mhe. Rais kuwa waheshimiwa wajibiwe maswali yao kikamilifu. Kwa hiyo niombe anapojibu swali ajibu kwa ukamilifu kwa usahihi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 74 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba nimpe pole kwamba kutokuwa hadhiri kwa siku ya leo lakini Inshaallah namuomba nimtowe shaka kwamba majibu nitakayomjibu yatakuwa yana uhalisia.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa la Mjini kwa kushirikiana na wafanyabiashara wa soko la samaki Darajani limefanya matengenezo ya vibaraza vya kuuzia samaki na nyama kwa kuweka vigae vibaraza hivyo kazi ambayo inaendelea. Vibaraza vya nyama 36 na vibaraza vya samaki 37 vimetengenezwa. Aidha, Baraza katika robo mwaka huu iliyobaki limeanza kutengeneza matenga maalumu ya "Aluminium" ili bidhaa hizo zipokelewe na kuwekwa katika mazingira salama zinazopoteremshwa kutoka garini.

(b) Mhe. Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba mazingira machafu sehemu yoyote ni chanzo kikuu cha kuhatarisha afya ya binaadamu. Hivyo basi, hali kama hiyo inakuwa ni hatari zaidi pale mazingira machafu yanapokuwa katika maeneo ya vyakula. Kwa kulitambua hilo, Baraza linaendelea kuchukuwa hatua kama nilizozieleza katika jibu langu (a). Aidha, hatua hiyo zitajumuisha pia upakaji rangi ya mafuta ambayo itaweza kukosheka kwa maji. Sambamba na hili, Baraza litaendelea kutoa elimu kwa watumiaji wa soko na kushiriki kulitunza kwa kuepuka vitendo vya uchafuzi wa mazingira ikiwemo kutupa mabaki ovyo na kuchafua kuta za jengo kwa kufutia uchafu.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, naomba unilinde nitumie nitumie Kanuni ya 37 kwa lugha laini na nyepesi saa 2 kabla ya kuja hapa niko Barazani hivi asubuhi ndio nikafanya utafiti nikaja hapa.

> "Waziri au mjumbe yeyote anaeuliza swali ambalo ana madaraka nao atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu na kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa swali hilo aliloulizwa moja linaweza kujibiwa na waziri mwengine au Mwanasheria Mkuu".

Mhe. Mwenyekiti, haya majibu sitaki kusema lugha nyengine na Ramadhani nisije nikateleza, kwanza Mhe. Naibu Waziri hakuna ujenzi unaoendelea wowote si kitu cha ukweli hakuna ujenzi, saa 2 niko sokoni ndio ninachokwambieni Mhe. Waziri au Naibu Mawaziri fanyeni utafiti kabla ya kutujibu niko tayari ….

Mhe. Mwenyekiti: Swali Mheshimiwa

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, najenga hoja kama haiwezekani ende tukaone mguu kwa mguu kauli yake hii hakuna ujenzi wowote uanaoendelea saa 2 niko pale sokoni. Nilichokiona tu jana watu wamekatwa.....

Mhe. Mwenyekiti: Uliza swali usilete mkutano mwengine, muulize swali Mhe. Waziri.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ni maafisa wangapi wamechukuliwa hatua kwa kushindwa kusimamia kanuni za afya kwenye soko la samaki wanaouza chini kwenye soko hilo ni maafisa wangapi wamechukuliwa hatua, isipokuwa jana tu kuna watu kama 4:

1. Rashid Ali
2. Khamis
3. Omar
4. Said

Mhe. Mwenyekiti, watu hawa wamekamatwa na wakalipishwa Tshs. 15,000 soko chafu wakakamatwa wao

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub subiri akujibu umeshamuuliza swali usilete tena mkutano.

(a) Mhe. Mwenyekiti, ni sababu gani walizokamatiwa vijana hawa wakakamatwa wakalipishwa Tshs. 15,000 niliowataja wakati soko chafu kwa kushindwa kuvaa nguo rangi ya buluu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, uzoefu unaonesha serikali haiwezi kufanya biashara je, suala hili nimeshalisemea karibuni miaka 7 au 8 iko tayari kubinafsisha kama ilivyofanywa hoteli za African House, Zanzibar Hotel, Starehe Club yuko tayari kubinafsisha baada ya kushindwa kusimamia majukumu yao, Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Tawala za Mikoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kabla sijajibu maswali 2 ya nyongeza ya Mhe. Jaku Hashim Ayoub naomba Mhe. Jaku Hashim Ayoub atuamini na Waheshimiwa Wajumbe watuamini tunachofanya kazi hapa tunafanyakazi kwa umakini na majibu ambayo tunayatoa ndio yale ambayo tuliyokuwa nayo na ambayo ndiyo uhalisia wenyewe. Ukisema Mheshimiwa nikanushe kwamba hakuna ujenzi unaoendelea na atakumbuka kwamba hata mimi mwenyewe binafsi nimefika shughuli hiyo inaendelea hatujavunja jengo kwa maana hiyo, tunakarabati na ukarabati unaendelea. Hata sasa hivi Mhe. Mwenyekiti mimi kama utatoka na Wajumbe au utapeleka mtu yeyote ende kuthibitisha ukifika utaona kwamba kuna tofauti baina ya kazi ambayo imefanywa na mimi mwenyewe binafsi nimepita.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Mhe. lakini vile vile Jaku Hashim Ayoub alitaka kujuwa ni maafisa wangapi ambao walichukuliwa hatua kwa kushindwa kutimiza wajibu wao. Niseme Mhe. Jaku Hashim Ayoub kwamba hakuna taarifa sasa hivi ambayo kwamba kuna mtu ameshindwa kuchukua au kutekeleza wajibu wake kama ambavyo labda Mhe. Jaku utakuwa unataarifa na kama taarifa hizo zipo Mhe. Jaku Hashim Ayoub serikali ipo na serikali ipo kwa kuendelea kuajibika kwa wananchi. Kwa maana hiyo kama una ushahidi kama kuna mtu hatimizi wajibu wake vizuri naomba utusaidie tu lengo na madhumuni ni kwamba tunataka kuona sisi wananchi wanapata huduma kama vile ambavyo serikali imeelekeza

kwamba wananchi wapate huduma si vyenginevyo. Kwa hiyo kama kuna mtu sasa hivi hakuna hatua ambazo naweza kuzizungumzia hapa sina taarifa ya mtu ambae ameshindwa kutimiza wajibu wake.

(b) Mhe. Mwenyekiti, serikali anaona kwamba uzoefu unaonesha kwamba haiwezi kufanya biashara naomba nikanushe, sisi pale kiufupi ni kwamba hatufanyi biashara lakini tunatoa huduma, serikali inaendelea kutoa huduma haifanyi biashara pale. Kwa hiyo kama wafanyabiashara wao wanafanya biashara wameshindwa kufanya biashara Mheshimiwa atusaidie kwa kuwa na yeye ni mdau au ni muhusika wa majimbo yale ya mjini na utetezi wake mara nyingi unaonekana uko hivyo basi tunaomba atusaidie tu kwamba kuwaelimisha wananchi wafanyebiashara kwa mujibu wa sheria za serikali na serikali inavyoelekeza.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kweli kuhusu soko kwamba kwa namna gani linaweza kubinafsishwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub nimwambie kwamba nakushukuru sana ni ushauri umeutoa lakini kwa sasa hivi hatujaa na mpango wa kufanya ubinafsishaji wa soko lile na badala yake utaratibu utaendelea kutumika ukabaki vile vile ambavyo utakuwa upo.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Kuhusu utaratibu Mhe. Mwenyekiti

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Jaku Hashim Ayoub kaa kitako

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, nami kwa kunipa nafasi kuweza kuuliza swali la nyongeza, kwanza kabla sijauliza swali naomba nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kwa majibu yake mazuri lakini naomba nimuulize swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:

(a) Kwa kuwa ndani ya jibu lako Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ umekiri kusema kwamba soko hilo ni chafu na linaweza kuhatarisha maisha ya wananchi waliopo pale ambao wanatumia. Kwa kuwa mzigo huu baada ya kutokea maradhi ya miripuko unarudia kwenye serikali, yaani serikali inapata mzigo je, ni sababu gani zinazopelekea kwamba soko hilo kwa sasa hivi wakati ni chafu lisifungwe mpaka pale ambapo kwamba litafanyiwa marekebisho mazuri wananchi wakaachiwa kutumia.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Khamis Bakari swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba soko lile pale nakubaliana na mawazo ya Mhe. Mwakilishi kwamba ni chafu na kama nilivyokiri kwenye jibu langu, lakini Mhe. Ali Khamis Bakar ni kwamba hatujafikia hatua ya kwamba kulifunga soko kwa sasa hivi,

kwasababu bado ya kwamba ni chafu lakini hatua za dharura tumeanza kuzichukua na nikuona kwamba sasa hivi huduma ya maji inapatikana, nadhani hata hivyo na hatuwa nyengine zitafuata kwa kuendelea na ukarabati huu ambao kama nilivyosema kwamba ujenzi tayari umeshaanza kwa hatua hiyo ya kushirikishana kati yetu sisi na wafanyabiashara wenyewe. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi pia nimpongeze sana Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ kwa jibu lake zuri la ukweli kabisa na hakuna mtu mzuri katika ulimwengu huu kuliko anaekubali makosa yake.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana kwamba soko la Darajani chafu na wafanyabiashara wengi wanafanyakazi nje kabisa ya soko lile hasa nyakati za jioni. Je ili kunusuru afya za wananchi wetu wizara ina mpango gani wa makusudi kuweka meza pale maalum katika biashara zile ili afya za watu wetu wanapokwenda kununua bidhaa ziwe salama.

Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ: Mhe. Mwenyekiti kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, naomba niendelee kusema kwamba naendelea kukiri hali hiyo, lakini vile vile niombe niseme kwamba katika eneo ambalo limezungumziwa mara nyingi sana likionekana kama ni chafu ni sehemu ya ndani ya kuuzia bidhaa mle ndani katika soko letu hususan katika sehemu za kufanya biashara ya samaki pamoja na sehemu za kuuzia mabanda yale ya kuku zaidi na sehemu za nyama.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa upande wa pale nje bado mazingira ya pale hayaoneshi kwamba yana uchafu ambapo wananchi wanafanya biashara zao hususan wakati wa jioni. Lakini kwa kuwa ni ushauri, swali lake limekuja katika ushauri kwamba ushauri wa kuangalia kuweka juu ya meza tutaangalia kutokana na kwamba mji ule unautaratibu wake ni kwamba tunaweza tukaona kamba ni nimna gani tunaweza tukafanya ili kuweka katika mazingira ya usalama zaidi kwa wafanyabiashara wetu pamoja na wananchi, lakini nitowe hofu kwamba Mhe. Ali Suleiman Ali tunaendelea na taratibu za kuona kwamba tunajitahidi pamoja na mazingira hayo na tukiona kwamba Baraza la Mji litachukuwa hatua kunusuru hali ya uchafuzi isije ikaleta madhara zaidi katika kufanya usafi ule ambao tunaweza kuufanya wa *day to day.* Mhe. Mwenyekiti ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kutokana na majibu niliyoangalia kwenye swali naona bora hili swali niliondoshe maana yake nishadanganywa tena kwa dhahiri kabisa kwa hiyo bora kwa uwezo wa Naibu Waziri tusije tukagombona bora niliondoe, maana yake humu nishadanganywa tena.

Nam. 75

Maendeleo ya Ujenzi wa Mtaro wa Kisima Majongoo

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

Nam. 145

Utaratibu wa Kuongezwa Mikataba ya Ajira Wastaafu

Mhe. Jaku Hashim Ayoub – Aliuliza:

Sheria yetu ya Utumishi wa Umma na kanuni zake imeweka utaratibu wa mtumishi wa umma anapofikia umri wa kustaafu na kama bado ujuzi wake adimu na unahitajika huongezewa muda wa utumishi kwa utaratibu maalumu.

(a) Je, kwa vile soko la ajira limejaa wataalamu wa fani mbali mbali na nafasi za ajira ni chache kwanini utaratibu wa kuongezewa muda wastaafu usiondolewe ili kupisha vijana wenye fani hizo waingie kazini.

(b) Badala ya kuwa na utaratibu wa kuongeza muda wastaafu kwanini Serikali isiweke mpango maalumu kwa wanaostaafu kutumia miaka mitano ya mwisho ya utumishi wao kutoa ujuzi kwa vijana wapya watakaochukuwa nafasi hizo.

(c) Kwa nini kada zile ambazo zinachukua muda mrefu kujifunza kama vile udaktari watumishi wake wasiongezewe umri wa kustaafu kufika miaka 70 badala ya 60.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake Nam. 145 lenye vifungu (a), (b) na (c) naomba kwanza kutoa maelezo mafupi yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, mtumishi wa Umma anaweza kustaafu kwa hiari anapofikia umri wa miaka 55 baada ya kukubaliwa na Tume ya Utumishi husika na kwa mteuliwa wa Mhe. Rais anaweza kustaafu kwa hiari baada ya kuwasilisha ombi lake kwa Mhe. Rais kupitia kwa Katibu Mkuu Kiongozi. Aidha, mtumishi wa umma kwa mujibu wa kifungu nambari 44 cha Sheria ya ajira namba 11 ya mwaka 2005 anatakiwa kustaafu kazi kwa lazima pale anapofikia umri wa miaka 60.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Jaku Hashim Ayoub swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kwamba soko la Ajira limejaa wataalamu wa fani mbali mbali na nafasi za ajira ni chache. Hata hivyo,

Watumishi wa Umma waliofikia umri wa kustaafu kwa lazima huongezewa muda wa ajira kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma kifungu nambari 60(2) pale Wizara inapoona muajiriwa huyo anahitajika kulingana na ujuzi alionao na ni vigumu kumpata mtaalamu wa fani yake. Utaratibu unaotumika ni kuwa Wizara husika ndio inayoomba kuongezewa muda wa utumishi wa umma wa mtumishi huyo. Baada ya kukamilika kwa utaratibu huo, Tume ya Utumishi husika inaweza kuidhinisha nyongeza hiyo kwa muda usiozidi miaka miwili.

(b) Mhe. Mwenyekiti, ili kudhibiti utaratibu wa kuongeza muda wa watumishi waliofikia umri wa kustaafu kwa lazima, Serikali imechukua hatua za Muongozo wa Uandaaji Viongozi (*Succession Plan*), Muongozo ambao umeweka utaratibu wa Mtumishi wa Umma kabla ya miaka mitatu kufikia kustaafu, atatakiwa kuhamisha ujuzi wake huo kwa watumishi wanaofatilia.

(c) Mhe. Mwenyekiti, ili kuongeza muda wa kustaafu kwa watumishi wa Umma wakiwemo Watumishi ambao kada zao zinachukua muda mrefu wa kujifunza pamoja na Watumishi wengine wa Umma itabidi kufanyike marekebisho katika Sheria mbali mbali zikiwemo Sheria ya Ajira Nam 11 ya mwaka 2005, Sheria ya Utumishi wa Umma Nam. 2 ya 2011 na Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Nam 2 ya mwaka 1998 ambazo zimeweka masharti ya ukomo wa Utumishi na ulipaji ya mafao ya Uzeeni. Nashukuru.

Nam. 184

Vijana Kuiga Tamaduni za Nje

Mhe. Jaku Hashim Ayoub– Aliuliza**:**

Mnamo tarehe 16/3/2018 Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo alitoa kauli kupitia *ZBC* kwa vijana wa Zanzibar kuacha kuiga tamaduni za nje na kufuata mila na tamaduni za Kizanzibari.

(a) Je, ni tamaduni gani hizo ili vijana wakapata kuzielewa.

(b) Hivi sasa kumezuka mtindo wa vijana wetu wa kike na kiume kuvaa mavazi ya ovyo sana kama vile nguo fupi za kubana, suruali mlegezo na kadhalika. Je, hatua gani zinachukuliwa kupiga marufuku mavazi ya ovyo kama vile wenzetu Rwanda walivyofanya.

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo - Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, napenda kumjibu Mhe. Jaku Hashim Ayoub swali lake namba 184 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar inasifika kwa kuwa na utamaduni mzuri ambao umekuwa ndio kivutio cha watu na mataifa mbali mbali kwa kuja na kujifunza kupitia Wazanzibari

wenyewe. Utamaduni huo ndio hupelekea watu kuweza kuheshimiana, kusalimiana, kusaidiana na kushirikiana katika mambo mbali mbali ya kijamii bila kujali ni mtu wa aina gani.

(a) Mhe. Mwenyekiti, mila, silka na desturi za Wazanzibari ni vivutio vikubwa kwa wageni wanaotembelea Zanzibar, mfano maamkizi, kuheshimiana mkubwa kumuheshimu mdogo na mdogo kutoa heshima kwa mkubwa, mavazi yenye heshima ambayo huvaliwa na Wazanzibari yenye kutoa taswira ya kuthamini hadhi ya kila mtu au jinsia, mazungumzo yenye heshima ambayo huzungumzwa kati ya mkubwa na mdogo na ukarimu.

(b) Mhe. Mwenyekiti, ukweli ni kwamba katika jamii yeyote au Taifa lolote lazima kutakuwa na watu au kundi la watu ambao wanafanya mambo kwa kuiga au hufanya kutokana na utashi wao kulingana na umri, wakati na mazingira ambayo wanaishi. Kwa kulifahamu hili Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeamua kwa makusudi kuunda wizara ambayo itahusika na masuala hayo ya kulinda na kuhifadhi utamaduni ili vijana waweze kuishi na kufanya mambo yao kulingana na utamaduni wao na sio ule wa kuiga na kufanya kwa utashi wao. Aidha, hivi sasa wizara ipo katika hatua za kuifanyia mapitio Sera ya Utamaduni na baadae kuifanyia mapitio Sheria ya Utamaduni ya mwaka 1973 ili kukidhi haja ya mazingira ya sasa na kulinda utamaduni na kuelezea aina ya mavazi yanayokubalika katika jamii ya Kizanzibari pamoja na vazi la Taifa.

Nam. 31

Matokeo ya Tafiti Zinazohusiana na Uvuvi Zanzibar

Mhe. Ali Suleiman Ali (kny. Mhe. Shehe Hamad Mattar) – Aliuliza**:**

Kwa kuwa Wizara ililiarifu Baraza lako Tukufu, kwamba imetayarisha Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Uvuvi (*Fisheries Master Plan*) na ilieleza kuwa inashirikiana na Taasisi za TAFIRI, IMS, na SUZA kwa utafiti na kupata faida kubwa ya kuunyanyua uchumi wa Zanzibar.

(a) Je, mpango huo umeleta matokeo gani kwa faida ya Zanzibar katika nyanja ya uvuvi hadi sasa.

(b) Je, matokeo ya tafiti zilizofanywa na taasisi za TAFIRI, IMS, na SUZA yamefanyiwa kazi vipi hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 32 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyekiti, Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Uvuvi *Fisheries Master Plan* bado unaendelea kufanyiwa kazi na mshauri mwelekezi na atakapomaliza hatua itakayofuata ni kuwasilisha serikalini kupitia wizara yangu.

Hivyo, naomba kulijuulisha Baraza lako kuwa hadi kufikia mwishoni mwa mwaka 2018 Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Uvuvi *Fisheries Master Plan* tunategemea utakuwa umekamilika na tutauwasilisha rasmi.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kupitia mradi wa *Swiofish* ulioanza mwaka 2015 hadi 2021 kwa awamu ya kwanza tunazo tafiti mbali mbali tutakazoshirikiana na taasisi za Tafiri, IMS na Suza, na zaidi katika mambo yafuatayo:-

1. Sensa ya uvuvi

2. Uelewa wa mazalio, tabia, uvuvi wa aina za samaki tofauti kama vile pweza, jamii ya vibua, jamii ya samaki wa matumbawe na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, kazi hizi za tafiti bado zinaendelea na matokeo yake yatapatikana baada ya miaka miwili hadi mitatu.

Hivyo, naomba kuliarifu Baraza lako kuwa matokeo ya tafiti hizo tutayawasilisha mara tu baada ya kukamilika. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali ya nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, tafiti ni jambo muhimu sana kwa kujua kilichokuwemo katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu hasa katika sehemu ya uvuvi. Lakini tafiti hizo tumeambiwa tu kwa sensa ya uvuvi ya miaka miwili hadi mitatu itatoa ufafanuzi baadae swali langu liko hapa.

Je, kwa sasa katika tafiti hizo zimefanyika sehemu gani katika Zanzibar yaani Unguja na Pemba maeneo gani zilifanyika tafiti na imepatikana faida gani tukaelezwa hapa ili wananchi wajue.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa idhini ya Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi naomba kumjibu Mhe. Shehe Hamad Mattar aliuliziwa kwa niaba na Mhe. Ali Suleiman Ali swali lake ya nyongeza kama ifuatavyo:

Kwanza nampongeza sana amesifu tafiti, tafiti ndio kitu cha muhimu sana katika kuendeleza maendeleo ya kitu chochote. Kwa hiyo, hongera sana kwa kulijua hilo na hongera sana kwa kutaka kuhakikisha kwamba utafiti unafanyika na akataka kujua maeneo yanayofanyika uvuvi.

Maeneo yanayofanyika uvuvi ya utafiti ni yale maeneo ua Bahari Kuu yote na hata maeneo ya karibu karibu na Bahari Kuu ili kujua aina za samaki na mazalia yake kama tulivyoeleza hapo juu. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa kuniona lakini nimshuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa kujibu maswali mazuri sana yale ya msingi na haya ya nyongeza. Lakini pamoja na hayo nina swala moja lenye kifungu a na b kwa ufupi sana kama ifuatavyo:-

(a) Kwa sababu Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba utekelezaji wa *Master Plan* unaendelea. Nilikuwa nataka kujua mshauri muelekezi ametoka katika taasisi gani na lini itamalizika.

(b) Kwa kuwa tafiti moja kati ya tafiti zote zilizofanywa chini ya *Swiofish* ni jinsi ya kufanya mwani uwe chakula cha kuku na imetoa muelekezo mzuri sana na matokeo mazuri sana. Ni lini wizara ita-*launch* ili wananchi wajue wapate chakula cha kuku kwa urahisi zaidi.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. wenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mohamed Said Mohamed huyu ni bingwa wa uvuvi huyu alikuwa Naibu Waziri wa Uvuvi na mambo haya kayaanzisha yeye. Kwa hiyo, tutamjibu vile ambavyo tunaendeleza.

Kwanza kabisa kataka kujua mshauri muelekezi ametoka wapi?

(a) Mshauri muelekezi kwa kweli huyu ametoka katika Taasisi za Kimataifa za uvuvi na ana sifa za kimataifa za uvuvi.

(b) Kuufanya mwani chakula la kuku, ni suala zuri ni kweli kwamba mwani unaweza kuufanya chakula cha kuku, mwani unaweza kufanya peremende unaweza kufanya mambo mengi sana unaweza kutumia na hata ukaufanya kachumbari pia unakwenda vizuri.

Sasa hili suala la kufanya mwani uwe chakula cha kuku tumo katika harakati za kutaka kufanya hivyo na kwa sababu mwani wenyewe bado haujatosha sana tunataka tuuze nje wananchi wapate fedha na wale wanaofanyakazi hiyo ya kusafirisha mwani nao wapate pesa ili waendeleze.

Kwa hiyo, bado hatujaanza hasa kutengeneza chakula cha kuku kutokana na mwani, lakini mipango ipo ya kutengeneza vyakula vya kuku hapa nchini ili mifugo yetu ya kuku iweze kupata chakula kutoka hapa kuwapunguzia bei wananchi katika kununua vyakula hivyo vya kuku. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 61

Shirika la Biashara la Taifa la ZSTC

Mhe. Omar Seif Abeid– Aliuliza**:**

Shirika la Biashara la Taifa *ZSTC* ni Shirika linalojiendesha kibiashara na hivyo, ipo haja ya *ZSTC* kuwa na ofisi ya kudumu sambamba na kufungua maduka ya bidhaa zake zinazozalishwa na shirika hilo huko Tanzania Bara. Lakini hadi leo Shirika la Taifa la Biashara haina hata nyumba na inaendelea kukodi nyumba kutoka Shirika la Nyumba *NHC*.

(a) Je, *ZSTC* imejipangaje ili kuhakikisha kwamba inamiliki jengo lake na Ofisi.

(b) Je, kuna utaratibu gani kwa *ZSTC* kuanzisha maduka kwenye mikoa mengine ya Tanzania Bara kuuza bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyake.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda - Alijibu**:**

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 61 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Ni kweli *ZSTC* hivi sasa wanaendesha biashara zao katika nyumba ya kukodi ya *NHC* ambayo gharama zake ni kubwa. Kwa kuona umuhimu wa kuwa na Jengo la Kibiashara Shirika kupitia Wizara ya Biashara na Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais limo kwenye mazungumzo na wenzetu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupatiwa Jengo la *NHC* ambalo kwa sasa linatumiwa na shirika kwa kubadilishana na jengo lililokuwa la Bizanje lililopo Mizingani Mjini Unguja.

(b) Kwa upande wa kufungua maduka mengine kwa ajili ya kuuza bidhaa za Shirika, Shirika bado linaona kufanya hivyo ni kujiongezea mzigo kwani mahitaji ya mafuta kwa ujazo mkubwa ni makubwa kuliko uwezo wa uzalishaji wa shirika kwa sasa. Hata hivyo, shirika linafikiria kupanua zaidi biashara zake hadi kufikia mikoa mengine ya Tanzania Bara pale hali ya uzalishaji wa mafuta hayo utakapoimarika. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru na pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na jawabu fasaha. Nilikuwa na swali ya nyongeza lenye kifungu a na b kama ifuatavyo:

Kwa kuwa waziri umekiri kwamba shirika linaendelea kukodi jengo hilo kutoka *NHC* na kwa sababu ni siku nyingi sasa tumeendelea kukodi kwa bei kubwa.

(a) Sasa nataka nijue ni bei gani hasa *ZSTC* inayoilipa *NHC* kwa ajili ya nyumba hiyo na hatua gani imefikiwa katika mazungumzo hayo yanayohusiana na kubadilishana majengo kati ya *ZSTC* na *NHC* ili kuiwezesha *ZSTC* kuondokana na mzigo mkubwa unayoilipia nyumba hiyo.

(b) Je, ni chanamoto gani inayoikabili *ZSTC* hata wakashindwa kuzalisha zaidi ili hali soko la bidhaa hizo wanazozizalisha za mafuta wa ujazo mkubwa upo. Ahsante sana Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake la nyongeza kama ifuatavyo lenye kitoto (a) na (b).

(a) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu bei ni kiasi gani shirika linalipa kwa *NHC* suala hili naomba nimjibu kwa maandishi.

(b) Ni kiasi gani, lakini hatua gani na changamoto kwa uzalishaji mdogo. Mhe. Mwenyekiti, nataka kumueleza Mhe. Mwakilishi kwamba kiwanda tulichonacho Pemba kidogo ni kiwanda cha zamani lakini baada ya serikali kuja na sera ya viwanda tayari tumeshaingia mkataba na Taasisi moja ya biashara ya China kukiimarisha kiwanda pamoja na kuwahamasisha wakulima kulima bidhaa nyingi za biashara za mafuta kwa mfano makonyo ili tuweze kupata mafuta mengi na kiwanda kiwe kiwanda bora kiwanda imara tuweze kuuza ndani na nje ya nchi.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri na mimi ningependa kumuliza swali moja dogo lenye vifungu (a) na (b).

Kwa kuwa Shirika hili la *ZSTC* kazi yake kubwa ni kuuza biashara na kuengeza pato la serikali na kwa kuwa ina ofisi kule Dubai ambayo haina wafanyakazi wazalendo ningependa kujua (a).

(a) Ni lini shirika hili litapeleka wafanyakazi wazalendo pale ili kukuza biashara ile kwa sababu ya uchungu wa serikali yao na kuingiza pato kubwa zaidi.

(b) Kwa kuwa yule aliyepo pale ni mgonjwa kwa muda mrefu shirika lako lina mpango gani wa kutafuta afisi nyengine pale ya kuendeleza biashara ile. Ahsante.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Ningemuomba kidogo Mhe. Mwakilishi arejee suala b.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa Mjumbe rudia swali la b.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Kwa kuwa yule aliyeko pale Dubai ni mgonjwa kwa muda mrefu sasa ni lini shirika hili litaboresha afisi ile hasa kupeleka Wazalendo wenye uchungu wa nchi hii kwa kuongeza pato kubwa la serikali ya nchi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa naomba kumjibu Mhe. Hamad Abdalla Rashid swali lake la nyongeza lenye (a) na (b) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, nitaanza na swali (b).

Mhe. Mjumbe anauliza lini yule aliekuwepo pale Dubai wanaofanya kazi pale wataondoka ili wapelekwe wazalendo.

(b) Mhe. Mwenyekiti, suala hili tulipolijibu tulisema hivi. Katika nchi yoyote ile lazima aweko mtu ambaye anajua mazingira ya nchi, anajua lugha ya nchi kwa sababu lengo ni kutafuta masoko. Kwa hivyo, si tatizo kumpeleka mtu kutoka hapa lakini je, anajua mazingira ya pale, je, ataweza kuwatafuta whao wateja.

Kwa sababu ujue ni *marketing, element* moja ya *market* ni kuoongea lugha ya ile nchi ambayo unaifanyia *market* ile. Sasa na sheria ya *market* lazima aweko mtu mwenye kujua utamaduni wa watu wa aina ile unaotaka kuwauzia.

Kwa maana hiyo, Mheshimiwa kama serikali itaona inabidi kumpeleka mzalendo na atakuwa na tija kwa kazi tunayoifanya pale Dubai tutampeleka. Lakini kwa sasa tunae mtu yule tunamtumia na wanafanyakazi vizuri tunashukuru katika kuziuza karafuu zetu kama unavyojua karafuu zetu ni *grade* ya mwanzo na tunaziuza kwa wingi pale.

(a) Mheshimiwa wafanyakazi wazalendo hatuna tatizo na kupeleka wafanyakazi wazalendo. Lakini kama itahitajika lazima kummpeleka mzalendo tunawapenda wananchi wetu, lakini pia tunataka kuuza karafuu zetu kwa wingi ili tuongeze uzalishaji nchini kwetu. Kwa maana hiyo, kama itahitajika kumpeleka lazima apelekwe mzalendo tutampeleka lakini kwa sasa bado.

Mhe. Amina Idd Mabrouk: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swala la nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri umekiri kwamba Shirika la *ZSTC* linatumia nyumba ya kukodi la *NHC* na inatumia pesa nyingi. Je, Mhe. Naibu Waziri unaweza ukatwambia kwamba kwa muda gani sasa umekodi katika nyumba ile ya *NHC*.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda naomba nimshukuru sana Mhe. Amina Idd Mabrouk kwa suali lake zuri la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, swali lake anauliza tunakuwa tunakodi kwa kipindi gani sasa.

Mhe. Mwenyekiti, nyumba ile tunakuwa tunakodi kwa kipindi kirefu lakini tumeona jinsi gani tunatumia pesa nyingi na naomba tushukuru sote tumeanzisha jitihada makusudi ya kutaka nyumba ile kubadilishana na nyumba ya hapa ya Bizanje ili NHC watupe nyumba ile, hii ni baada ya kuona kwamba tunatumia pesa nyingi na hatuko tayari serikali kutumia pesa nyingi kwa sababu pesa zetu ziende katika maendeleo, hilo tumeliona na Mheshimiwa naomba utushukuru tutalifanyika kazi na *inshaallah* tutafanikiwa katika kubadilishana nyumba ile wao tuwape ya Bizanje na sisi tuchukue ile.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante waheshimiwa wajumbe maswali yamemaliza.

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa Fedha 2018-2019 - Wizara ya Biashara na Viwanda

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe majadiliano yanaendelea na kwa sasa mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa Mhe. Jaku Hashim Ayoub akifuatiwa na Mhe. Simai Mohammed Said.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Mhe. Mwenyekiti, kwanza msema kweli mpenzi wa Mwenyezi Mungu na tunapohoji serikali narudia tena kwa mujibu ya Katiba ya Zanzibar kifungu cha 88, na hii ndio katiba mama ya nchi 88 kazi za Baraza la Wawakilishi, Baraza la Wawakilishi pamoja na kuongoza shughuli zake kutokana na kifungu cha katiba hii litafanya kazi kwa mambo yafuatayo utekelezaji kama muakilishi:-

a) Kutunga sheria pale utekelezaji wa jambo unapohitaji kuwepo kwa sheria hiyo.
b) Kujadili shughuli za kila wizara wakati wa kila kikao cha mwaka wa bajeti wa Baraza la Wawakilishi.
c) Kuuliza masuala mbali mbali ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar katika Baraza la Wawakilishi.
d) Kuidhinisha na kusimamisha mipango ya maendeleo ya serikali katika njia ile ile ya mwaka ya kuidhinishwa hii ni moja ya katiba yetu ya Zanzibar Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya mamlaka ya Rais ndio itakuwa na uwezo kufanya maamuzi ya sera ya serikali kwa ujumla mawaziri chini ya uongozi wa Makamu wa Pili Rais watawajibika kwa pamoja katika chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi.

Kuhusu utekelezaji wa shughuli za serikali za Zanzibar maelezo ya kifungu (4)(5) hayatakamilika kuhusiana hii Katiba ya Zanzibar ndio inayotuongoza Mhe. Kwa hivyo tunapohoji serikali ni wajibu wetu kama wawakilishi kwa mujibu wa kanuni ya Zanzibar.

Baada ya maelezo hayo kwanza nimshukuru sana Mhe. Waziri naweza kusema waziri mzoefu au kwa lugha nyengine ni mkongwe Mhe. Amina katika mawaziri humu nikiwatazama mimi nafikiri sijui kama yuko anayeweza kukaribia kwa uzoefu wako Mhe. Waziri. Hii Wizara ya Fedha na Biashara ziko karibu sana Wizara ya fedha huwezi kufanya fedha bila ya kuwa na biashara kwahivyo ulipofika hapa inatokana na uzoefu wako na umakini wako.

Nikusifu sana Mhe. Waziri kwa uzalendo wa Zanzibar nikupongeze sana miongoni mwa mawaziri wenye uzalendo wa Zanzibar nikufisu sana Mhe. Waziri sana tena nikutakie kila la kheri kwa uchungu wa nchi hii. Mhe. nitakuwa sijafanya haki Katibu wako Mkuu ni kijana ambaye nilimkuta Wizara ya Kilimo wakati huo kipindi changu cha mwanzo nilimjua utendaji wake Dkt. Juma nafkiri kama sikosei, ni miongini mwa katibu bora

maana yake na nilimuona katika Wizara ya kilimo ni mpiganaji mzuri kabisa, lakini itakuwa sijafanya haki hata watendaji wako Mhe. Waziri wa vitengo vyote niliwahi kufaya kazi wizara hii najua vijana hawa jinsi wanavyojituma.

Mhe.Waziri kuna kitengo hichi ndio nitahitaji maelezo kidogo *Online Register System* ambacho kinategemea kuanza, huu ni mfumo wa kusajili taasisi za biashara kwa kutumia mtandao wa mfumo wa *online* na mali zisizohamishika. shida yangu Mhe. waziri serikali imejipanga vipi kuwezesha kusimamia mfumo huu kwa sababu usimamizi pia una gharama. Bajeti iliyokuwepo hapa nafikiri haihitaji Mhe. Waziri, ni jambo zuri mtu anaweza kujasili hata yupo nyumbani kwake yupo popote ni jambo la kupongeza sana serikali kwa hili inapunguza msongamano, tafauti na ile ya mambo ya *registration* ya mtoto wa *register* kwenda kuchukua cheti, unatoka Nungwi au Makunduchi shilingi 4000 gari kwenda ukifika pale cheti hujakipata ukienda PBZ unapanga foleni, inakuwa mwananchi tunamuumiza. Kwa hivyo, nikushukuru sana Mhe. Waziri kwa *fomular* hii lakini hii bajeti haikidhi nilivyoiona mimi.

Ni jambo la kupongeza sana Mhe. Waziri huu ndio ubunifu sio unatoka Makunduchi unataka cheti cha mtoto unakwenda kukaa foleni PBZ kwa shilingi 2000 nauli shilingi 4000 kurudi hujajua kutwa nzima ile siku unapoteza jambo la kupongeza.

Tuje kunako wataalamu Mhe. Waziri maslahi yakoje, uzoefu watu wengi wakishapata wanaondoka maslahi ya hawa yakoje, kitu cha utaalamu tuna uzoefu huko nyuma baadae wataalamu wanatukimbia maslahi yakoje, kwa jambo hili nitahitaji maelezo ya serikali mara nyingi inapotoza ghamara baadae watumishi wanaondoka.

Nije kunako kiwanda kile cha *cortex* kimekaa muda mrefu hakuna kinachoendelea Mhe. waziri hebu ukija nieleze nini nia ya serikali au madhumuni yake nini yaliyokusudiwa miaka mingi pale dude limekaa.

Mhe. nije kwenye changamoto ya Muungano wizara yako imegusa na nikushukuru sana hili umelisimamia uzuri sana kuhusu bidhaa za Zanzibar kwenda Tanzania Bara, Mhe. kitu cha kushangaza sana mali inayotoka Burundi, Zambia, Uganda, Congo mafuta yale katika bandari ya Dar-es Salaam TPA wana-*charge* dola 3 nafikiri mawaziri mtakuwa shahidi na mimi sio mkalifu, mkamilifu mmoja tu. Nitapokosea niko tayari kukosolewa kwanini wanatozwa dola tatu sisi Zanzibar tumeungana na wenzetu Tanzania Bara tukatozwe dola 10. Nishaliuliza bungeni na serikali ikakiri ya Jamhuri ya Muungano, Muungano wa aina gani huu mali ya Uganda, Mali ya Zambia, Mali ya Congo ya Ruandwa dola 3 sisi tumeungana na ndugu zetu dola 10.

Mafuta kule Bara ni rahisi kuliko hapa kwetu hii moja changamoto ya kero ya Muungano kwa hii bidhaa hizi inakuwaje leo sukari yetu inataka kwenda Tanzania Bara imekuwa kigugumizi. Soko la Afrika Mashariki tunashindwa kulitumia leo bia, maji, saruji, nondo zinatoka Mhe. Waziri naomba uwe makini sitaki kugombanisha lakini kama mimi hunipi wewe pokea haiwezekani tufike pahali hii *fomular* iwe vizuri. Sasa mtajua nyinyi kama mtazuia au mtafanya njia gani. Nipe nikupe jazwa ujazwe hasa ndio yale niliyorudia imekaa kama lugha ya kiarabu, kiarabu ukiandika inavutia kwako leo mfanyabiashara

mmoja tu Zanzibar kachukua TV akafila katika bandari ya Dar -es Salaam TV kanunua shilingi 100,000 anaambiwa alipe shilingi 200,000 kaichukua TV mwisho kaivunja uchungu Zanzibar ukiacha karafuu utalii, biashara.

Bila ya kuficha naomba nisikilizwe kwa makini hapa Zanzibar tumekuwa ni chuo matumizi ya dola tumeanza kutumia sisi mwanzo kuliko Tanzania Bara, vyama vingi vimeanza Zanzibar kabla ya Tanzania Bara. Kwa wenzetu watanzania Bara, Watanganyika wamesoma kutoka kwetu. Soko la biashara limenza Zanzibar sasa tunafika wakati mawaziri munatukwanza tusije tukafika pahali tukateleza Ramadhani hii lakini mawaziri muwe *serious.* Ndio yale aliyosema Mhe. Rais musikae maofisini tu leo tunapigana huko leo Zanzibar pahali pa kupiga hatua sana mali ya Zanzibar ikiingia Bara utafikiri umeleta unga, lakini mali inayotoa Zambia, inayotoka Uganda inayotoka Kenya haina madhara tunafanya nini tumeungana namna gani? Lazima pawe pana *fomular* biashara ni kitovu kikubwa Zanzibar. Zanzibar ina historia kubwa ya biashara leo mali ikitoka Bara huku haina tatizo yetu ikiingia kule aaa! Hii *no* waziri nakuamini sana na nimeona mimi utendaji wako sana nikupongeze sana sana.

Hii biashara itatusokota fanya ukae na Waziri Mujage leo biashara kiwanda kiko Tanzinia wala hikiko Burundi sukari inatoka wapi inaingia Tanzania Bara yetu inatoka hapa yule muekezaji kapata shida kubwa sana, yule kama kafufua maiti kafufua Kiwanda cha Mahonda, serikali inahitaji imlinde kile kiwanda kimefanya kazi kubwa sana.

Niipongeze serikali kupitia Mhe. Rais Ali Mohammed Sheni nafikiri zile nyumba zake zisharudishia ilikuwa nyumba zake aliwahi kuzuiwa mle nafikiri keshakabidhiwa kuwa kiwanda cha sukari lazima kilindwa matafute *alternative* ya kumsaidia yule mtu kafanya kazi kubwa vyenginevyo tutakuja kushindwa kuweka wawekazaji hapa. Kiwanda kile kina genereta naamini Zanzibar nzima inaweza ikaendesha genereta lake, yule maiti ndio kashafika kafufua kazi kubwa tufike pahali tumfikirie leo mali ukienda pale ahh! hayasemeki.

Mhe. nije katika biashara ya fedha za kigeni na hapa msikilize sana Mhe. Waziri kwa lugha nyepesi na laini huwezi kufanya biashara bila ya kuwa na pesa wafanyabiashara wetu wananyanyasawa au wanateseka au wanapata usumbufu, lugha tatu nimetumia kunyanyasika, kupata usumbufu, na waziri wa fedha nafikiri hayupo watu wanakamatwa na dola 20,000 anakwenda bidhaa dubai 30 na sheria nafikiri haipo wenzetu Tanzania Bara wana *fomular* hili waziri nakuomba sana mimi nakuamini sana ulitokea waziri wa fedha na utendaji wako naujua lazima tuweke *fomular* na hapana sheria kama pana kanuni mtueleze.

Leo mtu ana dola za 20,000 enaenda kununua buibui, hijabu huwezi kutuma TT maduka tufauti wananyanyasika wafanya biashara hii na zipo pesa nafikiri juzi tu zimerudishwa Polisi wanazichua wanakwenda pahali hawafikii muafaka na sheria nafikiri hapana TRA washazungumza suala hilo lazima uweke wazi utakapokuja Mhe. Waziri unipe maelezo ambayo ni mazuri kabisa, wanateseka wanasumbuka huwezi kufanya biashara. Huku nguruwe haramu lakini mchuzi wake unaunywa sio halali, biashara ni fedha, fedha ndio biashara na hii serikali isingelikuwa madarakani bila ya kuwa na wananchi wananachi

ndio serikali, kwa hivyo waziri hapa umekifahamu nilichozungumza wananyanyasika kwa hivyo nataka fomular na utaratibu maalum kakae na waziri wa fedha utakapokuja kunijibu unijibu vyenginevyo biashara hiyo haiofanyiki mapato yatapungua pawe na *fomular* maalum.

Mhe. nije katika masoko na zamani ilikuwa ikiitwa Wizara ya Biashara Viwanda na Masoko kama sikosei. Mheshimiwa leo nilikuwa na swali hapa nililoliondoa hapa Na 75 Naibu Waziri alitaka kunipa kitu ambacho hakielekei. Muda mrefu sasa umepita ujenzi wa mtaro wa Kisimamajongoo bado hakuna hatua za maana zilifikia licha suala hili kuulizwa hapa Barazani muda mrefu, hatua gani za maana zimechukuliwa kwa mtaro huu wa Kisimamajongoo. Kumekua na mtaro ule ule usijengwe anakuja kunijibu Naibu Waziri utacheka ndio nikaamua kuliondosha.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Manispaa la mjini kwa sasa halina mpango wa kujenga msingi wa maji wa mvua uliopo Kisimamajongo. Msingi huo wenye urefu kilomota 2.7 uliopo hivi sasa unahitaji, sikiliza Mhe. Mwenyekiti hapo, unahitaji kufanyiwa usafi kwa kutumia vifaa maalum gari la *crane* kunyanyua mfuniko wa zege ambacho hicho kitu sio kweli, mimi naweza kulinyanyua na niko tayari kuja kuadhibiwa ndani ya Baraza hili. Sasa mawaziri na manaibu waziri tunapokwambieni mfanye utafiti mimi niko tayari kwa lolote lile, ati mtaro unataka *crane*. Mimi saa mbili nauliza swali leo eti ndio unasafishwa leo napita saa 2:30 nakuja huku na tukienda pale tutakuta watu.

Sasa mawaziri na manaibu waziri hamtufanyii haki ati tumekuja kuwambia unataka *crane* mimi naunyayua naibu waziri watukuuzeni, haya mambo sisi tunafatilia hatukuja kuropokwa humu ndani. Niko tayari kuja kuaadhimiwa Mhe. Mwenyekiti kwa hili kama huo mfuniko unahitaji *crane* mimi nanyanyua, nije nipigwe mikwaju na bukta tu humu ndani, uchi siwezi kusema maana yake kanuni haziruhusu, nije nipigwe mikwaju na bukta tu. Sasa naibu waziri mnachokifanya mnafanya vichekesho hamfatilii majukumu yenu na Rais kakuagizeni hichi chombo cha wananchi mara mbili Mhe. Rais kashazungumza hata juu huko mashahidi. Alizungumza Mhe. Jaku *kuluhaku wakulumruwa* unachozungumza ni sawa sawa wajumbe mashahidi nyinyi sasa mnafanya kitu unanambia ufuniko unataka *crane* jamani nini Mhe. Shamata *nothing*.

Mhe. nije katika kodi za ZBS *Zanzibar Bureau Standard* na *Food Drags* hapa kitengo hichi kidogo mfike pahali mkae pamoja mwananchi anakamuliwa mfanyabiashara anakamulia mara mbili hichi kakikalieni uzuri. Huku kodi hiyo hiyo ZBS inahitaji huku *Food Drags* wanahitaji, kitengo hichi mkakae pahali wafanyabiashara tunawahitaji.

Mhe. kwa kumalizia nije suala la mwani nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema aliyonipa kwenye jimbo langu karibu vijiji vyangu vyote vimezungukwa na pwani, wananchi wangu wanateseka sana suala la mwani. Mhe. Waziri wanateseka sana kwenye suala la mwani, Mhe. waziri hili nikuombe sana mlifanyie utafiti suala la mwani limekuwa muda mrefu na hili nafikiri utawafunika mawaziri wengi wameshindwa kulipatia ufumbuzi hili na ukiliweza hili Mhe. Waziri Mwenyezi Mungu atakulipa mimi sina cha kukulipa maana yake thamani ya kitu kama huu ukucha hujui umuhimu wake ndani ya kidole ukisha kutoka ndio utajua umuhimu wake.

Hili nikuombe sana tushapigwa tiktaka mara nyingi kwenye suala la mwani, katafute *formula* namna gani ya kuwawezesha wananchi wetu wanaumia ni wanyonge wa nchi hii. Sitaki kulichangia sana mwani ndio kimbilio la wanyonge Unguja na Pemba na mpaka leo halijapatikana litafutieni masoko wananchi wanaumia. Muda mrefu leo kilo 300 mia 500 kwa hivyo tafuteni soko la uhakika la wananchi, kama mlivyofanya karafuu kuzinunua tafuteni tuwasaidie wananchi wananchi ndio serikali, serikali ndio wananchi. Lazima tufikirie tusingekuwa madarakani hapa bila ya kuwa na wananachi wananchi ndio walioweka serikali, serikali ndio wananachi. Kwa hivyo suala la soko liangalie tafute njia yoyote kulitatua huu ni wimbo wa taifa wa muda mrefu na hili ukilimaliza Mhe. Waziri utawafunika mawaziri wengi humu ndani

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. muda wako umemaliza.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi sitaki kushindana na kiti chako nikushukuru Mhe. Mwenyekiti sitaunga hoja mkono mpaka nitakapopata maelezo ya kutosha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sasa naomba nimwite Mhe. Simai Mohammed Said akifuatiwa na Mhe. Nasor Salim Ali.

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsnte sana Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kwanza kwa kuanza kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini nikushukuru na wewe pia kwa kunipa nafasi hii kwa kuweza kutoa mchango wangu kwa kupitia wizara yetu hii jina jipya ambayo sasa inaitwa Wizara ya Biashara na Viwanda. Nimpongeze Mhe. Waziri kwa hutuba yake nzuri aliyoisoma pamoja na Mwenyekiti wa Kamati kwa ripoti yao yote waliyoleta ni nzuri kabisa na niwashukuru wananchi wa Jimbo la Tunguu kwa mawazo yao pia waliyoniletea ili niweze kuwasemea hapa na nitumie nafasi yangu kikatiba kuweza kuishauri serikali kwa kadri ninavyoweza.

Mhe. Mwenyekiti nikienda kwenye mchango wangu nataka nianze na ZBS Mhe. kwa mujibu wa utaratibu tuliojiwekea sasa tunakwenda katika mambo ya kimataifa lakini kitu kimoja ambacho bado kinanisumbua ni juu ya magari yetu, sasa hivi tuna wakala tayari tumeweka kwenye falme za kiarabu lakini pia nafikiria kwa ufahamu wangu wapo China ambao ni wakala ambao wanashirikiana ZBS katika kufanya kazi lakini pia katika masuala ya malipo pia. Lakini bado hatuna wakala katika upande wa Hongkong pamoja na Singapore ambao pia wazanzibari wengi tayari wamekuwa wanafanya biashara.

Sasa moja ambalo linanipa utata ni juu ya wakala ambaye yuko katika falme za kiarabu au Dubai sasa malipo mengi yanayofanyika sasa hivi wamekubaliana nafikiri na serikali au na ZBS pamoja na wakala wao ambaye yuko Dubai asilimia 70% anabakisha yule ambaye yuko Dubai, asilimia 30% wanachukua serikali Zanzibar. Sasa katika fedha ambazo zipo nafikiria ni dola 125 nafikiria kwa USD, sasa mimi nataka waziri atakapokuja atuweke sawa atufahamishe ni kwa nini tunalipa kule na kwa nini makubaliano hayo yapo asilimia 70% ili wananchi na wafanyabiashara wapate kufahamu kwa sababu wengi wananiuliza wanatuma salamu pengine wanahoji wanataka wajenge uelewa kwa nini pesa zile zinabakia Dubai na haziji Zanzibar.

Lakini halkadhalika ukiangalia sheria ya na.7 ya mwaka 2003 gari yoyote ambayo inatakiwa itembee barabarani inatakiwa iwe na *road l license* lakini pia iwe *insurance* sasa gari inafika bandarini inashushwa kwenye meli gari inatoka pale inatembea haina namba, haina *insurance*, haijapasishwa inakwenda zake inatembea barabarani pengine jioni gari imetoka, siku ya pili pia inachukuliwa tena inapelekwa kwenye *ZBS* wakapasishe. Gari hilo baadae ipelekwe sijui karakana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nataka nifahamu nani yuko *responsible*, kwa sababu gari lile ikitokezea ajali barabarani nani atachukua dhamana ya kwenda kulipa. Kwa sababu ile gari haina *road license* lakini serikali imeruhusu ile gari itembee barabarani. Sasa mimi ningeomba serikali watengeneze utaratibu, kwa sababu tayari wanazo *bill of lading* wanajua gari ngapi zinakuja, kama namba zipewe *temporary* kama namba moja, mbili, tano lakini pia wakatie *temporary insurance*, wakati anapotembea barabarani japokuwa sio *comprehensive*, juu ya *third part* angalau inapotokezea ajali mwananchi awe *covered*, kwa sababu yeye kukata *insurance* ya wiki au siku tano, kwa ule muda ile gari itakapotoka bandarini mpaka inakwenda kufuata sheria, basi waangalie utaratibu angalau mwananchi wa kawaida awe *covered*. Hilo la kwanza.

La pili, nataka nichukuwe nafasi hii kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri. Mhe. Mwenyekiti ni ukweli kabisa jana nilikuwa naisoma hii hotuba ya Mhe. Waziri, nimeipita usiku kwa muda wa saa moja. Kwanza nimegundua imefanyiwa kazi ipasavyo, katika hotuba ambazo tangu Baraza la Wawakilishi nimeingia basi hii ni *impressive* , anapokuwekea neno la Kizungu anakuwekea na la Kiswahili, halafu anateremka kwa mteremko kama vile unasoma kitabu cha Charles Linkens, anakuletea *story* anakuvuta kidogo kidogo anakupeleka mpaka anakufikisha katika hoja yake.

Kwa hivyo, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Tunguu nasema kwamba sitozuwia hata fungu lolote, kwanza nampongeza sana na iwe ni mfano kwa mawaziri wengine juu ya hotuba kama hizi zinazoletwa hapa. Natambua kuna changamoto nyingi za wafanyabiashara wetu, naelewa mapungufu yaliyokuwepo, lakini ukiisoma hii hotuba inaanza tayari kutoa mwanga. Naomba katika *strategy* ambazo waziri amejipangia akamate hapa hapa kwenda alipo, maana yake wafanyabiashara wakubwa mpaka wadogo wameguswa.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ipo na ni lazima nikubaliane na wenzangu waliotangulia, walivyozungumza kwamba katika masuala ya masoko. Nilimsikia Mhe. Rashid Makame jana alipochangia Mwakilishi wa Magomeni, nilimsikia Mhe. Jaku Hashim Ayoub walichangia kwamba bila ya kuwa na soko la kutegemea kwa upande wa wanzetu wa Tanzania Bara na maeneo mengine, ni vigumu kuendeleza viwanda. Hilo ni kweli kwa sababu sisi sote tunalotegemea kubwa ni kule.

Mhe. Mwenyekiti, sasa katika mfano huu nataka nitowe mawazo yangu, ikiwa sisi soko la Tanzania Bara tunapata changamoto hasa katika masuala ya *VAT* na mengine, kwa nini tusiangalie soko la Kenya. Sisi kama tunataka tununuwe bidhaa, tunataka tuuze pia, lakini pia kuna bidhaa nyengine tunaweza kununua kutoka Mombasa na Wakenya sasa

hivi wana-*produce* bidhaa nyingi, kwa sababu kwa hali tunavyokwenda tunawatia umaskini wananchi wetu hasa wafanyabiashara.

Mhe. Mwenyekiti, leo unaposafiri kutoka Bara kuleta mzigo huku, kutoa kule kuleta usumbufu wanaoupata ni mkubwa. Mhe. Mwenyekiti, najua unalo lile *briefcase* lako kubwa unalotembea nalo, hebu jaribu kushuka kwenye boti Dar es Salaam utamuona mtu anakuangalia utafikiri anataka kukumeza, kumbe begi lako lile lina makaratasi yako ya Baraza, inauma wakati mwengine.

Kwa hivyo, mimi niombe kwamba suala hili katika hizi changamoto au kero mapungufu ambayo tunakuwa tunakutana nayo hasa kwa wafanyabiashara na mwananchi wa kawaida, tujitahidini sana kuyaondoa. Lakini ukiangalia kwenye hotuba ambayo waziri amesoma nambari 26 na 27, mimi nampongeza kwa sababu kasema ukweli. Naomba nimnukuu.

"Mhe. Spika, katika kipindi hiki biashara kutoka Zanzibar kwenda Bara zimeendelea kupungua na hivyo kusababisha urari mkubwa wa biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara, ikilinganishwa na mwaka 2016. Haya ni maneno ya serikali. Hali hii ilitokana na vikwazo vya biashara visivyokuwa vya kiushuru hasa vibali vya ruhusa za kuingiza bidhaa na kulazimisha wafanyabiashara wajisajili tena Tanzania Bara. Hali iliyoleta usumbufu kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Mwenendo wa biashara baina ya pande mbili hizi ni kama inavyoonekana katika mchoro alioutoa. Ina maana amelikubali".

Namba 27 nanukuu tena, amesema:

"Mhe. Spika, hali hii sio nzuri kibiashara na wizara yangu inafanya jitihada kwa kushirikiana na taasisi nyengine za serikali kurejesha hali ya kibiashara iliyokuwepo baina ya Zanzibar na Tanzania Bara, hasa kuongeza bidhaa zinazosafirishwa kutoka Zanzibar kwenda katika soko la Tanzania Bara".

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo mimi namuomba mama yetu Mhe. Waziri usichoke kwa kweli umeshalijua tatizo, basi endelea kupambana, endelea kuwaelimisha na endelea kuudumisha Muungano wetu ambao tumetoka nao huko zaidi ya miaka 50.

Jengine ninalotaka kuzungumza ni suala la *Zanzibar Brand*. Mhe. Mwenyekiti, mimi inaniuma sana wakati mwengine ninaposoma katika mitandao ya kimataifa. Najua Mhe. Waziri alikuwa balozi kule Washington kuna mkahawa maarufu unaitwa The Zanzibar, utasikia kila pahala watu wanatumia neno la Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nataka nifahamu katika sheria za kimataifa yaani mmiliki na mwenye uwezo wa kutumia neno la Zanzibar ni nani. Leo kila mmoja anatumia *brand* ya Zanzibar. Utakuta viwanda pengine viko India vinatengeneza bidhaa. Pengine inawezekana karafuu inasafirishwa kutoka Indonesia inaambiwa made in Zanzibar. Haya yote inawezekana kwa sababu unachotaka ni kuweka kitambara ukaweka ile made in

Zanzibar kupeleka, kwa sababu hata inawezekana wale wenyewe wenye hilo neno la Zanzibar wametulia.

Sasa mimi nataka nimuulize pengine Mhe. Mwanasheria Mkuu atusaidie, atakapokuja Mhe. Waziri atuambie hili *made in Zanzibar*. Nimeona kwenye kifungu namba 98 ametumia juhudi na amefanya kazi nzuri katika kuanzisha hizi *product* za *made in Zanzibar*. Lakini katika *product* utakapokwenda kwenye anga za kimataifa, hawa wanaotumia kwenye mitandao ambayo hasa kwenye *website made in Zanzibar* mwenyewe hasa ni nani. Zanzibar ina umaarufu kuliko hata neno la Tanzania kibiashara, kwa sababu bado watu wengi wanaijua Zanzibar kihistoria huko tulikotoka. Kwa hivyo, mimi nataka kufahamu sana leo atakapokuja Mhe. Waziri atueleze neno la Zanzibar, *who is the owner of this name 'Zanzibar'*.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nataka niongelee kwenye kifungu namba 40. Nimeona Mhe. Waziri amefanya kazi kubwa sana na kuwaunganisha wafanyabiashara na Kampuni ya *Shanghai Min Hang Group* kutoka China. Kwanza nampongeza sana Mhe. Waziri kwa juhudi hizi. Mimi nilikuwa namuomba kitu kimoja tu basi Mhe. Waziri, ikiwezekana nguvu yake aliyoitumia katika kuileta kampuni hii, basi aunganishe mawazo yake na wizara ya Mhe. Haji Omar Kheir ya tawala za mkoa, ili kuangalia vikosi vyetu kama JKU. Kwa sababu kitu ambacho Zanzibar tukonavyo na vikosi vyetu tuna *labour* ambayo ni *main power*, tuna eneo zuri la kuweza kuwekeza kwa upande wa Zanzibar. Kwa nini tusichukuwe juhudi tukaunganisha nguvu na watu ambao wana uzoefu wa kutumia wajasiriamali katika nchi kama China, India na Malaysia tukaja kuongeza nguvu zetu hapa tuaanza ku-*produce goods* ambazo ni made in Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza mwaka jana kwa mfano *furnitures* ambazo kila mtu anahitaji kiti. Mhe. Mwenyekiti, kiti unachokalia wewe naamini sisi kama tunaweza kutengeneza kiti. Hicho kiti ukikiangalia pengine kimetengenezwa China au India, lakini kiti kama hicho tunaweza kufanya *assembling plan* hapa hapa za *TV* na za *Nokia* kwa sababu watu wapo, muhimu kuziweka hizi *incentives* na kuwavutia. Sasa kama *labour* ipo, tunao kwa upande wa Zanzibar na tunawapa na Micheweni pia, basi haya maeneo yaliyotengwa tuunganishe nguvu zetu, japo tuanze katika maeneo aliyoyataja madogo madogo kwenye sijui vidagaa, chumvi ambayo tayari ametaja sana kwenye hotuba yake. Basi kidogo kidogo hayo maeneo tukiyafungua kwa kutumia maeneo kama *SMIDA* wakala wetu pamoja na wengine wote pamoja na taasisi yetu ya *ZIPA*, basi tunaweza tukaleta miradi mikubwa mikubwa na midogo ya kati ili kwenda mbele.

Mhe. Mwenyekiti, pia nataka nimpongeze Mhe. Waziri nimeona kwenye suala la karafuu. Mwaka huu msimu huu ukiangalia kwenye kifungu namba 127 tume-*produce* karibu tani 6,770, *this is the record break after* miaka 21 haijawahi kutokezea Zanzibar. Kwa hivyo, nawapongeza sana wakulima na nawapongeza pia *ZSTC* waendelee na juhudi hizi ni nzuri sana kwa wananchi wetu. Lakini shukrani za pekee ziende kwa Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti, wa Baraza la Mapinduzi, kwa kujitahidi sana na suala hili, kwa sababu alilivalia koti yeye mwenyewe pamoja kuingia vitani kuhakikisha kwamba hili jambo anaweza kulikamilisha.

Mhe. Mwenyekiti, pia nimeangalia kwenye *issue* ya mwani kwenye namba 45. Mhe. Mwenyekiti, nataka nitowe tahadhari kwamba japokuwa wizara imejipanga katika kuhakikisha kwamba changamoto za mwani, lakini pia wataingia katika suala la usarifu, ambapo amesema katika *carrageen* nimeangalia neno kidogo gumu kuli-*pronouns*.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka niseme vitu viwili. Wenzetu *Philippines* na maeneo mengine huko ya South Asia wanaanza kujipanga sana katika suala la bei na hasa katika kuongeza ile *value change*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika mbili.

Mhe. Simai Mohamed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti. Kwa hivyo, mimi niombe sana kwamba Mhe. Waziri atakapojipanga ahakikishe kwamba, kwa sababu hili suala la mwani hasa katika Jimbo letu pia la Tunguu, maeneo ya Uzi, Unguja Ukuu wanalima sana mwani hata na Pemba pia. *Production* ambayo Zanzibar tuna-*produce* zaidi ya tani 3,000 najua na Pemba wana tani 12. Tukazane sana kuonesha kwamba bei na soko hasa kwa wananchi wetu, tunapokuja ku-*add value* tunakwenda sambamba na kuweza kuleta ushindani na ikiwezekana tuwatafute wataalamu ambao wana uzoefu waweze kutusaidia.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie tu, nimesoma katika kifungu namba 38 juu ya suala la ku-*link Africa markets* na *partnership* pamoja na *SMIDA*. Hili ni jambo zuri Mhe. Waziri kwa kweli unakwenda na wakati. Pia nimeona katika makusanyo yako ya mapato, mara hii umevunja rikodi umeweza kukusanya asilimia 190. Kwa kweli umefanya kazi kubwa sana, japokuwa sababu zilizokufanya ni kwamba umetaja kwenye kifungu namba 53. Moja iliyokusaidia ni suala la *ZRB* kukusanya mapato kwa wamiliki hasa katika kubadilisha majina kwenye umiliki wa vyombo vya moto, lakini pia unakuweko utaratibu mzuri katika *complains*. Sisi tunawapongeza wananchi. Hata hivyo, hivyo, juhudi hizi umezichukua wewe kama wizara umeweza kupata fedha nyingi, kwa hivyo mimi nikupongeze kwa hilo.

Mhe. Mwenyekiti, pia katika kitabu chake *record* ambazo uloziweka hasa ukiangalia katika mauzo ya bidhaa za usafirishaji katika Bara la Afrika, kwamba Afrika tunasafirisha asilimia *only 2.4*, na sisi Zanzibar na Tanzania tumo humo humo. Kwa hivyo, hili kwa kweli ni jambo ambalo limenishtua sana. Kwa hivyo, mimi niseme tu kwamba endeleeni kutupatia hizi *record* pamoja na hizi takwimu zitatusaidia sana sisi katika kujua. Naomba hiki kitabu pia kiunganishwe na wizara nyengine kama Wizara ya Fedha na Mipango wakipitie wataalamu, pamoja na Wizara ya Habari, Utalii na Mambo ya Kale kwa ndugu yangu Mhe. Mahmoud Thabit, pamoja na Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, ili waende sambamba kwa pamoja wote.

Baada ya hapo Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi, na kwa kunikumbushia wakati wangu na mimi nijipongeze pia kwa kutumia muda wangu vizuri sana. Nawashukuru wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa kunisikiliza.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Simai Mohamed, anayefuata ni Mhe. Nassor Salim Ali na Mhe. Panya Ali Abdalla ajitayarishe.

Mhe. Nassor Salim Ali: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia kidogo hotuba hii ya dada yangu Waziri wa Biashara na Viwanda Mhe. Amina Salum Ali.

Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze sana Mhe. Waziri kwa kazi nzuri ambayo anaifanya katika wizara hii, lakini vile vile nimpongeze sana Naibu Waziri Mhe. Hassan Khamis Diaspora, mtoto wa mkulima na mkwezi. Kwa kweli Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, nimpongeze kwa kumteua Mhe. Hassan Khamis Diaspora kuwa Naibu Waziri katika wizara hii, kwa sababu ni kiongozi ambaye anawajali wananchi hususan wale watoto wa wakulima na wakwezi.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika mwenendo wa biashara na viwanda. Mhe. Mwenyekiti, ni kweli mwenendo wa biashara na viwanda duniani umekuwa ukikua siku hadi siku, na hii inatokana na mahitaji makubwa ambayo yanatumika kwa wananchi duniani na hapa kwetu Zanzibar, na hasa ukiangalia kwamba Zanzibar ni watumiaji wakubwa sana wa mahitaji haya ya mchele, sukari, unga pamoja na mafuta ya kupikia.

Mhe. Mwenyekiti, Wazanzibari tunapenda vyakula hivi mchele, sukari, unga na ni utamaduni wetu. Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, kipenzi chetu cha Wazanzibari wote, ni kiongozi ambaye kwa kweli anawajali sana wananchi wake. Sasa kuendeleza sekta hii ya viwanda na kuimarisha masuala mazima ya biashara, kwa kweli ni wajibu wetu kumpongeza sana Mhe. Rais wetu. Kazi kubwa ambayo anaifanya Mhe. Waziri ni kazi kubwa ambayo inatokana na miongozo ya Mhe. Rais wetu.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar na Tanzania kwa jumla tunakwenda na ule msemo unaosema kwamba viwanda na biashara ndio tegemeo la mahitaji ya wananchi wetu. Nimpongeze sana Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuunga mkono na juhudi hizi kubwa ambazo anazifanya katika kuwekeza katika sekta hii ya viwanda.

Lakini mbali na hayo Mhe. Mwenyekiti, kutokana na uwekezaji huu wa viwanda na mimi nichukuwe fursa hii pia na serikali yetu kuhakikisha kwamba inatia juhudi kwa kuona kwamba Kiwanda chetu cha Sukari kinazalisha sukari, ili kuweza kuwasaidia wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa jumla na kuweza kuongeza pato kwa serikali yetu.

Vile vile kumlinda mtumiaji. Mhe. Mwenyekiti, serikali yetu katika kuwajali wananchi wake. Nichukuwe fursa hii kuiomba sana serikali yangu na nina imani kwamba serikali yetu hii tukufu na ni sikivu chini ya Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa kuwajali wananchi wake kutoendelea au kutokuongeza kodi kwa bidhaa hizi ambazo ni muhimu na ambazo tunatumia sisi wananchi, zikiwemo mchele, sukari na unga.

Mhe. Mwenyekiti, ili kukiendeleza Kiwanda chetu hiki cha Sukari cha Mahonda, serikali yetu iweze kuyapunguzia majukumu makubwa ambayo yapo katika kiwanda hiki, ili kile ambacho wanazalisha basi kiwe faida kwa mtumiaji yule wa chini, yaani mtoto wa mkulima na mkwezi.

Mhe. Mwenyekiti, jana wakati tulikuwa tunazungumza tunanong'ona na Mhe. Naibu Waziri, nilimwambia kwamba serikali yetu ina nia njema katika kukiendeleza Kiwanda hiki cha Sukari. Vile vile tufikirie pia wafanyabiashara ambao wanaingiza sukari hapa Zanzibar. Kwa kweli tukikipa au tukikiongezea majukumu makubwa kiwanda hiki, lakini vile vile tukiwaongezea majukumu wafanyabiashara kwa kuwaongezea ushuru wafanyabiashara katika bidhaa hizo wanazozileta zikiwemo sukari, unga na mchele tutawapa tabu wananchi wetu masikini ambao kwa kweli ni wajibu wetu sisi kuwatetea.

Mhe. Mwenyekiti, niiombe serikali yangu kwa unyenyekevu mkubwa kuwaangalia kwa jicho la huruma wananchi wetu, kutoongeza kodi ya aina yoyote kwa bidhaa hizi za mchele, sukari na unga. Kwa sababu utakapoongeza kodi kwa wafanyabiashara wanaoleta bidhaa hizi za sukari, unga na mchele tutawapa shida na tutawapa mzigo wananchi wetu masikini ambao kwa kweli ni wajibu wetu sisi sote kama viongozi kuhakikisha wananchi wetu wanaishi katika maisha ambayo ni mazuri na wanaendeleza maisha yao katika kiwango ambacho wanaweza kujiendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, wafanyabiashara wa Zanzibar ni wafanyabiashara ambao wanafanyabiashara kizalendo, lakini wako wengine wakorofi. Kuna wafanyabiashara kama vile Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil mfanyabiashara mzalendo mwenye kuwapenda wananchi wake na nchi yake, wanafanyabiashara kiuzalendo kwa kuwasaidia wananchi wao na wako ambao wanafanyabiashara kwa kuwasaidia wananchi wao kwa kupata faida ndogo. Sasa sio vyema tukaanza kuwapandishia makodi, kuwapa vikwazo ambavyo wananchi wetu watakuja kupata tabu na serikali hii naiamini ambayo imepewa jukumu na Chama cha Mapinduzi, kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi ni kuwasaidia wanyonge.

Kwa hivyo, nina imani kwamba serikali yetu haitaongeza kodi ya aina yoyote, hususan katika suala la sukari, unga pamoja na mchele pamoja na mafuta ya kupikia. Mheshimiwa niipongeze serikali yangu kwa kuondoa kodi hasa katika kipindi hichi cha mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Mimi niiombe serikali yangu iendelee kuondoa kodi katika bidhaa hizi muhimu kwa wananchi wetu katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani, kwa kweli bidhaa hizi ambazo zimendolewa kodi ni muhimu sana kwa wananchi wetu.

Lakini vile vile kuna bidhaa hii ya mafuta Mhe. Wazanzibari tunapenda sana kukaranga karanga, sasa bidhaa ya mafuta pia ni muhimu, mimi niiombe serikali yangu. Mhe. Waziri naomba ulichukue hili na serikali yetu nina imani kwamba watalichukua kuhakikisha kwamba hata bidhaa hizi za mafuta basi inaondolewa kodi katika kipindi hichi cha Ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika suala zima la maendeleo ya Wajasiri Amali, niipongeze serikali yangu kwa kuwasaidia sana hawa wajasiri amali. Kwa kweli Mhe. Waziri

amekuwa akifanya kazi kubwa sana katika kuwasaidia hawa wajasiriamali. Hata katika kitabu hiki ukiangalia nyuma hapa utaona picha za wake wa viongozi wetu kuna picha ya Mhe. Mama Mwema Shein na kuna picha ya Mhe. Mama Asha Balozi, wakiwashajihisha na kuwaongezea bidii kwa wajasiri amali na kuweza kusaidia kuendeleza wajasiri amali wao.

Mhe. Mwenyekiti, haya yote yanatokana na viongozi ambao kwa kweli wanawajali wananchi wetu. Wajasiriamali ambao wamekua hususan kinamama, Mhe. Mwenyekiti, biashara ya dagaa sasa hivi imekuwa ikipanda kasi siku hadi siku. Dagaa limekuwa ni bidhaa kubwa sana na lina faida kubwa sana. Dagaa leo linauzwa hata nje ya nchi, wafanyabiashara wa dagaa wanapeleka dagaa katika nchi za jirani, lakini wamekuwa wakipata changamoto kutokana biashara hii ya dagaa hasa katika nchi za wenzetu katika Jamhuri ya Muungano wetu wa Tanzania, sasa nimuombe Mhe. Waziri ili aweze kufatilia ili wananchi wetu hawa wanaofanya biashara hizi za dagaa waondokane na matatizo wanayoyapata katika kusafirisha biashara hii ya dagaa.

Mhe. Mwenyekiti, dagaa sasa hivi linatumika hata katika kuwalisha viumbe vyengine wale wanaofuga kuku linatumika hata kuwalisha kuku. Nimuombe Mhe. Waziri ili kuwasaidia wajasiriamali hawa ambao wanazalisha hili dagaa kwa biashara na kuweza kukimu katika maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, lakini vile vile wafanyabiashara wa mwani, nimshukuru sana Mhe. Waziri nimekuwa nikifuatilia sana mwenendo wao katika kuwasaidia wafanyabiashara hawa wa dagaa pamoja na mwani pamoja na wale wanaozalisha chumvi. Kwa kweli kazi ambayo anaifanya Mhe. Waziri ni kubwa ni wajibu wetu kumuunga mkono na nina imani Wawakilishi wenzangu na Viongozi wote tutaweza kuiunga mkono serikali yetu katika kuwasaidia wananchi wetu katika kujikwamua na maisha, katika kuendeleza biashara hizi ndogo ndogo ambazo kwa kweli wajasiri amali hususan akina mama wamekuwa wakifanya kazi kubwa sana ili kutusaidia akina baba sisi katika kujikwamua na maisha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilisema nichangie kidogo, lakini nirudie kuiomba serikali yangu kuangalia zaidi wananchi wetu ambao ni wanyonge ili kuhakikisha wananchi wetu wanapata bidhaa kwa urahisi na kuweza kuendeleza maisha yao.

Mhe. Mwenyekiti, nimuunge mkono sana na naiunga mkono hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda, dada yangu Mhe. Amina Salum Ali na huyu ni dada kweli kweli sio mas-hara, kwa sababu mimi naitwa Nassor Salim Ali na yeye anaitwa Amina Salum Ali ni dada yangu wa damu. Kwa hiyo Mheshimiwa nakuunga mkono kwa asilimia mia moja (100%) na nawaomba Wawakilishi wenzangu leo Bajeti hii tusipige buti hata moja tuipitishe kwa sababu ni kitabu ambacho ni kizuri, kinamaelekezo mazuri, kina mambo mazuri na nina imani haya yote katika kutekeleza vyema Ilani ya chama cha Mapinduzi.

Mhe. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Mwenyekiti: Anayefuata ni Mhe. Panya Ali Abdalla na Mhe. Suleiman Sarahan ajitayarishe.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahasante sana Mhe. Mwenyekiti, nichukue fursa hii na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia uhai tukaweza kukutana mahala hapa tukijadili amasuala ya Bajeti zetu.

Pia nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda, Naibu Waziri na watendaji wake wote. Nampongeza sana Mhe. Waziri kwa utendaji wake makini, mwanamke anayejiamini, mwanamke mchapa kazi, uwepo wetu sisi hapa basi niseme amechukua hamasa kubwa sana kupitia *UWT* kutuhamasisha tukaweza kupita hapa. Ni kiongozi shupavu na ameweza kupata uwongozi wake kuanzia ujanani kwa hivyo ana kila aina na sifa katika uongozi. Namuombea kwa Mwenyezi Mungu azidi kumzidishia hekma na busara na aweze kumuwezesha katika majukumu yake. Mhe. Naibu Waziri una waziri mzuri naomba utulie uwe msikivu, uwe mtaratibu utagema hekma nyingi kupitia Waziri wako na unaweza kufika mbali katika mafaniko yako. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naishukuru na kuipongeza Kamati na hasa muwasilishaji aliyewasilisha jana ni muwasilishaji mzuri kabisa nampongeza na nawapongeza wana kamati wote.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika *Programu* ndogo ya Viwango na Udhibiti wa Ubora. Kwanza niishukuru na kuipongeza serikali yangu ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuona umuhimu mkubwa wa kuweka kitengo hiki. Naipongeza sana kwa sababu bila ya kuwepo kitengo hiki tungeendelea kupata dhiki. Napongeza kitengo hiki lakini ni kitengo hiki ni kitengo muhimu sana ambacho ndicho kinachotulinda afya zetu lakini ndicho pia kinachotuweka na kinachofanya kuangalia, kumlinda mlaji. Kitengo kina umuhimu mkubwa sana na naomba sana serikali iangalie katika utendaji inapopanga fedha katika kitengo hichi ili kiweze kufikia malengo yake basi kitengo hiki kiwe asilimia kubwa sana ya fedha ili kiweze kuendelezwa.

Mhe. Mwenyekiti, tuangalie kiwango hiki kimepangiwa milioni mia mbili lakini nne na thamanini mwaka wa jana lakini fedha zilizoweza kupatikana ni 866. Sasa tujue mambo muhimu ya kumlinda na kumnusuru mlaji yanaweza yakakosekana. Kuna mavyakula yanayoletwa bila ya kitengo hiki kuwezeshwa kikaweza kikafanya kazi yake vizuri tutazidi kuangamia. Naishauri sana serikali iwe makini sana katika chombo hiki, hiki ni chombo ambacho mmekiweka kitatusaidia sana katika kujenga afya zetu na kutulinda.

Mhe. Mwenyekiti, pia niendelee na mchango wangu katika ukurasa wa 69 ambapo mmeonyesha kuna maeneo tengefu ya viwanja. Mheshimiwa nashukuru kwa jambo hili na naomba maeneo hayo kama dhamira yetu mlivyoyaweka ya kuweza kuyapima maeneo hayo, maeneo yapimwe msisitizo wangu ni hati miliki kupatikana kwa haraka wakati yatakapopimwa maeneo haya, lakini pia maeneo haya kuweza kudhibitiwa ili yasiweze kupata uvamizi hizo siku za usoni.

Mhe. Mwenyekiti, naliomba sana kwasababu mara nyingi maeneo anayotengwa na serikali halafu baadae yanaachwa huria na yanakuja kuvamiwa, kwa hivyo maeneo ambayo yatatengwa kwa viwanda yawekwe na yaweze kudhibitiwa.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika sekta ya viwanda ambapo kuna program ndogo ambayo hii imepangwa kuwasaidia wajasiri amali.

Mhe. Mwenykiti, hapa zimepangwa shs. 644,000,000 kwa mwaka 2017/2018 lakini fedha iliyoweza kupatikana ilikuwa ni shs. 271,000,000 ikiwemo mishahara kazi za kawaida. Mhe. Fedha hizi hapa ni kiasi gani ambacho kimepangwa kwa hawa wajasiri amali ambao tunataka kuwasaidia, kwa sababu wajasiri amali ambao tunawategemea hivi sasa bado hawajaweza kusimama kwa miguu yao miwili. Ni lazima tuweze kutenga fedha, tuwasaidie wajasiriamali ili sasa tuweze kupata hivyo viwanda ambavyo serikali inategemea kuja kuwa na viwanda na lazima tuanze na wajasiriamali wadogo wadogo, ambao ndio baadae wataweza kuzalisha viwanda vikubwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ni lazima, wajasiriamali tuwaangalie kwa jicho la huruma na hasa pale nilipozungumza katika kitengo cha *ZBS,* Mhe. pale nilikuwa naombi nilikuwa niparuka nimesahau, wajasiriamali bado fedha tunazowatoza ni nyingi kwa wao ambao fedha yenyewe hawana mpaka wasaidiwe huku na huku. Kwa hivyo lazima tuwangalie wajasiriamali katika kuwasaidia hili, ili waweze sasa nawao katika kiwango waende wapimiwe bidhaa zao na bidhaa zao niseme zina ubora, kwa sababu kuna vitu ambavyo mimi nishavifanyia utafiti nilinunua jam, nikanunua jam katika wajasiriamali wetu hawa, nikanunua na jam ile ambazo tumezinunua katika maduka ya wenzetu, ambazo bidhaa hizo huwa huwa zinatoka nje ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, yetu ina ubora, tena tujiamini na niishukuru Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuwasomesha vijana wetu hawa katika kuwekeza katika ujasiriamali wao kwenda kwenye kutengeneza vitu ambavyo tulikuwa tunategemea kuzalishwa huko nje ya nchi yetu. Kwa hivyo, sasa tukiwawezesha wajasiriamali hawa lengo litafikia lile la serikali kuwa na viwanda. Mimi naomba sana wapunguziwe kwa sababu wao bado ni watu tegemezi.

Nikiendelea na mchango wangu niende katika suala zima la takwimu ambapo Mhe. Waziri wakati wa kuwasilisha hotuba yake alisema kuna udhaifu wa takwimu. Mheshimiwa mimi naiomba sana serikali, kwanza jambo la takwimu ni jambo muhimu mahala popote, ili mambo yako yaende vizuri basi lazima takwimu zikuongoze katika usahihi, kama takwimu zimepinda pinda hizo ujue na mipango yako itapinda vile vile. Kwa hivyo, Mheshimiwa mimi naomba sana suala la takwimu hasa kwa wale watendaji wetu ambao wanahusika sana na suala hili wajikite sana katika kuzipata takwimu zetu ili mambo yetu yaweze kwenda kama tulivyoyapanga.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu huu kuna viwanda hivi ambavyo mwaka jana walitueleza Kiwanda cha Soda wanategemea kiweze kutusaidia kuzalisha na Kiwanda cha Nguo cha *COTEX*. Mheshimiwa mimi nawaomba mufanye juhudi zanu zote, utegemezi huu wa kuwa kila wakati tuagize vitu sasa hivi tujikite katika kupunguza

mahitaji yale ambayo tayari sisi uwezo tunao wa kuzalisha katika nchi yetu, basi lazima rasilimali tulizonazo tujitume tuweze kuzitumia ili ziwe manufaa. Hiyo azma ya kufikia katika viwanda *Wallahi* ndipo itakapofika. Lakini bila ya kujaribu vile ambavyo tayari sisi tushakuwanavyo na serikali imeshatupa fedha nyingi kwa kusomesha watu, mimi naomba na nategemea sana kwa umakini wa waziri wetu huyu Bi. Amina Salum na Bi Amina ni mtu makini sana, nategemea tutaweza kujikita mimi nashawishika sana kuanza kutumia vitu vyetu ambavyo tunavizalisha. Kwa nini siku zote sisi fedha yetu tuipeleke kwa wenzetu tu, baada ya kuiacha hapa wakanufaika wajasiriamali wetu tukaondosha ile dhana ya *vision 2020*. Wajasiriamali wetu wakakua na fedha zetu zikawepo na tukaweza kukua na sisi kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, nilitaka kusisitiza hiki Kiwanda cha Soda na cha *COTEX* tuanze ili tuone tunafikia wapi.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba sana serikali ilisema habari ya sera hii haijakamilika, naomba sana juhudi za sera hizi ziweze kukamilika ili sasa azma hiyo ya kuwa na viwanda kwa sababu huu ndio utakuwa muongozo wetu na utaweza kurekebisha sheria zetu pale zilipokuwa hazijakaa vizuri ili tuweze na sisi kufikia katika hatua hiyo. Tunaweza, tunaweza nasema tena tunaweza.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika masoko. Masoko bidhaa bila ya soko utazalisha utashindwa vya kuiuza na utashindwa kuweza kuwa na hiyo mitaji mikubwa mikubwa. Mheshimiwa mimi nimuombe sana Mhe. Waziri aanze kudhibiti haya masoko yetu ya ndani ili sisi tukitaka wajasiriamali wetu wakue kwa bidhaa ambazo wanaweza kuzizalisha lazima ufanyike utafiti wa kuona bidhaa gani sasa wajasiriamali wetu wanaweza kuizalisha na tukaweza kuitumia sisi hapa. Tafadhalini tuwaweke katika maeneo ambayo wataweza kuuza bidhaa zao hizo na sisi tuanze kupunguza mahitaji yale ya kuchukua bidhaa kule ambazo tayari wajasiriamali wetu sisi wanaweza kuzizalisha. Kwa sababu wajasiriamali serikali mmeshafanya na mmeshapoteza fedha nyingi kwa kuwasomesha, ili zirudi fedha zetu hizo lazima tuwainue wajasiriamali hawa ndipo tutaweza kufikia huko ambako tunataka kufika.

Kwa hivyo, mimi naiomba sana serikali kuweza kudhibiti soko hili kwa zile bidhaa ambazo tayari tunazizalisha ili tuweze kupunguza huo umasikini lakini tuweze kufikia azma yetu ya kuwa na viwanda vikubwa na vidogo.

Mhe. Mwenyekiti, wajasiriamali ili tuwasaidie lazima fedha fedha itengwe kabisa, kwa sababu mwaka juzi 2016/2017 tulitenga shs. 56,000,000 na walipata shs. 8,000,000 bado hatujawa na dhamira hasa ya kuwasidia wajasiriamali, 2017/2018, tulitenga shs. 267,000,000 wameweza kupata 34,000,000 sawa na asilimia kumi na mbili 12%, bado hatujawasaidia wajasiriamali wakaweza kusimama kwa miguu yao. Mimi sasa hivi nashawishika katika nchi yangu na najua uwezo upo, lazima tujifunge katika kuwasaidia wajasiriamali hawa ili sasa azma iweze kupatikana.

Mhe. Mwenyekiti, nina lalamiko kidogo katika ukurasa wa 51, kuna neno linaitwa ukondoweshaji. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, lalamiko langu kidogo, mimi ni muhusika sana katika Kiswahili, na nasema kila siku tutumie Kiswahili chetu ambacho kimo katika makamusi yetu. Kuna neon linasema ukondoweshaji, neno hili linapatikana katika kamusi gani na maana yake nini, ili mimi niweze kuelewa na wazanzibari wanasikiliza bajeti hii waweze kuja neno hili lina maana gani, kwa sababu huko nje wanatusikiliza sana kutaka kujua bajeti yao, na wajasiriamali wetu wapo pia wnatusikiliza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Mimi sina tatizo na mama huyu na ni muelewa na msikivu na ni mchapa kazi, kwa hivyo, naiunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja na nawaomba wenzangu tumuunge mkono Bi. Amina kwa sababu ni mchapa kazi, ni hodari, ni msikivu, anakubali maelekezo, na naamini na naibu wake ataendelea kuwa hivyo na watendaji wake katika wizara yake wataendelea kuwa hivyo kwa sababu wana kiongozi makini ili tuweze kufikia dhamira kuu ile ya serikali kwa nchi yetu kufikia viwanda. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaaliwa kufika hapa salama na Mwenyezi Mungu aturudishe majumbani salama.

Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote na mimi nipende kmshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein, katika juhudi zake za kuwaletea maendeleo wananchi wake wazanzibar na Zanzibar yenyewe kwa ujumla.

Mhe. Mwenyekiti, pia na mimi niungane na wenzangu kumshukuru wazi katika kitabu chake ambacho kwa kweli kina ukweli mtupu katika mazingira ama kwa mantiki yoyote amezungumza neno ambalo lina uhakika wa kuweza kutoa ukweli na tathnia nzima ya biashara.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi nianzie na ukuaji wa uchumi. Mhe. Mwenyekiti, Katika nchi yoyote kuna ukuaji wa uchumi, wa nchi yenyewe na ukuaji wa uchumi wa wananchi wenyewe. Wananchi huwa hawaoni ukuaji wa nchi kama pesa mifukoni hawana au hawawezi kuona kwamba maisha yao yanakuwa upatikanaji wa chakula na mambo mengine ya madawa na elimu vikiwa ni vitu vigumu wanaona kwamba hata ukuaji wa nchi bado wanaona kwao ni ngumu kidogo. Lakini niishukuru serikali yetu kwa upande mmoja, upande wa elimu wamesaidia sana serikali katika kufanya kila jitihada za kuwaondolea wananchi majukumu ya kulipia wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini Mhe. Mwenyekiti, nchi yetu imepiga hatua katika kukua uchumi na imekuwa nchi huru sana katika kuleta bidhaa unapoona kwamba inafaa basi unaruhusiwa kuleta lakini Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar ni nchi ambayo ina tegemezi sana katika nchi za nje. Zanzibar ni ndogo biashara yake kufanya kwake ni taabu kwa sababu wananchi wake ni kidogo na maeneo yake ni kidogo lakini asili yake ni wafanyabiashara.

Mhe. Mwenyekiti, watu wengi wamekwishazungumza suala la kupeleka bidhaa kutoka Zanzibar kupeleka upande wa Dar es salaam kwamba kuna matatizo ambayo

yanajitokeza hasa Mhe. Waziri nilipomsikia hapa aliposema kwamba uchumi umeteremka katika masuala haya ya kodi na mambo mengine kutokana na kutokupelekwa kwa bidhaa ambazo nyingi zimeweza kuleta utata kule Dar es salaam. Sasa na wenzangu wamezungumza suala hili Mhe. Mwenyekiti na mimi nimuombe Waziri kama mwenyewe alivyosema asichoke tukalizungumzia tena suala hili kwamba sisi tufahamike kwamba ni tegemezi kubwa la ndugu zetu katika biashara zetu.

Inawezekana hizi zikawa ni sheria inawezekana haya ikawa ni jumla ya mtu mwenyewe kufanya utashi wake katika kutubana katika mambo haya ya kupeleka biashara Tanzania Bara kwa hivyo ningeomba Mhe. Waziri mwakani tukijaaliwa 2019 atakapo kuja hili suala awe keshalitafutia ufumbuzi na sisi tuendelee na biashara zetu.

Mhe. Mwenyekiti, naendelea na viwanda vikubwa, Waziri ni mtu mwenye *experience* kubwa sana mimi kwa sababu ni mdogo wa umri kidogo nataka akija hapa atufahamishe kidogo kwamba zanzibar ilipiga hatua gani katika miaka ya nyuma ikaweza kujenga viwanda vikubwa sana hapa, mpaka ikawa tunaweza kuwatafuta watu kutoka nje kuja kutusaidia wananchi hawapo au vijana hapana. Sasa hivi tumekwama wapi kuviendeleza viwanda vikubwa ambavyo mimi naamini Zanzibar kwa mkondo huu wa vijana ambao tunahitaji kuwapatia ajira tukipata viwanda viwili vikubwa lazima tukatafute watu kutoka nchi nyingine hatuna watu wa kutosha. Ningemuomba waziri katika hatua ambayo atatusaidia sana kuondokana na mkondo wa vijana ambao hawana ajira yeye ni mmoja wa kututafutia viwanda vikubwa ambavyo vitatusaidia kuzalisha kuongeza pato lakini pia kutoa ajira kwa wananchi. Ningeomba sana Mheshimiwa hilo nalo aliangalie kwa kina.

Mhe. Mwenyekiti, nije na viwanda vidogo vidogo waziri anajitahidi na namuona sana Pemba hatoki anakwenda sana katika sehemu za viwanda vidogo vidogo na vipo viwanda vidogo vidogo lakini kwa kweli bado vinahitajika viwanda vidogo vidogo, mimi namuomba Waziri kwa kumwambia bado vijana wanahitaji sana kazi lakini bado muelekeo wa wananchi au kwa upande mwingine. Mimi nizungumzie suala la viwanda vidogo vidogo, Waziri kwa hili ajitahidi kuzungumza na serikali kama bado wajasiriamali ambao wana uwezo wa kuweza kuja kuleta viwanda pale Pemba vya matunda na mambo mengine mengi, kama bado hawajajitokeza na serikali imeshatoa mwanya na kupiga kelele siku nyingi, serikali sasa iweke mkono wake wa kuweza kuleta viwanda ambavyo vitaweza kufanya kazi na kuweza kuyaokoa mazao ya wananchi yale ambayo mengine anazalisha Mwenyezi Mungu kutokana na maembe yanayokuja kila siku lakini mengine wananchi wanajitahidi kwa nguvu zao lakini kwa sababu matunda yenyewe yanakuwa hayawezi kustamili yanapotea bure.

Kwa hivyo ningeomba kuna uzalishaji ule wa muda mrefu ambao ni maembe yanayokuja kwa msimu na mambo mengine lakini kuna kazi ambazo za juhudi za mwenyewe mtu halafu anafia njiani kutokana na kukosa soko au kukosa kuweza kuwekwa katika sehemu ambayo au kupeleka kiwandani. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri suala hili kwa upande wa Pemba hasa mazao yanaharibika sana na sasa hivi imekuwa kama suala la maembe bora uyachume machanga uyapeleke yakafanyiwe *juice* kuliko kusubiri yakiiva yanakuwa hayana soko. Ningeomba sana Mheshimiwa akatizama katika suala zito, sasa hivi hakuna hata mtu mmoja atakaezungumzia katika nchi yoyote ukisema wewe ni

uchumi basi biashara ndiyo sababu yake, ukisema kodi biashara ndiyo sababu yake, ukisema afya biashara ndiyo sababu yake kila utakachokigusa biashara ndiyo inayoleta maendeleo. Kwa hivyo ningemuomba Waziri wa Biashara kwamba yeye juhudi zake zikiongezeka basi ndiyo ukuaji wa nchi utaongezeka kwa wananchi na pato la nchi litaongezeka.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nizungumzie kwamba kuna suala ambalo hili kidogo linakuwa na maelekezo mengi tulianzisha *Sunday Market*, hizi *Sunday Market* naona mpaka sasa hivi nimeiona kule Pemba hasa Chakechake ndiyo iliyodumu lakini haina makaazi mpaka leo inakaa barabarani, wala sioni kwamba imefanyiwa juhudi kubwa za kuweza kupata eneo ambalo litakuwa *permanent* na kuongezeka kwa wale *Sunday Market* hata watu wa maeneo ya Pemba nzima wakaweza kufika pale kuja kununua vitu. Kwa kipindi kilichoanza wananchi wengi walihamasika lakini sasa kadiri hali inavyokwenda ni kukosa kwa eneo maalum ambalo litakuwa karibu na mji. Mimi sasa hivi kuna maeneo ambayo imewekwa pale katika soko la Michakaini tumeomba tuwajengee maeneo lakini Mheshimiwa kama mfuko wangu wa jimbo sina uwezo wa kuliimarisha hasa soko la *Sunday Market.* Ningemuomba waziri atakapokuja akifika Chakechake tukutane nimpeleke kwenye soko la *Sunday Market* aongee nao na aweze kupata utaratibu kamili.

Ningemuomba Mheshimiwa atakapokuja katika jumla ya mazungumzo, sasa hivi mji wa Chakechake tunauteremshia Tibirinzi kidogo ukae pahala pazuri kuna ile sehemu iliyojengwa katika Wizara ya Fedha wamejenga jengo lile ambalo halikuleta manufaa lile eneo lipo, mimi ningeshauri waziri utakapokuja pale ukatuombea kwa kipindi kwanza *Sunday Market* ikaweza kukaa pale inaweza ikafanya vitu vingi sana na wananchi wakaongezeka kuwa wengi katika masuala hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nazungumzia tena suala la biashara, namshukuru tena Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Watu wengi sana hapa wamesifia kwamba ukuaji wa karafuu au zao la karafuu limeongezeka kwa asilimia kubwa sana. Mheshimwa zote hizi nasema bila kificho ni juhudi za Mhe. Rais katika hali ya kuirudisha mikarafuu katika hali yake amejitahidi sana katika kipindi hiki, lakini amefanya mambo makubwa ya kuweza kuzalisha miche lakini Mhe. Mwenyekiti namuomba Waziri miche imekuwa michache katika msimu huu na pamoja na kuwa wewe ni wizara yako na wizara ya kilimo ningeomba kwenda kuongeza nguvu kwa sababu mara hii miche ilikuwa ikitoka mwisho mtu anapata miche mitano mpaka kumi wakati miche ilikuwa ikitoka kuanzia elfu nne au elfu tano kwa shehia na mtu akiweza kuigawa. Kwa hivyo naomba sana Mheshimiwa miche ya mikarafuu ukashirikiana na wizara ya kilimo basi ikajitahidi sana katika msimu huu watu wamehamasika sana kutaka mikarafuu mpaka huwezi amini kama watu walianza kupigana kwa kuwania mikarafuu. Kwa hivyo Mheshimiwa hizi ni juhudi za Mhe. Rais na zimezaa matunda na vile vile zimeonesha mwelekeo na muitikio wa wananchi wa Pemba kuzalisha karafuu zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nizungumzie kwamba kuna mabwawa haya ya samaki ambayo yanaundwa, Mhe. Waziri wa Kilimo aliyepita hapa aliwahi kunijibu katika maeneo ya Tibirinzi Mheshimiwa pale pahala sasa hivi kwa suala la kilimo limeondoka halifanyiki tena kilimo pameingia chumvi na maji ya chumvi yamejaa muda wote lakini aliniambia hapa kuna uwezekano mkubwa wa kwamba tayari kuna ufugaji wa samaki. Mheshimiwa naomba pale uje upaangalie pahala pamekaa vizuri sana pamekaa kwa *style* yote kwa hivyo, ningeomba uje utusaidia maarifa ili tuweze kujua kwamba mabonde yale yanaweza kusharifika vipi ukiachia kwamba tutashirikiana na wizara ya kilimo ili kuweza kuongeza pato zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, nimefurahi sana umezungumzia habari ya wananchi wa kipato cha chini, ningeomba sana suala ulilolisemea ni suala kweli kweli. Katika ukurasa wa 38 umewazungumzia watu wengi sana hapa ambao kwa kweli nimefurahishwa na hicho sasa katika kifungu cha 72 umewataja watu wengi sana wakiwemo Madereva, Matarishi, Makarani, Walinzi na wengi tu ambao wana kipato cha chini, Mheshimiwa mimi nimekusifia sana hapa. Hawa watu nasema ni asilimia kubwa sana ambao wanafanya hizi kazi ukiachia madereva wa dala dala na wengine lakini hao tuliowataja kama tuseme walioko kwenye serikalini wanahitaji kukopeshwa, wanahitaji kuongezwa mishahara wanahitaji kulindwa katika sehemu tofauti.

Lakini Mheshimiwa watu hawa bado hawajapatiwa kipaumbele, ningeomba sana Mhe. Mwenyekiti. Kwanza suala la madereva wewe kama ni mfanyabiashara sijapata kuona madereva wa kike angalau sisi kama serikali madereva wa mawaziri nao tungewaona nao wanawake. Waziri mwanamme akaendeshwa na dereva mwanamke na waziri mwanamke akaendeshwa na dereva mwanamme tukaonesha kuchanganyika na kuweza kuwapa nguvu. Mheshimiwa wewe una upeo mkubwa wa kuliangalia hili lakini pia utakuja kuliona kama lina uzito wake, kwa hivyo ningeomba.

Mhe. Mwenyekiti, nimwambie tena Mhe. Waziri ukikosa kazi, kazi yoyote unaifanya kuna kazi nyingine za kike wanafanya wanaume na kazi za wanaume wanafanya wanawake. Mhe. Waziri ningeomba sana baadhi ya mambo mengine ukapiga marufuku. Kazi nyingine wanaume wasifanye wawaachie wanawake angalau na wao kwa sababu nguvu zao ndogo, wewe unaweza kumkuta mwanamme mkubwa dukani linamkamatia mwanamke *underwear* anamfundisha yule akafanye kazi asikae dukani, anakaa dukani awaachie wanawake wewe jibaba kubwa mali inawezekana ya mtu yoyote lakini wale wauzaji basi baba kubwa mpeleke akafanye kazi asikae ndani na wale wanawake waliokuwa afya zao ndogo, kuna kazi ya kuuza madafu sijawahi kumuona mwanamke akiuza madafu. Ni kweli hawaziwezi kupanda minazi na kuchonga madafu, lakini kazi za maduka unalikuta baba kubwa lina miraba ngapi anauza vitu. Mheshimiwa sehemu nyingine piga marufuku wakae wanawake angalau na wao wajisaidie lile baba lipeleke kazini likafanye kazi lisikae tu.

Mhe. Mwenyekiti, jengine nataka nimwambie pamoja na mambo yake ya biashara....

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika mbili Mheshimiwa.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti, kuna mambo mengi ambayo muda hautoshi lakini nikwambie kwamba uongee na Mhe. Waziri wa Fedha biashara za mabenki wanatoza *amount* kubwa sana, asilimia ya mfanyabiashara anachumia benki na matokeo yake mpaka anauziwa nyumba hapati asilimia hiyo. Hasa nikwambie kitu kimoja Mhe. Mwenyekiti, mfanyakazi wa Pemba akishakukopa kama anakwenda Dubai uangalie mzigo wake mpaka ufike Pemba akauuze lini. Wakati kila mwezi anakatwa *intrest* lakini chengine ni kwamba mfanyabiashara huyo huyo katika mazingira ambayo unayaona ni kwamba katika kile kipindi ambacho hajafanya biashara, kwanza hawana hata mwezi mmoja wa kumpa *offer* ya kuanza kwenda kufanya biashara ningeomba Mhe. Mwenyekiti kwa sababu siwezi kuelezea sana muda haupo ukaongea na Waziri akaongea na benki hasa *offer special* kwa upande wa Pemba na Zanzibar wakaweza kutugaia nafasi kidogo wakatupunguzia *intrest* na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, tuzungumzie suala la kwetu wewe angalia katika mji wetu wa Zanzibar mabango ya matangazo hamna, ukitia tangazo ZRB anakukamua maana watu wanaangalia pamoja na mabango ukiandika bango kubwa basi ujue utakoma. Sasa watu hawaandiki hata bango wanauzia mlangoni kwa sababu bango linampelekea akakamuliwe. Waangalie sana ZRB wasitizame mabango yale ni matangazo tu unaweza kumkuta na bango kubwa biashara yake ndani ndogo lakini bango lile anaambiwa unaliona lile bango sasa Mheshimiwa tusitizame bango tutizame biashara tumkamue mtu kutokana na *percentage* yake tusimkamue mtu kutokana na tunavyomuona.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo ningeliomba hili na wewe ukaweza kulizungumzia, lakini kule Pemba tulikuwa ni watu adhimu sana na tulikuwa tunapendwa na watu wengi sana. Mhe. Mwenyekiti Pemba kidogo tumekuwa na matatizo ya kuiga hatuna asali, asali zote za kutia sukari, mambo mengine yoyote karafuu tunaziharibu, Mhe. Mwenyekiti ungekaa na watu kule tukazungumzia yale mambo siku hizi mtu akitaka asali ile ya uhakika hata wale wagonjwa wa sukari bora ale sukari hii kuliko kula asali.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana naunga mkono hoja ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Suleiman, Waheshimiwa nilimtangaza Mhe. Abdalla Ali Kombo lakini kwa bahati kaondoka kwa hivyo atafuatia Mhe. Ahmada Yahya na Mhe. Miraji ajitayarishe.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuweza kuchangia wizara hii muhimu yenye ustawi wa nchi yetu na tegemeo kubwa sana katika uchumi wa nchi yetu. Awali ya yote kwa sakafu ya moyo wangu napenda kumpongeza sana Mhe. Waziri na timu yake kwa jumla jinsi ya maandalizi mazuri ya kitabu hiki chenye kuonesha takwimu, muendelezo, vyanzo vya habari na mengineyo. Katika maisha yangu ya Barazani tangu niingie basi sijapata kupata kitabu kizuri ambacho kipo *interested* nikenda nikakisoma nyumbani leo asubuhi ili kuja na *point* zifuatazo katika kukazia na kuhuisha uchumi wa nchi yetu. Mheshimiwa hongera sana.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nitaanza na ukurasa wa 13 ni kweli kwanza nakupongeza kwa uwazi wako kwamba biashara kati ya Zanzibar na Tanzania Bara imeshuka from 33.6 wakati tulikuwa tuko 84.7.9, hiyo inaonesha ni ubaya *balance of trade* wazungu wanaita *balance of trade, balance of trade* ni mbovu mno na haitupi moyo. Lakini Mheshimiwa nakuamini umefanya kazi katika mashirika makubwa na sina wasiwasi hii hali kwa diplomasia yako unaweza ukaichunga na ikaja katika hali ya kawaida na Zanzibar tukaanza kurejesha ustawi wa biashara, baina ya Tanzania Bara na Zanzibar. Hali ni mbaya na umekiri mwenyewe kwa hivyo mimi sina wasiwasi, hili suala kwa diplomasia yako bila kuathiri upande wowote nina hakika tutakuja katika hali ya usawa wa lete, chukua, rejesha, uza. Kwa hivyo hongera sana.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nakuja ukurasa namba 20 maeneo tengefu ya viwanda *Industry park* kwa kila wilaya kwa sasa tunatarajia kuanzia matatu naomba utakapo kuja uweze ku-*indentify* matatu haya Unguja mangapi na sehemu gani, ili kusudi *white* watujue kama maeneo haya ambayo pengine *pilot* umejielezea katika kitabu chako kiwilaya lakini haya maeneo matatu ambayo labda ni *pilot* tuweze kujua yapo katika maeneo gani katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba ili kusudi watu waelewe namna gani maeneo hayo na sehemu gani yatapokuwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo nakuja ukurasa wa 52 kwanza kwa udhati wa nafsi yangu sina budi kumpongeza Mhe. Waziri na timu yake, lakini neno magazebo bado nilikuwa nikiangalia kwenye kamusi neno magazebo sasa sijui ni mashamiana au *I don't know,* magazebo kwamba umeweza kununua magazebo yetu wenyewe na sasa tunafanya maonesho kupitia zana zetu wenyewe. Utakapo kuja hapa Mhe. Waziri ningependa kujua baada ya kuokoa hii hali ya kununua haya magazebo yenyewe kama ni kamusi nilikuwa naangalia kamusi lakini sikuliona kwamba kiasi gani cha fedha ambacho kwa hakika tume-*save* kutokana na kuwa sasa tunafanya maonesho kwa kutumia zana zetu. Kama ikiwa tunakodi tulikuwa tunakodi kwa kiasi gani na sasa hivi tunaonesha wenyewe kwa kiasi gani. Hiyo ni ukurasa wa 52.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo kwa heshima kabisa kwamba ndani ya Novemba 2017 Baraza hili lilipitisha mswada wa kuanzisha Baraza la Biashara. Hili ni jukwaa *white*, jukwaa huru kabisa na leo tupo katika mwezi wa juni ni juni hiyo kwamba ni lini jukwaa hili litakutana na kufanya majadiliano ya kibiashara na kwa uzoefu wangu hili jukwaa linachukua muda mrefu si chini ya kutwa nzima saa tatu mpaka saa nne usiku. Wafanyabiashara wanatoa pale maelezo yao na linakuwa ni jukwaa zuri tu na nishawahi kuhudhuria chini ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Muda umefika sasa sababu tena tunaingia katika mwezi wa tisa, kwa hivyo kwenye kitabu chako hukuzungumza kama lini jukwaa hili litaanza na pale ndipo tunapopata hasa *in and out* wafanyabiashara wanataka nini, wanakwazwa na nini na changamoto zao mbali mbali, haya mambo yote haya ya biashara ya Unguja na Tanzania Bara yatazungumzwa pale.

Kwa hakika katika *point* hizo Mhe. Waziri mimi sina mengi zaidi mambo mengi yameshazungumzwa katika bajeti yako, bajeti ambayo ni bajeti yenye kutekelezeka na yenye kuonyesha mswada mzima kama umekamilika na umeandaa kitakwimu hasa. Mara

nyingi nilikuwa nasema kwamba na tushakaa pamoja pahala Marekani ukanambia huu uchumi ni nini, ukanambia uchumi ni shimo ambalo kazi yake kupokea na kutoa, sasa mimi naamini kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar hakukosea kukuchagua kuwa Waziri wa Biashara na Mkwezi na Mkulima Bin Hafidh hakukosewa kuchaguliwa Naibu Waziri, hongera sana. Bila ya kuficha wananchi wengi wana matumaini sana hili niseme wananchi wengi sana na wafanya biashara hivi vikwazo vidogo vidogo vya ndugu yangu Jaku ni mambo ya kuweka sawa.

Lakini kwa hakika hasa ndani ya sakafu mama unafanya kazi nzuri mno tena wala huna kishindo. Nilikuwa nikifuatilia katika mijadala ya kiwanda cha sukari ambacho ni kikwazo kidogo ukiangalia katika hali ya *Input* na *output* na humu umehimiza kwamba waendelee kununua mashamba ya kuzalisha miwa. *Take my point* lakini pale pale inakuja *back to square one*. Ikiwa wao wataendelea kuzalisha miwa na kupatikana sukari kwa wingi lakini tatizo la soko bado lipo pale pale, lakini kama nilivyosema kwamba haya yote yanazungumzika na naamini wewe ni Waziri Mkongwe tena mkongwe mno. Naamini utatumia busara zako na mwanangu hapo au ndugu yangu Diaspora kuweka sawa hili jambo likae sawa. Unapozalisha mara nyingi unakuwa na soko vitu hivyo vinafuatana, kama huna soko makini utarejea kulia kwamba tuna mzigo mkubwa lakini *market* hakuna na kitu biashara maana yake ni neno la kiarabu biashara, nunua, zalisha, uza ndio linakamilika kuwa neno biashara.

Kwa hivyo Mheshimiwa kiwanda kile kiokoe kwani kimewekeza pesa nyingi na kinasaidia ajira na uchumi wa taifa letu Mhe. Mwenyekiti, mimi si mtu wa dakika nyingi kwa jumla natamka rasmi kwamba bajeti hii ya Wizara ya Biashara, Viwanda, Masoko naiunga mkono hasa kwa asilimia mia moja. Ahsante sana *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Ahmada Yahaya Abdulwakil, sasa naomba nimuite Mhe. Miraji Khamis Mussa na atafuatiwa na Mhe. Shaib Said Ali.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba ya Makadirio ya Wizara ya Biashara na Viwanda kuhusu Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Kwanza na mimi niungane na wachangiaji wote waliochangia kwa kuipongeza Wizara hii, kuwapongeza viongozi wanaongoza Wizara hii Mhe. Waziri, Naibu Waziri, Makatibu Wakuu na Wakurugenzi kwa hotuba nzuri na uwasilishaji mzuri wa bajeti yao. Na mimi inawezekana nikawa na buti mbili tatu lakini sio za kubwa ni nyepesi nyepesi zile angalau za kuzuia fungu ili tupate ufafanuzi mzuri kama Mhe. Waziri atashindwa kunijibu haya ninayoyasema.

Naomba niende ukurasa wa tatu aya ya nane katika maelezo Mhe. Waziri amezungumza vizuri na anasema muundo wa Wizara umebadilika kuna taasisi mbili hapa zimeanzishwa lakini mimi naizungumza hii ya Tume ya Ushindani halali wa kibiashara, *Fair Competition Commission.* Kwa ujumla Wizara ya Afya ina nafasi kubwa sana ya kuwawezesha wafanya biashara wetu wadogo wa kati ninakusudia wafanyabiashara wadogo.

Lakini kwenye viwanda vidogo, viwanda vya kati vile vya juu hatujafikia lakini Mwenyezi Mungu atatufikisha kwa uwezo wake. Hapa nataka tafsiri ya maneno halali ya kuwa Serikali imekuwa na adhma njema ya kuanzisha viwanda na nakizungumzia kiwanda cha sukari Mahonda, kiwanda ambacho Serikali imeamua wenyewe kukianzisha lakini kimekuwa kikizalisha na kinashindwa kuuza hata ndani ya Zanzibar sukari yake, maana sizungumzii kutoka kwanza Zanzibar hapa kwetu.

Lakini sigombani na adhima ya Serikali ya misamaha ile ya kodi kwenye bidhaa ambazo zinatupa unafuu mkubwa, lakini nataka majibu ya kuonekana kuna mkakati gani wa Wizara maana kuanzisha kiwanda ni jambo moja, lakini kuviendeleza ni jambo la pili, tusianzishe kiwanda chetu baadae sisi wenyewe tukakipiga vita. Maana kama kutakuwa kuna bidhaa tutakuwa tunaziingiza na zina msamaha mkubwa kiasi kwamba ile faida na dhamira ya Serikali katika kuanzisha viwanda na kuvisaidia ikapotea. Sasa nilikuwa nataka majibu ya ule mkakati na ule mpango wa Serikali kwenye majibu ya kitaalam ambayo yatatufikisha pahala pazuri. Viwanda tuwe navyo sukari tuingize nchini lakini wote katika hiyo *Fair Competition* maana yake ifanyike kwa utaratibu mzuri, kila mmoja afaidike.

Sasa ile dhamira njema ndio mtapata majibu mazuri kunako eneo hili kwa hivyo mimi nilikuwa naomba majibu ili tuone kama tuna dhamira njema ya kuanzisha viwanda na kuvilinda, ili kuweza kutengeneza ajira, kutengeneza mapato ya nchi lakini kutengeneza mustakbali mzuri wa kuwasaidia wananchi wetu, mimi sina tatizo sana lakini majibu niyapate vizuri. Kwa sababu nataka kujua azma ya Serikali.

Lakini aya ya tisa ukurasa huo huo wa tatu niliwahi kuchangia kuna matayarisho ya bajeti yamezingatia nyenzo muhimu zifuatazo, lakini niliwahi kuisema nyenzo moja tu na Mhe. Waziri ukanipa majibu. Kwa sababu sisi katika utaratibu wa kibiashara tuko katika makubaliano ya pamoja ambayo tunayapata kwenye *EAC*, tunayapata kwenye *SADC*, lakini nitazungumza suala la *Customer Union* ambayo ya 2005 muongozo wa 2004 niliizungumzia sana katika bajeti iliyopita. Lakini mara hii naizungumzia katika nyenzo ambazo zilikuwa zina umuhimu wa kuwekwa katika kulinda ule umoja wa kibiashara katika eneo hili na kuwafahamisha wafanyabiashara, kwa sababu maudhui mazuri, maelezo mazuri katika kitabu yana mtiririko mzuri na mbele huko nitachangia ili hapa nipate kukazia vizuri zaidi, sasa nyezo hii kwa nini isikae katika nyenzo muhimu ambazo tunazitumia.Kwa sababu kama tumo katika umoja ule wa jumuiya ile kwa nini suala hili tunaliacha katika nyenzo muhimu ambayo tunaweza tukaiweka na tukaitumia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niede aya ya kumi na sita ambayo mwisho kabisa inazungumzia *data,* lakini nilipokuwa nazisoma kwa ujumla nilipata *data* Zanzibar ilisafirisha kwa ujumla wa bidhaa zenye thamani ya Tanzania 145,756,000,000/= ambapo kwa jumla ya bidhaa za thamani za Tanzania Shs. sasa hapa ndio nataka Mhe. Waziri anisikilize vizuri akaana na 300,850,000,000/= lakini bidhaa hizi zilisafirishwa kwenye katika hilo la Afrika ya Mashariki, lakini baadae chini akaja na takwimu ya 300,793 ambazo zimekwenda Uganda tu ile Afrika ya Mashariki tuna nchi nyingi. Kwa maana

kwenye soko hili la *EAC* kuna nchi tofauti lakini ile 3,700, kwenye 3,800, maana yake jumla ni 3,800 lakini elfu 3,700 imekwenda Uganda tu.

Sasa kuna nchi kama Kenya tumepakana nayo na wenzetu wale wanaotoka Micheweni pale kuna biashara kubwa inafanyika, hivi hii asilimia iliyobakia maana hapa karibu asilimia 98% maana yake bidhaa hizi zimekwenda Unganda, kwa hivyo sisi soko tulilolitumia la Uganda na hii asilimia iliyobakia maana yake masoko yale mengine yote hatukupata kuyatumia kwa dharura ipi. Mhe. Waziri nahisi kama *data* hazijakaa sawa, lakini kama zimekaa sawa basi tupate ile tafsiri maana asilimia kubwa imekwenda Uganda, zile nchi nyengine katika jumuiya hii tumefanyaje.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba niende kwenye aya ya 17 lakini twende moja kwa moja kwenye chanzo kilichochora na WBV kutoka takwimu za *OCGS* ya 2018, nimekipitia kitabu katika maeneo mengi zile tafsiri za kiurefu kwa maneno kama haya *OCGS* maana yake sisi tukifuatilia tutaipata tafsiri yake, ukienda kwenye uchumi ukitengeneza data ndio utapata tafsiri yake. Lakini wale wakwezi na wakulima ambao mara nyingi alikuwa anawatetea Mhe. Hassan na ndio wanaotakiwa kufaidika na taarifa hizi hawawezi kujua. Kwa hivyo ule urefu wa ile *table abreviation* ipatikane ili kutoa tafsiri kamili kwa watu wetu, mimi sina tatizo na eneo hili, lakini nimkumbushe hasa mkwezi na mkulima asituandikie vitu ambavyo wakwezi na wakulima hawawawezi kuvifahamu wakati yeye ndie anawatetea.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niende aya ya kumi na nane, kumi na tisa na ishirini kuna maneno ambayo katika tafsiri ya kawaida na Wizara hii wenzangu walisema ina Waziri na Naibu Waziri wote wazuri katika kusimamia utaratibu wa kuandika taarifa, lakini katika uelewa ukiisoma Afrika ya Kusini katika tafsiri ya kiswahili maana sisi tukienda South Afrika maneno yale yanapotea, Afrika Kusini haiwezi kuwa Afrika ya Kusini.

Lakini na Sudan ya kusini katika ya hizo tatu nimezisema zinasema Sudan ya Kusini na South Sudan, sasa ile tafsiri na maana halisi sasa sijui wenzetu inawezekana nyie mmesoma katika shule za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sasa tupate tafsiri maana ile ya wakati mwengine nazungumza haiwezi kuwa South of Africa sasa hii Afrika ya Kusini au Sudan ya Kusini maana katika tafsiri ya kawaida maana yake South Sudan, South Africa kwa hivyo nafikiria nimefahamika katika kuandika tafsiri za kiswahili ambazo tunazitoa kwenye maana kamili, kwa sababu zinabadilisha maana hata ukenda katika utaratibu fulani naona tutafahamiana mbele tunakokwenda.

Lakini niende aya ya ishirini na nne ina ripoti ya bidhaa ambazo za vyakula ambazo zimetajwa hapa, lakini katika bidhaa moja ambayo mmeisahau ni ya samaki ina nafasi kubwa mmetaja bidhaa zote tungule, mbogamboga, viazi, viazi vitamu matunda, vitu vya *electronic* magari. Lakini samaki ni bidhaa na kama labda mlikuwa hamuwezi kuitaja nyinyi hajaitaja Waziri wa Kilimo na Mifugo na Uvuvi pia mtwambie, lakini hapa katika ile sura ya viwanda mbele ambako kuna aya ameizungumzia suala zuri tu la kwenda katika sera ya viwanda na viwanda ambavyo naamini Wizara inataka kuvishughulikia kikiwemo hichi kiwanda cha samaki.

Sasa tuna visiwa kama Pungume vinatoa asilimia kubwa sana ya samaki wengi tunakwenda kuwauzia wenzetu Tanzania Bara na visiwa vyengine kama Misali, Uvinje katika namna hiyo mimi nilikuwa napendekeza tu Mhe. Waziri mara nyengine basi na bidhaa ya samaki iingizwe, kwa sababu nayo ndio miongoni mwa bidhaa ambayo tunasafirisha.

Lakini naomba aya ya ishirini na tano kuna kipengele kinasema uingizaji mkubwa kutoka Tanzania Bara umetokea katika bidhaa za kilimo, vyakula, vyuma, magari, maji na vinywaji na dawa. Sasa mimi nazungumzia maji wenzetu wanatuletea maji lakini sisi kuyapeleka kwao ni tatizo maana mimi natumia sana maji ya *drop* na nateseka sana nikisafiri vyenginevyo nisafiri nayo, sasa lakini huku wenzetu tunakuta Kilimanjaro yote wanayaleta wao lakini yale ya kwetu hayendi, ya kwao yanakuja. Mimi sina tatizo la kuingizwa vya kwao, lakini nilikuwa nataka nipate tafsiri ya biashara katika nchi yetu hii yenye Serikali mbili. Kwetu sisi kutoa kwetu kwenda kwao kuna tatizo lipi? Labda sisi wafanyabiashara wenyewe tu hatujakuwa tayari kupeleka kule, lakini lazima tupate jawabu maana wao wanaingiza mimi sina tatizo la kuingiza lakini sisi fursa hiyo tumeikosa kwa misingi ipi tuna tatizo lipi. Sasa Mhe. Waziri naomba katika kuwasaidia wafanyabiashara na hapo uje unijibu.

Lakini aya ya ishirini na sita pia ina vikwazo vya kibiashara umevielezea, lakini inamalizia ukurasa wa kumi na nne ambayo hali inayoleta usumbufu kwa wafanya biashara wa Zanzibar. Hapa nataka kujua kwa sababu kila mara tunaona viongozi wetu mnakaa kupitia Wizara yako nataka kujua hatua mlizozichukua katika kutatua huu usumbufu maana mmeuripoti nyinyi wenyewe viongozi wa Wizara, kuna usumbufu basi tunataka kujua kwa sababu sisi tumekuja kuwatetea wafanya biashara na wakulima pamoja na wakwezi. Sasa tunataka kujua mpaka hatua hii tuliyonayo sasa kama Wizara mmechukua hatua gani katika kupunguza huu usumbufu maana huu usumbufu sikuusema mie mmeusema kwenye kitabu chenu, kwa hivyo tunataka kujua ule mkakati wa Wizara lakini na hatua mlizozichukua katika kupunguza huo usumbufu.

Lakini aya ya ishirini na tisa pamoja na lile table mimi hapa nina mchango ambao nitauzungumza kwa kubana kidogo, kwa sababu kuna maneno…….

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia dakika mbili.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Dakika mbili Mheshimiwa kama utazitizama vizuri utanisaidia kwa sababu nimebakisha sehemu kama nane hivi. Mhe. Mwenyekiti, katika aya ya ishrini na tisa niende haraka haraka ili nitume dakika vizuri kuna maneno kwenye hiyo *paragraph* ya mwisho kabisa ambayo yana neno kutoa, unafuu huko mbele siwezi nikazungumzia inamalizia ukurasa wa pili kwa sababu mwenzangu watakuwa wameshanielewa. Sisi tunaishi katika nchi ambazo za Jumuiya ya *EAC* taarifa nyengine kama hizi zinapokuja *direct* humu Barazani, sisi tunajua ni faida za watu wetu kujua lakini faida ya wananchi kuelewa lakini tutafute lugha ambazo *data* kama hizi na tafsiri kama hizi maana wenzetu wanaweza wakarusha ikawa ni sehemu ya kuandaa ule mgongano katika ule umoja tuliokubaliana, naamini nikizungumza hivyo Mhe. Mwenyekiti viongozi wanaoongoza Wizara hii wameshanifahamu.

Lakini niende katika aya ya 33 kuna kipengele ambacho hapa niwapongeze sana viongozi wangu, wanataka kuelekea kwenye kusarifu bidhaa za kilimo, uchumi wa bahari ikiwemo uvuvi na usarifu wa mazao ya baharini ambao sambamba na aya ya 41-42 zote zinazungumzia vitu vya aina moja. Mimi hapa niwapongeze sana, hatua hii ya serikali katika kujipanga kuelekea katika maeneo haya basi mimi nakupongezeni na muongeze bidii ili tuweze kufikia katika hatua njema ambazo amezikusudia. Lakini aya 39 nayo inazungumzia katika kutenga maeneo ya viwanda ambavyo vinashabihiana na tafsiri ya ile sera katika maeneo haya niliyochangia kwa uharaka wake ili nimalize.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Namalizia Mhe. Mwenyekiti, katika eneo hili naomba nishauri mambo yafuatavyo:

Ushauri wangu wa maeneo haya ambayo mnayatenga basi yasiwe ni maeneo ya kilimo, maana tutaenda kujenga viwanda lakini ushauri wangu yasiwe maeneo ya kilimo, tutenge maeneo ambayo yatakwenda na utaratibu mzuri. Lakini ushauri wangu wa pili yazingatiwe upatikanaji wa zile huduma, ziwe *resource* mbali mbali katika ujenzi ule. Mhe. Mwenyekiti, dakika chache lakini naomba niunge mkono hoja kwa asilimia 100 sina tatizo na Mhe. Waziri na wala sina tatizo la wizara hii niliyoyachangia nikipata majibu nitashukuru sikupata pia nashukuru zaidi. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Miraji Khamis Mussa anayefuata Mhe. Shaib Said Ali na Mhe. Mussa Ali Mussa.

Mhe. Shaib Said Ali: *Bismillah Rahman Rahim*, Mhe. Mwenyekiti awali ya yote tumshukuru Mwenye ezi Mungu kukutana leo hii mwezi 14 Ramadhan, mimi nimuombe tu Mwalimu Haroun kidogo anisaidie kusema chungu cha 14 ni halali katika hii sehemu zetu za mwezi au vipi ningemuomba kidogo lakini namuona kama hayupo.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri pamoja na Naibu wake na watendaji wake na Afisa Mdhamini kule Pemba pamoja na watendaji wake kwa kazi nzuri wanazotufanyia katika masuala ya wizara hii.

Pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri, uliokuwa hauna doa hauna matata na kadhalika na pia nimpongeze Mhe. Naibu Waziri, Naibu Waziri ambaye aliahidi kwamba atawatetea wakwezi na wakulima mpaka damu yake tone lake la mwisho la damu lakini juhudi yake itaonekana.

Mhe. Mwenyekiti, mimi leo mchango wangu sana katika wizara hii niende katika Shirika la ZSTC, kwa sababu Mheshimiwa tukataka tusitake kwamba bado zao letu la karafuu katika nchi hii, ndio kimbilio kubwa la wanyonge wa visiwa hivi. Kama ilivyo chama chetu cha Mapinduzi CCM na viunde vyama 100 katika nchi hii, lakini bado CCM itakuwa ni kimbilio kubwa la wanyonge katika nchi hii.

Kwa hivyo nasema kwamba bado na zao la karafuu na ziundwe sekta nyingi sana viwanda mwani watu wafanya lakini bado zao letu la karafuu litakuwa ndio kimbilio letu kubwa katika nchi hii. Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, mimi nina mambo kama matano hapa katika ZSTC naomba Mhe. Waziri anisaidie, na badala yake ampe mtendaji wake, Naibu wake mtoto wa mkwezi na mkulima ayafuatie masuala haya ili wananchi wapate kuelewa vizuri.

Moja Mhe. Mwenyekiti, nije katika mikopo, Mheshimiwa kuna manung'uniko makubwa sana tunajua kwamba Shirika hili hutoa mikopo kwa wachumaji wa karafuu au matajiri wa karafuu, lakini kuna manung'uniko Mheshimiwa kama mikopo hii:

(a) Kwanza huchelewa kutolewa.

(b) Kile ambacho mwananchi anakiomba kuhudumia ile kambi au nini huwa hakipati, hupewa tu kiasi cha kuhudumia lakini huwa hakipati kile, sasa kuna tazizo gani au kuna utaratibu gani mtu kupata mkopo ule.

Kwa hivyo mimi nikimuomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa kilio hichi cha wakulima hawa wa karafuu katika suala la mikopo basi anielezee, kuna changamoto gani kinachosababisha kwamba wananchi wale hawapati mikopo ile wanavyohitajia kwa wakati na pia kuna pungufu kubwa la ule mkopo anaouomba, kama mtu kakopa 200 anapewa 50, au 20 na kadhalika.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo hapo katika Shirika hilo hilo, nije katika suala la vipimo, Mheshimiwa hapa hana manung'uliko makubwa sana pana manung'uniko makubwa sana wananchi wanaopeleka mazao yao pale sijui wewe wenyewe wana vipimo vyao vya aina gani lakini wanasema kwawmba kuna upungufu mkubwa wa vipimo vyao wanavyovichukua uko na unavyovipeleka pale.

Kwa hivyo, Mhe. Waziri namuomba tu kwamba, alifuatilie suala hili kama ni la ukweli wananchi wetu wapate haki yao, na kama halina ukweli wowote basi wananchi waeleze tu, wananchi wanapima vipimo vyao kutoka nyumbani mimi nachukua gunia yangu hii ya karafuu nikifika pale nitapata kilo fulani, lakini anapofika pale kutakuwa na upungufu mkubwa sana. Sasa Mhe. Waziri mimi naomba aelezee tu, wananchi kuna utaratibu gani wa upimaji mpaka wananchi wananung'uniko vipimo vya karafuu wanaopimiwa haviendi sawa.

Nikiendea katika Shirika hilo hilo la ZSTC, viwango vya karafuu Mheshimiwa juzi niliuliza swali hapa kwamba kuna mashine za viwango bora vya karafuu, lakini nikatoa ushauri kwamba hapa wakati wa zao la karafuu msimu wa vuli Mheshimiwa karafuu nyingi hupotea. namuomba Mhe. Waziri basi na mashine ya ukaushaji wa karafuu iingie katika bajeti yake anunue kwa sababu kule Pemba karafuu nyingi hupotea. Ingawaje Mhe. Waziri alijibu kwamba hakuna karafuu iliyokuwa hainunuliwi, lakini mwananchi haitajii karafuu yake kuuza katika lango la mpeta.

Kwa sababu karafuu inapopigwa na mvua haiwi tena *grade* ya kwanza hubakia kuwa mpeta karafuu ile, kwa hiyo mwananchi pale akiwa tutapata chombo hichi cha ukaushaji wa karafuu kwa sababu pale matajiri hupata hasara kweli kweli na hasara ile huwa si ya matajiri peke yake mpaka wale wanaochuma karafuu, kwa sababu fedha yao hawalipwi kutokana na matajiri kupata hasara ile. Kwa hivyo namuomba Mhe. Waziri wafanye utaratibu wao wafanye utafiti, lakini chombo au mashine ya ukaushaji wa karafuu wainunue mashine hii, ili wananchi karafuu zile zipatikane zisiwe hazipotei tena.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo, katika shirika hilo hilo bado nilisema kwamba kuna vijana wetu wale waliokuwa wanamiliki mikarafuu kinyume na utaratibu, tunakumbuka kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, au serikali naipongeza kwamba safari hii, kulikuwa mikarafuu mingi sana ambayo wananchi walikuwa wameimiliki kinyume na utaratibu. Lakini wananchi hawa waliambiwa kwamba mikarafuu ile, serikali ilichukua lakini wakaambiwa kwamba watapata jasho kiinua jasho kidogo, au kiinua mgongo cha kuihudumia mikarafuu ile ikawa bado mpaka leo ipo, lakini Mheshimiwa cha kusikitisha ni kwamba tunaingia katika msimu wa pili wa zao lile lakini wananchi hawa mpaka leo hawajaambiwa chochote kwamba watapata ile fidia yao au hawapati.

Mhe. Mwenyekiti, nikimaliza katika suala hilo kuna njia yangu ya Mgelema Mheshimiwa naomba Mhe. Waziri anisikilize kidogo nataja njia ingawa atanambia naingia kwa nini naingia katika njia, Mheshimiwa njia hii ya Mgelema, Mgelema katika Pemba Mheshimiwa ni kijiji kimoja kinachotoa karafuu kwa wingi katika kisiwa chetu cha Pemba. Nimpongeze Mhe. Waziri kwamba shirika lake mwaka jana lilitoa fedha kuitengeneza njia ile, nashukuru sana ahsante nampongeza sana lakini Mheshimiwa tusingoje mpaka ng'ombe azae wakati tunamkamua maziwa ndio tumtafutie majani mazuri. Ile njia Mheshimiwa sasa imeharibika haipitiki tena hata kidogo nimuombe Mhe. Waziri kwamba bado ile njia ataihudumia tena basi aitekeleze na kama ndio mwaka jana hana haja nayo tena, basi anambie ili akija Waziri wa Ujenzi Mawasiliano na Usafirishaji nije kumbana katika njia ile, kwa sababu njia ambayo imeharibika wananchi wangu hawapati kupita hata kidogo. *(Makofi)*

Sasa niingie katika mchango wangu wa viwanda, nije katika mchango wangu wa viwanda Mheshimiwa mimi hapa kidogo nina masikitiko, Mheshimiwa Zanzibar tuna mambo mengi tunayoamua na tuna mambo sana tunayojipangia, lakini Mheshimiwa tunafeli katika masuala ya usimamizi. Mheshimiwa Zanzibar kama kweli tulikuwa na usimamizi wa viwanda, viwanda vilivyokuwepo Zanzibar hivi sasa ingelikuwa sisi tushafikia lengo la ishirini ingelikuwa tumeshafikia.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar kulikuwa na viwanda vya viatu, kulikuwa na viwanda vya soda, kulikuwa na viwanda vya sigara, lakini Mheshimiwa viwanda vile hivi sasa ni historia mtu tu. Mtu ukimwambia kama hapa kulikuwa na viwanda, kiwanda cha viatu kikiitwa mwendo haamini, lakini na kiwanda hicho kilikuwepo lakini Mheshimiwa usimamizi ndio uliotufikisha hapa tukawa leo tunaanza tena hapa kutafuta viwanda, sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri katika masuala yake ya kuanzisha viwanda hivi vidogo vidogo, ana mpango gani? ana utaratibu gani? kuna sera ngani itakayovisimamia viwanda

hivi mpaka vikasimama na vikaendelea tusije tukaja kutafuta mbinu nyengine huko mwisho, anielezee Mhe. Waziri hapa ni suala gani au mpango gani wa kuviendeleza viwanda hivi.

Zanzibar kuna viwanda vingi sana lakini usimamizi hatuna tatizo usimamizi hatuna, wananchi wanaanzisha viwanda lakini hawana usimamizi lakini matokeo yake kiwanda kile kinakufa baada ya siku mbili, kwa hivyo mimi nimuombe Mhe. Waziri katika moja ambalo namuomba anieleze ana mpango gani na masuala gani atakapo vianzisha viwanda hivi au hivi viwanda vilivyopo hivi sasa ana usimamizi wa aina gani mpaka viwanda hivi viweze kuendelea.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende katika hivyo vidogo vidogo Mheshimiwa. Mheshimiwa viwanda vyetu vidogo vidogo, bado ajira haijawapa kipaumbele wanawake kuna viwanda vingi lakini Mheshimiwa mwenzangu kasema kule Mhe. Suleiman lakini viwanda vingi vidogo vidogo, bado wanawake hawajafaidika navyo. Kwa sababu viwanda vingi vinatumia nguvu Mheshimiwa viwanda vingi vinatumia nguvu mimi ningemuomba Mhe. Waziri ajitahidi katika masuala ya kuleta viwanda au kubuni viwanda ambavyo na ndugu zetu wanawake watapata nao kufanya kazi katika viwanda hivi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nije katika viwanda vya usarifu, kwanza nimpongeze kwamba katika Jimbo langu la Pujini nimebahatika kupata kiwanda kimoja cha usarifu wa mazao, na kiwanda hichi kipo Pujini pale na kwa bahati nzuri Mhe. Haji Omar Kheri kiwanda kile alikwenda kukifungua katika Sherehe za Mapinduzi nampongeza sana, lakini Mheshimiwa masikitiko yangu ni kwamba kiwanda kile kimefunguliwa mpaka leo hakijafanya kazi na wala hakijakuwa na huyo mtu atakaeshughulikia hayo masuala ya usarifu wa hayo mazao mengine kipo tu kile kiwanda.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri kile kiwanda Mheshimiwa kisiwe gofu, kiwe kiwanda endelevu kwa sababu naamini kwamba katika kisiwa chetu cha Pemba kiwanda kile kitahudumiwa na wananchi wengi sana wa kisiwa kile cha Pemba. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri kiwanda kile akitafutie wafanyakazi, wenye sifa za kusarifu mazao, kwa sababu sasa hivi kiwanda kile anaekishughulikia ni mtu ambaye ni bwana shamba pale, sasa bwana shamba sijui kama anazo sifa zile za kusarifu mazao au kazi yake ni kupita katika kilimo tu nakadhalika lakini bado masuala yake hayo.

Halafu nikitoka hapo nije uimarishaji wa sekta ndogo ndogo mwani, chumvi na kadhalika, Mheshimiwa mimi katika jimbo langu sikubahatika kupata mwani kwa sababu ardhi yangu bado haikubali kuotesha mwani, lakini masuala ya samaki, ingawa Mheshimiwa Mwenyekiti wangu wa PAC Mhe. Miraji alizungumza kwamba mbona haoni masuala haya ya kiwanda cha samaki, lakini Mheshimiwa nnayo mabwawa ya chumvi katika jimbo langu na yanatoa chumvi sana.

Lakini ninaloliomba Mheshimiwa utaalamu bado mdogo, ndio ninaloomba pale ule usimamizi wa viwanda hivi uweze kutekelezwa ili wale wananchi wanapotoa yale mazao yao, tupate soko la kuuza ile bidhaa iwe bora zaidi. Bado utaalamu wa kuvua chumvi

pale au wa kutoa chumvi bado ni mdogo ingawa ni mwaka wa 10 huu, lakini bado utaalamu ni mdogo. Kwa hivyo mimi namuomba Mhe. Waziri viiwanda hivi au masuala ayafuatiye ili wananchi wapate kutekeleza. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi mchango wangu nimalizie kwa biashara zinazoingia au zinazopata msamaha wa kodi, Mheshimiwa hapa tuna kilio kikubwa sana, hususan katika huu Mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Huambiwa kuwa bidhaa nyingi sana zimeachiwa kodi, lakini Mheshimiwa mbona vitu havinunuliki madukani. Hii kodi mimi naongezea Mheshimiwa hii kodi inamnufaisha nani? Alitakiwa anufaike nani, anufaike mfanyabiasha au anufaike mlaji au mnunuzi wa ile biashara. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kuna manung'uniko makubwa sana hapa Mheshimiwa sasa hivi nathubutu kusema kwamba kutokana na upandaji wa bei kwa Mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani watu wengi sana walio wanyonge waliokua kipato chao ni kidogo, wanakula ule ule mlo ni sembe ni wali basi lakini Mheshimiwa vyakula hivi navyo vimepanda bei sijui kwa nini?

Sasa mimi nimuombe Mhe. Waziri, nimuombe Mhe. Naibu Waziri, naibu ulisema kwamba utatumia nguvu zako zote, jasho lako lote kuwatetea wakulima na wakwezi katika nchi hii, nikuombe kwamba bado wakulima na wakwezi wananyanyasika hususan kwa zile bidhaa ambazo zimetolewa msamaha katika huu Mwezi Mtukufu wa Ramadhan, bado bei inakwenda chini au bado inakwenda juu na wananchi hawa bado kipato chetu cha chini, na Mheshimiwa mimi nataka niseme kwamba kuna dhana mbaya sana, kuna dhana kwamba kwa nini hii biashara itolewe ushuru lakini kwa bei inabakia ile ile au hizi biashara huwa ni za wakubwa. *(Makofi)*

Hii Mheshimiwa ni dhana iliyoko kwa hivyo mimi naomba kwamba hii dhana iondoke, kwamba wale ni wafanyabiashara hawana *target* na wakubwa lakini Mheshimiwa hii dhana ya kuwa biashara zile kwa sababu haziteremshwi bei na msamaha umetoka lakini bado bei iko pale pale, ina maana hawa wafanyabiashara wanakula na wakubwa, kwa hivyo ningeomba Mheshimiwa hususan mkwezi na mkulima kilio hichi ukifuatilie kwamba bado bei ya mapembe iliyoingizwa humu mimi nakuhakikishia kwamba bei ya mapembe.....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako umemaliza.

Mhe. Shaib Said Ali: Ahsante bei ya mapembe kama ni shilingi mia moja na moja na hamsini huu, basi nyumbani kwetu kule Pemba inauzwa inauzwa elfu moja mia mbili na hamsini mpaka elfu moja na mia tatu, kwa sababu Mheshimiwa kuna usafiri wenyewe husema kuna usafiri kutoka Chake wakaja mashamba huku basi wanaongeza bei.

Mheshimiwa nakifikiri mama tumemsikia pale na mtoto wa mkulima na mfanyakazi amenisikia atalifuatila suala hili, naunga mkono kwa asilimia 100 lakini naomba kuwa maelezo niyapate. Ahsante Mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Shaib Said Ali anayefuata sasa ni Mhe. Mussa Ali Mussa na Mhe. Mohamed Said Mohamed ajitayarishe.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kunipa fursa hii ndogo niweze kuchangia Wizara hii ya Biashara na Viwanda, wizara ambayo ina waziri mahiri, waziri mzuri, waziri mzoefu pamoja na Naibu Waziri mtoto wa mkulima na mkwezi. *(Makofi)*

Pia nimpongeze Katibu Mkuu wa Wizara hii Ndugu Juma Ali Juma ambaye hivi karibuni alitoka Wizara ya Kilimo ni jirani sana na wizara hii, huyu kijana naye ni mzuri na ni hodari. Sitasahau kumpongeza Afisa Mdhamini Pemba Ndugu Abdalla naye ni kijana hodari nataka niseme kwa dhati kabisa kuwa wizara hii imeleta kitabu ambacho kinafahamika kitabu kizuri kinaeleweka hakina matatizo hongereni sana, Wizara ya Biashara na Viwanda.*(Makofi)*

Mtukufu Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohamed Shein ametambua kwamba nyinyi ndio watu wa biashara, sasa na nyinyi nataka hasa yule mtoto wa mkulima athibitishe kwamba sisi ni kweli ni watu wa biashara. *(Makofi)*

Sasa nianze mchango wangu, mchango wangu uko kwenye zao kuu la taifa, zao la karafuu, zao hili ni ndugu baba mmoja mama mmoja na mvua hasa inapokuwa kubwa. Mwaka jana, zao hili tulipata tani 6,700 ingekuwa haikunyesha mvua basi tungepata hata tani milioni moja. Tatizo kubwa ni mvua ingawa nayo mvua ni neema, lakini karafuu ikiwa nyingi na mvua inakuwa nyingi. Sasa mvua inapokuwa nyingi zao hili tunalikosa, maana yake linaoza, likiwa juu linaoza, likiwa chini linaharibika.

Mhe. Mwenyekiti, ningemshauri mtoto wangu Waziri katika Wizara hii, katika bajeti hii tuliyonayo basi alifikirie zao hili kwa kulipatia vifaa ambavyo vinaweza kusababisha visioze pindi ikitokezea mvua. Vifaa hivi atavipata katika nchi ya Uchina ambayo ni nchi jirani inayounga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Akatafute mashine mbili kubwa, mashine moja aifunge Zanzibar kule kwetu Donge kwa shemeji zangu na mashine moja aifunge Mkoani Pemba, ikitokezea mvua kubwa na zao hili limeshakuwa tayari basi watu wote wapeleke karafuu zao kwenye mashine zile ili kwenda kukaushwa.

Mhe. Mwenyekiti, tunataka zao hili lisipotee hata sekunde moja, hata karafuu moja isipotee wala isioze, karafuu zote tunataka tuzipate kukiwa na jua kukiwa na mvua. Karafuu ndio uchumi wa nchi yetu unaofuatwa sasa hivi tukitoa utalii. Jambo hili namuomba Waziri alishughulikie kwa haraka sana ili tupate zao hili kwa uhakika na tulipate lote.

Mhe. Mwenyekiti, pia namuomba Mhe. Waziri ashirikiane na Wizara ya Kilimo, kwa sababu zao hili linahitaji kupandwa kwa uweledi. Watu wa kilimo washirikiane na Wizara hii ya Biashara na Viwanda, wapande mikarafuu kwa wingi, vijana wahamasishwe kupanda mikarafuu. Mikarafuu ni ajira hasa na Mheshimiwa aingize bajeti katika miche ya mikarafuu ili ipatikane kwa wingi, mara hii miche ya mikarafuu haikupatikana ukilinganisha na mwaka jana, mwaka huu miche ya mikarafuu imekuwa

kidogo, haitoshelezi. Sasa hivi watu wamehamasika, mtukufu Rais ameifanya karafuu kuwa ndiyo almasi ya nchi hii. Watu wote sasa hivi wako tayari kupanda mikarafuu. Mhe. Waziri jambo hili liangalie ili ushirikiane na Wizara ya Kilimo ipatikane miche ya mikarafuu kwa wingi na ipandwe sana.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Waziri wa Biashara na Viwanda kwamba zao la karafuu wataalamu wake na wanaolihudumia na wanaolikubali ni wananchi hasa wa Pemba Jimbo la Ole. Ole ndio watu wanaochuma karafuu kwa wingi. Jimbo la Ole ndilo linaloshughulikia karafuu Pemba nzima, unasikia karafuu zimekodiwa basi wanaokodi karafuu wanatoka Ole, sio pahali pengine popote. Umo mwengine utakuta Wingwi 10, Mchangamdogo 8, Mkoani 40, lakini Ole asilimia 90 wote wanashughulikia zao la Karafuu.

Ukifika msimu wa karafuu nataka wananchi wa Jimbo langu la Ole wote wapate mikopo ili wakalishughulikie zao hili. Zao hili kwao ni muhimu sana na ni wazalendo wa kulihudumia zao hili. Vile vile kuna wananchi wanaokaa sehemu mbali mbali kwa mfano mtu anakaa Vitongoji ana mikarafuu yake miwili Mtambile, Mikarafuu hiyo kaipata kwa njia ya mirathi, mtu huyu hawezi kutoka Vitongoji akenda kujenga kambi Mtambile hiyo haiwezekani.

Mhe. Mwenyekiti, sasa siku hizi kuna usafiri Zanzibar ina barabara zimepita mpaka vijijini ukitoka Chambani kuja Ole ni dakika 2. Serikali ya Mapinduzi imejenga mabarabara kila mahali ambaye tena hataki ni hiyari yake. Mtu anatoka Vitongoji anakwenda Kipapo kuchuma karafuu zake na mkewe na wanawe wakati wa kurudi saa 9 akifika njiani anabambwa, karafuu zina mashada, sio kavu anapata tatizo mpaka anafikishwa polisi. Hapa hapana magendo huyu, anatakiwa tu achukuwe kibali tu kwa Sheha kwenda kuchuma karafuu zake. Akiziacha kule zitaharibika na haiwezekani mtu mmoja aende akajenge kambi kwa mikarafuu miwili. Kambi ya karafuu inaanzia mikarafuu 100 na kuendelea au mtu anayekodi karafuu. Lakini kambi ya karafuu haiwezi kusimama kwa mkarafuu 1 au 2 huyu aruhusiwe kuchuma karafuu zake na kupeleka kama Vitongoji, Pujini au Chakechake kwenda kuanika, ilimradi Sheha anatambua, diwani anatambua, Serikali ya Wilaya inatambua, kamati ya ulinzi kibali anacho, hili lisiwe tatizo, likiwa tatizo hili karafuu nyingi tutazikosa.

Twende kwenye mpeta, kumekuja tifu kubwa kuhusu watoto na akina mama wanaokota mpeta. Nasema Mhe. Waziri karafuu ni neema, neema inapoingia kila mtu anastahiki kuipata. Zamani watoto skuli zikifungwa wanakwenda kuchuma karafuu na kuokota karafuu, kina mama na wao walikuwa wanakwenda kuchuma karafuu au kuokota karafuu. Kina mama wengine hawapandi juu inabidi wakae chini, baba anapokuwa juu akimuona mwana mama chini yupo hachoki kuchuma karafuu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, vile vile mwana mama ameondoka kwa mfano Wingwi amekaa huko Wingwi haonekani, amekwenda kuchuma karafuu kwa mfano Mtambile kule anaweza kupata riski akapata mume akaolewa. Maana karafuu ni neema na hiyo ni neema kuolewa. Kwa hivyo suala la mpeta libakie pale pale, akina mama waokote, watoto waokote, neema ipatikane, faida ipatikane. Akina mama wengine wale ninakokula mimi

kwa mama nitilie ninako futari, wale na wao huhamasika, wakatoka Bara, Unguja, wakaja wakawapikia vibarua siku za Ijumaa inakuwa ni furaha kubwa sana. Akina mama ntilie na wao wapewe nafasi waje wawapikie wachumaji wa karafuu kwa sababu karafuu ni neema, karafuu ni faida katika nchi hii.

Tuondoke kwenye karafuu twende kwenye mwani. Mhe. Mwenyekiti, nataka nikuombe Mhe. Waziri mwani nao ununuliwe na serikali, wakulima wa mwani wanadhalilika, ile kazi ya mwani ni ngumu tena ni ngumu sana, maana mwani unapandwa baharini. Hebu angalia mtu akakae baharini apande mwani halafu auvune, aukaushe, anakwendanao kwa tajiri anapewa kilo sh 400/ zile kamba, matatizo, yote yale tajiri hayaoni anakwambia hauna soko. Wakati huko Philipino mwani unaliwa ni chakula na hapa kwetu sisi mwani sasa ni chakula, vipi uwe hauna soko.

Mhe. Mwenyekiti, naiomba serikali hii tukufu hasa Wizara hii ya Biashara, Wizara ya mkulima, Naibu Waziri mkulima, angalia wakulima wa mwani wape, nafasi na wao sasa nunua mwani, usafirishe mwani, hiyo ndiyo ajira. Tulisema kwamba serikali yetu itatoa ajira, sio lazima ajira zote zitoke serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, sasa tutoke kwenye mwani, mtoto wa mkulima nakwambia Pemba kuna neema kubwa ya embe, sasa hivi tungule hatuagizii tena Tanga, tunalima wenyewe Wapemba tumeamka, tumetoka kule tulikotoka sasa tunakuja kupya. Embe sasa hivi zinaharibika ovyo, embe zikipea zinapea kwa umoja, tungule zikipea zinapea kwa umoja. Hebu lete kiwanda pale Mchangamdogo kati kati ya Pemba watu wa Micheweni, watu wa Wingwi, Ole, Pandani, watu wa Mtambwe kwa ndugu yangu yule, walete pale embe tufanye kiwanda tupate juisi zetu wenyewe, tuache kuagizia juisi wakati matunda ya kufanya juisi tunayo.

Mhe. Mwenyekiti, tungUle sasa hivi Pemba inapatikana bila ya kuagiziwa Tanga, nayo inapotea hivyo hivyo, Pujini wanatoa tungule nyingi. Mhe. Shaibu Said Ali yupo hapa anajua. Tutengeneze tomato zetu tusinunue tena matomato yale yanachanganywa na michanga kuharibu afya zetu.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niunge hoja kwa asilimia 100 kwa sababu sina sababu ya kupinga hata moja na Wawakilishi wenzangu nawaomba tumpe nafasi huyu dada aende akafanye kazi yeye pamoja na mtoto wake. Ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mussa Ame Mussa na sasa naomba nimwite Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) na mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame kwa leo.

Mhe. Mohammed Said Mohammed: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini kwa masikitiko mkubwa sana pengine nisiweze kuchangia kama nilivyo tegemea. Kwanza kutokana msiba mkubwa wa jirani yangu uliotokea hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri, lakini kuwa mahiri sana katika utekelezaji wake wa kazi zake.

Vile vile nimpongeze sana Mhe. Hassan Hafidh Ameir Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda kwa uteuzi wake mkubwa na Mhe. Rais nataka kusema hakukosea kafanya kitu cha uhakika.

Mhe. Mwenyekiti, nianze katika ukurasa wa 13 kwenye hotuba hii ya Mhe. Waziri kushuka kwa samani ya usafirishaji ya biashara kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara. Nilikuwa nataka kujua tu ni kitu gani kilichoathiri, ukiwemo mfumo wa bei kutokana na gharama kubwa au bidhaa za nje, naomba kupatiwa ufafanuzi namna gani Wizara imejipanga katika kukabiliana hali kama hii, ili tuone namna gani wafanyabiashara wa Zanzibar wanafaidika katika soko hili la Bara.

Mhe. Mwenyekiti, soko la Bara linatupa ukakazi mkubwa sana. Tulikuwa na Viwanda vya Mahonda, Viwanda vya Maji, lakini leo Zanzibar utakuta kuna viwanda vingi sana vya maji lakini maji yake huwezi kuyakuta Bara. Lakini vile vile Bara kuna viwanda vya maji lakini maji yake utayakuta Zanzibar. Jengine kuwa Zanzibar kuna Kiwanda cha Sukari na Bara sukari yao inakuja Zanzibar ya Zanzibar haiendi Bara. Nataka kujua nimeona katika hotuba yake humu Mhe. Waziri anasema bado majadiliano haya yanaweza yakaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kusema Mhe. Waziri awe mkweli sana wakati anapozungumza jambo hili awe mkweli kwa wananchi wa Zanzibar, kuwa mazungumzo hayafanyiki, wameshakutana mara nyingi hakuna kitu kinachokuwa. Mimi naomba tuwe wakweli na tumefunga Ramadhani hivi vitabu visituhadae kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kwenda ukurasa wa 15 katika kitabu hiki cha hotuba ya jaduweli, 15. Uingizaji wa sukari ni mkubwa kuliko mahitaji ya kupelekea bakaa kubwa sana. Hali hii inawezekana kuathiri kiwanda chetu cha Mahonda, kwa nini tunaagiza sukari wakati Kiwanda hiki kipo. Juzi Bara wameagiza tani elfu sabini, mia tatu na hamsini (70,350) Zanazibar inataka kuingiza tani 1,000 tu Bara haiwezekani. Napata kigugumizi sana.

Mhe. Mwenyekiti, niondoke hapo niende kwenye ukurasa huo huo paragraph ya 29, inaelezea kuwa bei muhimu za mchele na unga na sukari. Serikali imekuwa inatoa *exemption* mwezi kama huu wa Ramadhani lakini *impact* safi kwa wananchi haionekani. Bei inauzwa vile vile na Mheshimiwa amejinasibu kuna Idara au Kitengo kinachoratibu bei. Hichi ameambiwa ukiangalia mchele atwambie Mhe. Waziri mchele huu shilingi ngapi, huu shilingi ngapi, asiseme tu kwa bei hii aliyoitaja humu ndani. Wananchi wanaumia sana, msamaha watu wanapewa wanautumia sivyo, tungeomba tuangalie kwa haraka haraka bei hizi alizozitaja na katika ongezeko la soko la dunia na utulivu wa bei uliokuwepo Zanzibar ukoje. Hakuna utulivu wa bidhaa Zanzibar, bidhaa za Zanzibar zinakwenda zina *fluctuate* kila siku. Ukenda dukani leo imekuwa hivi utafikiri mafuta, hayo mafuta tutasema si yetu ZURA wanapandisha wanavyotaka. Lakini bidhaa hizi tunatoa ushuru na hasa katika mwezi huu.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Rais anaposimama anasema Mwezi huu wa Ramadhani tuoneane huruma, lakini siku ya pili bei ndio zinazidi kuliko pale alipokuwa hajasema.

Sasa mimi nimuombe Mhe. Rais bora ata asiseme, kwa sababu akisema ndio wao wanatuzidishia, wananchi wanapata tabu, siye tulioko chini.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 16 la Jaduweli Nam 2 inaonyesha wastani wa bei za reja reja kwa chakula muhimu katika Soko la Dunia hilo kuanzia 2018 kulikuwa na 1200 lakini kipindi cha Julai mpaka Septemba 1250. Naanza sasa kumpa ile *trend* ya bei hizi zinavyotoka, hazitii ushawishi mkubwa sana kwa serikali yetu kuweza, lazima tukaze buti tuweze kuweka *constant* ya bei ile ambayo tunaitaka.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye ukurasa wa 17 wa kitabu hichi vile vile, unazungumzia hali ya viwanda na ujumla wake, suala ambalo tunaweza tukajiuliza Wizara kwa kauli nyepesi tu, serikali kwa ujumla ikiwa tunataka kuvutia wawekezaji zaidi je, wana vivutio gani *incentives* ambazo zitapatikana kwenye viwanda. Mimi sio muumini mkubwa sana wa kusema Zanzibar ndio nchi ya viwanda kama wenzetu sera yao ya Bara. Kwa sababu Zanzibar tuna *incentive* gani za kuvutia, tumejitayarisha vipi. Mheshimiwa hebu akija anambie amejitayarisha vipi na *incentive* ambazo zinaweza kupatikana kwa wawekezaji ambao tutawashawishi kuja kuwekeza katika Viwanda vyetu mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu nikasema siyo muumini naona tuna Kiwanda kimoja cha Mahonda kinatushinda, lakini tuna Viwanda vinne vya maji vinatushinda, tunapata leo maji ya uhai, maji ya dasani, maji ya Kilimanjaro yapo hapa, kwetu kule mbona hayendi kwa wenzetu kuna nini. Mheshimiwa hebu ukija unambie na ninaomba sana niweke nia na makatibu mnisikilize vizuri nina nia ya kuchukua mshahara wa Mhe. Waziri.

Lakini niende kwenye ukurasa wa 23 *paragraph* ya 45, Mheshimiwa naomba niinukuu kwa heshima yako.

> "Wizara imeeleza kwamba ina mpango wa kufanyia usarifu zao la mwani na kutengeneza bidhaa za mwani na pia inafanya utafiti wa soko la bidha hiyo".

Hata hivyo, haijeleza usarifu huo utafanywa lini kwa uhakika gani na je serikali imejipanga vipi yenyewe, kwa sababu haya maneno tushapata kuyasikia sana wakati anajibu suala Mhe. Waziri, leo hapa alisema usarifu wa mwani umetoka kwenye mambo mengi, lakini wamejipanga vipi hebu tuambiwe watawawezesha vipi, wananchi wanalia kila siku bei ya mwani ndogo hebu tuambie tumejipanga vipi.

Mheshimiwa, soko lake likoje naomba na nimalizie kwa kitabu hiki ukurasa wa 88 kiambatanisho namba 1, kinahusiana na mwendo wa biashara Zanzibar kwa kipindi hichi cha mwaka 2012 – 2017 kinaoneshwa uingizaji wa viwanja nchini umekuwa ukiongezeka kulinganisha na usafirshaji wa bidhaa. Kwa kuwa miongoni mwa majukumu ya wizara hii ni kuwepo mwa ushindani halali wa kibiashara ili kumlinda mtumiaji.

Sasa suala langu ni jepesi sana tu je! jinsi ya takwimu zilizoonesha kwa namna gani wizara imejipanga katika kulinda wazalishaji wa ndani kwa kuwa kuna uingizaji mkubwa wa bidhaa nchini na je! wamezingatia vipi mtumiaji katika uwekaji wa bei za bidhaa

hizo, nilikuwa nataka kujua tu lakini hata hivyo ni muhimu kuipongeza sana wizara kwa namna kitabu chake kilivyojipangia vizuri sana. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba niende kwenye kitabu kikubwa lakini kabla ya kitabu kikubwa niliona mfumo hapa kielotroniki wa kuandaa mfumo wa usajili wa kutumia mtandao wa kusajili biashara nikaona wameweka *model* mbili, *model* ya kwanza ni usajili wa taasisi za kibiashara, lakini nyengine wameweka usajili wa amana kwa mali zisisohamishika, ambao unatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni.

Mhe. Waziri nikupongeze sana kwa kazi kubwa ambayo hiyo unaweza kufanya, lakini tunatumia mfumo huu utakaongeza gharama za uendeshaji wa BP (RA) jambo ambalo haliwezi kuepukika na matatizo yetu na itosheleze kuwa Bajeti ya BP (RA) inakuwa ni ngumu sana.

Mhe. Mwenyekiti, wizara inabidi ifanye mpango maalum wa kuelimisha jamii kuhusu matumizi ya mfumo huo hakuna bajeti inayotosha katika kazi hii. Mheshimiwa lakini kubwa zaidi ni kuangalia maslahi ya hawa wataalamu ambao tutawaweka hapa. Maana yake tumezoea kwenye serikali hii kuwasomesha watu Chama cha Mapinduzi kinawasomesha watu vizuri, lakini baadae wanakimbia.

Sasa nimuombe Mhe. Waziri kuzingatia sana kuweza sana watu hawa wasikimbie na tuweze kujua maslahi yao tunawapa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye kitabu kikubwa naomba Mhe. Waziri, afike na mimi kwenye kifungu cha RO (1) kwenye namba 3 kuna viashiria hapo, kiashiria kimoja kinasema:

“Uandaji na uibuaji wa sera na tafiti za wizara idadi ya tafiti zilizofanywa katika mwaka 2017 – 2018 imefanya tafiti 2 lakini 2018 – 2019 amepanga tafiti 9 lakini *target* ya mwaka 2019 – 2020 kapanga 3 na inayoendelea kapanga 3”, sifahamu vizuri ningeomba tu ufafanuzi.

Lakini vile vile kuna *target* ya 2, “Idara ya Sera iliyofanyiwa mapitio na ziliandaliwa” 2017 ilifanywa 1 lakini nyengine zimefika 2,2,2 pia nilikuwa naomba hapo nipate ufafanuzi.

Lakini vile vile usimamizi wa mamlaka katika ukurasa wa RO (1)5, chini kabisa “Usimamizi wa mamlaka zinazotowa leseni” idadi ya mamlaka zinazotowa leseni zimehakikiwa mwa 2017 – 2018 (25) lakini zilizobaki zote pamoja na *target* za mbele zimekuwa 45, sasa nilikuwa nataka kufahamu tu kwa nini zimefikia hivyo.

Lakini jengine katika ukurasa wa RO (1) 16, kuna Shilingi 2,000,000,000/- zimetengwa katika kifungu kidogo HRO 104010 4 udhibiti na ubora wa bidhaa zimepangwa Shilingi 2,000,000,000/- 2017 – 2018, lakini 2018 – 2019 hakikupangwa kitu na hakuna *target* ambayo ipo, ningemuomba Mhe. Waziri anapokuja aniambie.

Mhe. Mwenyekiti, huwa nnashangaa sana kila mara tunapokuja Mhe. Waziri anakuja tunaendelea haya mambo mengine tunasema yanaendelea kuimba na sijui wimbo huu utakuwaje wakati jana wasanii walikuwepo lakini leo kitabu hiki tunaendelea kusema. Ukikiangalia kitabu hiki nina wasiwasi na takwimu ambazo zipo, takwimu za bidhaa nyingi zimepikwa nimuombe Mhe. Waziri atwambie hapa alifatilia vipi takwimu hizo.

Mhe. Mwenyekiti, leo nilitaka nizungumze mambo mengi sana lakini kutokana na msiba huu siko sawa naomba niunge mkono hoja kwa asilimia 90% asilimia 10% naomba nichukue mpaka nitakapopata maelezo nikushuru sana.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa), na sasa naomba nimwite mchangiaji wetu wa mwisho ambae ni Dr. Mwinyihaji Makame katika mchangiaji wa mwisho kwa siku ya leo.

Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini: Mhe. Mwenyekiti, na mimi kushukuru sana kupata wasaa huu mdogo kwa kuweza kuchangia hotuba hii muhimu sana ya mustakbali wa biashara na mwenendo wake wa uchumi kwa ujumla katika nchi yetu hasa ukizingatia kwamba kuna mazao makubwa ya uchumi, moja wapo ikiwa karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi naomba niungane na wenzangu kwa sentesi moja tu, kumshukuru Mhe. Waziri na Naibu Waziri na timu yao kwa kazi kubwa sana na kitabu kizuri kabisa kilichojaa takwimu na mambo ya msingi sana kuhusu wizara yao.

Naomba moja kwa moja nisipoteze muda zaidi nende kwenye kitu kikubwa cha nchi yetu karafuu, na mimi niwapongeze sana wenyewe *ZSTC* pamoja na wizara na serikali kwa ujumla kwa kutetea sera ya nchi yetu ya kusimamia suala zima ya kuifanya zao lao la karafuu kuweza kununuliwa au kudhibitiwa na serikali na hasa kutoa bei yenye asilimia 80% ya bei ya kuuzia nje yaani mkulima wa karafuu analipwa asilimia 80% ya bei ambao serikali inauza nchi za nje.

Hiyo ni kwa kweli ni hatua moja kubwa sana serikali tunaipongeza sana na kwa nini serikali imefanya hivyo, imefanya hivyo kwa sababu kulikuwa na watu wanataka kutupeleka njia nyengine walikuwa wanataka tutaifishe zao hili, biashara hii ifanywe na watu wachache au ibinafsishwe na nini hatima yake, ingekuwa magendo. Lakini serikali ikajipiga moyo konde ikasema hata, sisi hili suala tutalichukua wenyewe na *Alhamdullilah*, tunaishukuru sana Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kulisamamia hili na Mhe. Waziri kasimama kidete tunamsikia safari zake za Pemba anavyofanya kazi na wizara nyengine *multi- sectoral,* wizara mbali mbali kulifanikisha hili suala. Hongera sana Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo nisije nikaondoka kumezungumzwa kwamba katika karafuu walizonunua *eight thousand tonnes* tunawapongeza sana nafikiri ni rekodi nzuri *so far*. Mimi nakumbuka rekodi ya mwisho ilikuwa kama tani 10,000 na ushei hivi, kunako sixty hizi huku na ambayo haijafikiwa kwa muda mrefu sana. Sasa mimi niwapongeze sana.

Je, katika hao watu waliokopeshwa madeni yale wameshalipa yote, au kiwango gani cha madeni bado yako kwenye mikono ya wananchi? Nimejaribu kuitafuta *statement* hiyo kwenye kitabu cha Mhe. Waziri sikuiona, najua ni wachache tu kwa sababu madhali mifuko imejaa naamini wananchi wengi wamelipa madeni yao. Lakini tulitaka tujue tu tuweze ku–*compare* na ku-*construct* hizo takwimu, kiasi gani basi hayo madeni bado wanayo wananchi.

Vile vile shirika wamesema kwamba kwa mwaka ujao wamepanga kununua karafuu za kilimo cha Ugani kwa Sh. 17,500/-. Hebu Mhe. Waziri aje atuelekeze wengine tushakuwa wakulima wa karafuu na Mheshimiwa nakuomba ukipata nafasi na timu yako na mimi uje unikague ili uniingeze kwenye mpango wake.

Mhe. Mwenyekiti, tulitaka kujua hicho kilimo cha Ugani kwa mikarafuu anataka nini na nini tufanye na wakulima wengi pengine bei kubwa sana hii, ukilinganisha daraja la kwanza kwa kawaida Shilingi 14,000/- hii 17,000/- kwa kweli bei nzuri sana. Kwa hivyo, aje utuelekeze kwa Maafisa wako watuelekeze nini tufanye.

Mhe. Mwenyekiti, niende kwenye eneo la viwanda. Mheshimiwa niipongeze sana wizara, sera nzuri hii na muono wa mbele kabisa ambao serikali yetu nao kuhusu uchumi wetu ambao tuweze kufikiria viwanda. Tunapozungumza viwanda unajua kuna viwanda vyengine *row materials* ziko za hapa hapa, lakini kuna viwanda vyengine malighafi unaweza kuitoa nje ikawa kama unafanya *transition trade* zinapita hapa unatengeneza unatoa yote yanafanyika na mifano ipo tu kama nchi za Singapore na kwengineko.

Mhe. Mwenyekiti, wazo hili ni zuri sana kwa nchi yetu na naamini tukilisimamia vizuri linaweza likatupeleka pazuri sana. Kweli wenzetu wamezungumza wengine kuna viwanda vidogo vidogo vimekufa, viwanda vya viatu, viwanda vya sigara, lakini kufanya kosa ni sehemu ya mwanaadamu lakini kurejea kosa ni kosa, tujipange vizuri tuone sasa kwa *model* za kileo biashara hiyo na viwanda hivyo vinapangwa vipi.

Mhe. Mwenyekiti, nampongeza sana kwa wazo lake la kuweka hayo maeneo kiwilaya kama alivyosema. Mimi nataka kumuomba Mhe. Waziri kule Ethiopia mji wa Hawasa juzi nimesoma kwenye gazeti kuna *industrial pack* moja kubwa sana Wachina wameijenga kwa miezi tisa na imezunduliwa tokea mwaka 2016. Rais Kagame unamjua ni hodari sana wa kusoma na kuigiza. Juzi alikwenda kutembelea na akaona *model* za viwanda vilivyopo pale vya vitambaa na nguo, yaani *model* yake kwa duniani inaongoza kabisa. Sasa ningemuomba sana Mhe. Waziri haya maeneo ya viwanda *industrial parks* anazotaka kuzijenga katika wilaya basi hebu afanye safari ende Hawasa, Ethiopia pale akasome wamefanya vipi wenzetu, wamepanga vipi na wanakwendaje. Naamini kabisa japo wao ni eneo kubwa lakini hayo madogo madogo anayotaka kuyafanya ya kiwilaya yanaweza kutusaidia na kutuongoza na sisi tufanye vipi.

Mhe. Mwenyekiti, wanasema wanatarajia mapato ya Shilingi Bilioni 2 kwa mwaka katika eneo hilo. Kwa kweli ni *income* kubwa na naamini itasaidia sana uchumi wa nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naomba niunganishe kwenye viwanja vya maonesho yale ya biashara. Nimesoma hapa Mheshimiwa azma yake ya kuendeleza Kilimani na maeneo yale. Sasa nakumbuka wizara walipewa eneo la Nyamanzi jimboni kwangu kule, lilipimwa lile likazungushwa senyenge kwa muda mrefu kabisa sijui wamefakia wapi au tena Mheshimiwa keshapata mpango mwengine na Wizara lile wameliacha, nafikiri huo mpango upo labda ningemuomba sana Mheshimiwa na mimi kidogo nina jimbo nitafurahi sana na namshawishi eneo lipo kubwa, bado wazo lake la kufungua eneo la maonesho na litakuwa la kudumu sio la kuhamahama. Kwa hivyo, ningeomba sana afikirie lile wazo kuliendeleza.

Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa wa 22, Mhe. Waziri alivyozungumza suala la umuhimu wa utafiti na mimi nimpongeze sana, usipofanya utafiti hasa kwenye mambo kama haya ya kilimo, mambo ya viwanda mambo ya biashara kwa kweli utakuwa hutizami nyuma unafanya nini na huna muelekeo hujui na utizame wenzako wanafanya nini.

Kwa hivyo, mimi nampongeza sana, tunavyosema *research* unaangalia wenzako walichofanya na wewe unafanya nini na unalinganisha matokeo kwa aliyofanya mwenzangu ndio au sio wewe sasa unafanya nini.

Kwa hivyo, mimi nampongeza sana wazo hili Mheshimiwa anasema anashirikiana na *COSTEC,* anashirika *UNIDO,* anashirikiana na wengine. Lakini nataka kumuomba sana Mhe. Waziri kuna kazi kubwa sana walifanya Waingereza *ODA, research* kubwa sana juu ya mazao haya ya viungo na bahati nzuri sana mmoja wapo ambaye *scientist* anae mwenyewe Katibu Mkuu. Katibu Mkuu wa wizara yake alifanya nao kazi Waingereza wale bega kwa bega walikwenda kila kona mpaka wakamalizia Daya Mtambwe kule.

Kwa hivyo, mimi ningemuomba sana ndugu Katibu Mkuu anajua mpaka *literature* zilipo na ripoti zilipo na *finding* zinazopatikana naamini hapo walipo waunganishe na haya wakina *UNIDO* naamini tutafanikiwa mpaka *market survey* walivyosema wanataka kufanya sasa hivi basi wao wamefanya, walikwenda Kenya wakenda Bara yote hayo wakalinganisha.

Mhe. Mwenyekiti, hapo hapo kwenye utafiti sikusikia kwenye ukurasa wa 36 – 37 kataja miongozo mbali mbali ambayo wameipata baada ya utafiti ule uliofanywa na *AU, Trade come,* na wengineo juu ya *value chain analysis on agro processing industry for spices sea weeds and hot culture* sasa mimi niko hapa kwenye *hot culture* kwenye mengine nasema muongozo umeandaliwa umepatikana na umesaidia kupata sera ya mwani na viungo. Je, kwenye *hot culture*. *Hot culture* sasa Mheshimiwa imeendelea kwa kiwango kikubwa sana nchini mwetu, leo Mheshimiwa fanya mpango uwende sokoni Mombasa pale asubuhi utizame mazao yetu yanavyomiminika, matunda yale na mboga mboga yaani huwezi kuamini kwamba wakulima wetu wanajitahidi sana. Mengi yale zamani yanatoka nje, yanakuja majahazi, yanakuja madau yanaleta leo yanatoka pale sio bamia, sio bilingani, sio tungule mpaka tumesafirisha juzi kwenda Bara, ukija kwenye matunda Mheshimiwa matikiti, ma avocado hivyo hivyo. Kenya wale ndio walivyoanza hivyo

wadogo wadogo tu wamezalisha kwa wingi wakatia kwenye maboksi leo madege yao yale ya Cargo yanatoka moja kwa moja yanatoka Nairobi mpaka London.

Mhe. Mwenyekiti, niliona kwa jicho langu mboga ya kisamvu inatoka Kinshasa unaikuta Brussels Ubelgiji, unaikuta sokoni pale nilishangaa kabisa, muhogo mkavu, viazi tona, viazi moja kwa moja *fresh* kabisa, sasa haya yote yanawezekana ni kujipanga tu Mheshimiwa.

Kwa hivyo, ningeomba sana kwenye upande huu wa matunda na mboga mboga tuiendeleze maeneo *potential* tunayo, matikiti leo watu wengi wameacha kazi nyengine wanalima matikiti na inawalipa.

Kwa hivyo, ningeomba sana Mheshimiwa miongozo upande huu unao na tuwasaidie *marketing* suala la watu wetu ni suala la kupata *marketing* wapi wauze wengi kuna *middle man* hapa kati kidogo wanawaangusha, wanaangusha bei wao sasa ndio wanafaidika.

Mhe. Mwenyekiti, nakwenda haraka haraka sina mambo mengi sana, nimalizie tu suala la ukaguzi wa mezani na vipimo kwenye ukurasa wa 28, kunazungumzwa pale, kuna jadweli pale namba 4 linazungumzia kwamba asilimia ya makusanyo mapato ya wizara kwa kipindi cha Julai 2017 hadi March 2018. *Column* inaonesha kifungu 1422014 asilimia ya makusanyo Julai – Machi kwa upande wa ukaguzi wa mezani na vipimo asilimia 29.6%. Sasa nikawa najiuliza hivyo mezani zote hizi zilizoko mjini na maduka madogo madogo wameweza kukaguwa kwa kiwango hiki kidogo kuna tatizo.

Bekari zote zile sisi tokea wadogo, Mhe. Waziri, anakumbuka vizuri mkate wa boflo ule tonge ile ilikuwa inapimwa na mezani pale ipo inapimwa tonge, ile tonge ndio inatiwa kwenye kibati ndio mkate, leo mezani zilizoko zile wameweka pambo tu wala hazifanyi kazi.

Kwa hiyo, tonge unakisia tu unatia kwenye kibati basi, mkata wa boflo ule zamani unauza pesa nne nafikiri leo sijui shilingi ngapi. Sasa hivi mtoto mdogo unaweza kumpa minne ile Mheshimiwa anaikata hivi hivi wala hajashiba. Sasa ningeomba sana ninapozungumzia *quality and standard* halafu tukizingatia hasa mkate wa boflo Mhe. Mwenyekiti ni chakula chetu kikubwa sana ukiacha mchele, sukari na unga. Unga ndio matumizi haya ya mkate wa boflo kwa hiyo ningeomba sana mheshimiwa hii *percentage* ya ukaguzi kwa mezani kidogo hairidhishi. Halafu hata ukienda kwenye ukurasa wa 54 jadweli namba 6 inaonesha mfano kwenye mabekari umeweza kukaguza bekari 16 tu.

Bekari 16 sijui mjini tu hizo bekari ziliopo sijui ngapi kama bekari 16 tumeweza kukagua ni kidogo mno kwa hiyo ningemuomba sana mheshimiwa akaze kamba yule lengo la kumlinda mlaji kama nilivyosema umuhimu wa mkate wa boflo nchini mwetu kwa kweli hiki ni kiwango kidogo sana, akaze kamba ili tumsaidie kumlinda mlaji.

Mheshimiwa sina mengi sana nimpongeze sana na nimalizie kwa kumpongeza yeye pamoja na kuendeleza sera za serikalini lakini hasa na *initiative* anazozichukua,

mheshimiwa tunamuona, ana muono mzuri na hii inaonyesha kweli ukomavu wake katika sekta hii na anavyoiongoza.

Mheshimiwa kila la kheri na mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja ahsante sana. *(Makofi)*

MICHANGO YA MAANDISHI

Mhe. Naibu Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo: Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nawapongeza wote viongozi pamoja na watendaji wote. Niende moja kwa moja kwenye mchango wa bajeti hii.

Suala la kwanza ni kuhusu kuimarisha ulinzi. Kwa kweli, bado uvuvi haramu unaendelea kwa kasi kwa baadhi ya wavuvi, hususan maeneo ya kisiwa cha Pemba kwa macho yangu nimeona pweza na ngisi waliovuliwa.

Jambo la pili kuhusu kufanya vipindi kwenye TV mbali mbali kuhusu matumizi ya mwani na faida zake. Kuhusu suala hili bado jamii ina mwamko mdogo wa matumizi ya mwani, naishauri wizara iwasaidie sana hawa wanaosarifu mwani na kuendelea kutoa vipindi kwa kuelimisha jamii mwani na faida zake za kiafya na matumizi ya bidhaa za mwani.

Suala la tatu kuhusu usimamizi wa bei za mchanga. Mhe. Mwenyekiti, naipongeza wizara kupitia Idara ya Misitu na Mali Zisizorejesheka kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa kuwakamata wachimbaji holela wa mchanga.

Kwa hivyo, naiomba idara hii kusimamia vyema bei elekezi ya mchanga iliyotolewa kuwa bado wananchi wanaumia sana kwa bei za mchanga.

Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Ahmada Yahya Abdulwakil: Mhe. Spika, naunga mkono bajeti hii asilimia mia moja.

(1) Sijaona kuhusu suala la kero za ndege aina ya kunguru.

(a) Je, kuna *activity* yoyote.
(b) Je, wizara imejipanga vipi kuhusu kuwaangamiza.

Mhe. Said Omar Said: Mhe. Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kulihuisha zao la karafuu na kuwajenga imani wamiliki wa mikarafuu kiasi ambacho kila mwananchi kwa hiari yake anailinda mikarafuu yake na anaihudumia vizuri sana.

Nichukuwe nafasi hii kumpongeza Mhe. Waziri kwa umahiri wake wa kuiongoza wizara hii na kupelekea kupatikana kwa maendeleo makubwa ya kiuchumi na kuzinyanyua hali za wanyonge waweze kumudu maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, ili wakulima na wakwezi wajengewe imani juu ya mafanikio ya zao la karafuu, serikali ijitahidi kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wa mizani za kupimia karafuu, ili zile ambazo zimeshachakaa ziondolewe na kuekwa mizani zilizo sahihi.

Sambamba na kufanya utafiti wa vituo vyote vya kununulia karafuu, ili kubaini ni vituo gani watu wanavikimbilia katika mauzo ya karafuu na vituo vinavyoepukwa katika mauzo ya karafuu, yaani vituo vyenye watu kidogo kidogo wanauliza karafuu zao hapo. Kwa kweli, wapo wanaovikwepa baadhi ya vituo kutokana na kukosekana kwa uadilifu wa maafisa wanaonunua karafuu ima warekebishwe na kupewa taaluma au kama ni mizani ziwekwe mpya.

Mhe. Naibu Spika, kuimarika kwa uchumi na kuzifanya hali za watu zilingane katika maisha kunatokana na kuwepo kwa uadilifu wa mambo 4. Jambo la kwanza kuuza, pili kununua, tatu kukopa na nne kulipa.

Mambo haya manne yataleta tija endapo patakuwepo chombo maalum cha kusimamia. Kutokana na hali hiyo naiomba serikali iweke chombo maalum cha kupitia kwa wafanyabiashara, ili kudhibiti kupanda kwa bei ya vyakula kiholela. Serikali imejitahidi kuwasaidia wananchi kwa kutoa unafuu wa kodi, lakini hata hivyo wafanyabiashara wanaitaka nafasi hii kwa kujitafutia maslahi wao wenyewe tu bado hawajawazingatia walaji kwa jicho la huruma.

Nikiendelea na mchango wangu naomba nizungumzie kuhusu suala la viwanda ni miongoni mwa sekta inayoleta ufanisi wa haraka kwa maendeleo ya wananchi wetu. Kwa mfano, Pemba kunapatikana sana embe hususan katika maeneo ya Kiuyu Minungwini kiasi ambacho kama serikali itaamua kuweka kiwanda cha kusindika basi vijana wengi watafaidika kwa kupata ajira. Lakini pia serikali itaongeza pato lake.

Kwa hivyo, ni vyema serikali kuweka embe maalum kwa shughuli za viwanda kama hivi. Baada ya hayo naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja ahsante.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, naomba sana kuwe na *center* ya maonesho yetu iwe ya kudumu ambayo tutapata wafanyabishara wengi kutoka ndani na nje ya nchi yetu na tutapata kufunga nao mkataba. Kwa kweli, wajasiriamali wetu wataweza kupata manufaa makubwa, kama vile eneo lile la *SUZA* kwenye eneo la Tunguu ambalo alilitenga Mhe. Rais Mstaafu wa Zanzibar Dkt. Salmin Amour Juma na kama lingelikuwa lipo lingesaidia sana.
Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri asichoke apigania sana apate eneo la maonesho ya kudumu. Nakutakia kila la kheri katika azma kubwa waliojipangia katika majukumu waliyopewa. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naishukuru sana Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuiwezesha Wizara hii ya Biashara na Viwanda kuweza kuwakusanya wafanyabiashara wa Zanzibar kujua kwamba wanayo wizara yao ambayo inaratibu mwenendo mzima wa mipango ya biashara zinazoingia na zinazotoka na jinsi wananchi wanavyofaidika na biashara hizo. Lakini pia kufufua viwanda kibiashara, yaani uchumi wa viwanda.

Nampongeza sana Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda Balozi Amina Salum Ali kwa kuwasilisha bajeti hii kwa ufasaha na ujasiri mkubwa, kwa kweli inatosha sana na bajeti imekidhi mahitaji yake. Nampongeza Naibu Waziri pia watendaji na wafanyakazi wote kwa kushirikiana.

Suala la wafanyabiashara wetu Zanzibar kutozwa katika bandari ya Dar-es-Salaam na Zanzibar kwa biashara hiyo hiyo wanailalamikia sana vyema likatizamwa kwa upana zaidi.
Pia kuhusu suala la wenzetu Tanzania Bara kutothamini baadhi ya biashara zetu na kutetea kuziingiza katika soko lao. Kwa mfano tatizo la sukari limeleta gumzo kubwa kwetu Zanzibar ni vyema sasa wizara au serikali kukaa pamoja na wenzetu Bara, ili kuzungumza na kuweka sawa suala hili na kuepusha kuharibu Muungano na udugu wetu wa muda mrefu.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wanawake na Watoto: Mhe. Mwenyekiti kwa heshima yako napenda kuchukuwa nafasi hii ya kumpongeza Mhe. Rais wetu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kumuamini Mhe. Balozi Amina Salum Ali kuwa ni Waziri wa Biashara na Viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, wakati serikali inaendelea kujipanga namna katika kuviandaa viwanda. Kwa lengo la viwanda viweze kuimarika ni kuwaandaa wajasiriamali kutoka katika maeneo tafauti Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Habari, Utalii na Michezo na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto. Wakati wizara hizo zinajitahidi kuwachangisha wajasiriamali katika sekta mbali mbali, ili watoe *product* bora.

Mhe. Mwenyekiti kitendo cha kuanzisha vyombo kama *SMIDA* unadhani kuwa nia ipo ya kuboresha mazao yet,u ili tupate soko la uhakika zao la chumvi na kadhalika.

Suala zima la ushiriki nchi za nje zinawapa changamoto wajasiriamali wadogo wadogo, hujifunza kutoka nchi za jirani na inaonekana wazi kuwa wakisaidiwa katika mashindano ya bidhaa zao zinaposhindanishwa Zanzibar wanashinda. Hawajawahi kutoka nje ya duara la chini ya tatu.
Mhe. Mwenyekiti, wizara yangu itaendelea kutoa kila aina ya mashirikiano ili viwanda vilivyopo na vitakavyokuja kwa manufaa ya nchi yetu. Kwa hiyo, nawashawishi au nawashauri Waheshimiwa Wajumbe wenzangu kuunga mkono bajeti hii, ili atekeleze hali aliyokusudia kwa manufaa ya nchi yetu.

Aidha napenda kusema naunga mkono asilimia mia moja hoja hii. Ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe nashukuru sana kwa michango ambayo kuwa tumeweza kumsaidia Mhe. Waziri na huyu alikuwa ni mchangiaji wetu wa mwisho sasa naomuomba nimwite Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda ili na yeye atowe mchango wake kwa njia ya kujibu baadhi ya hoja.

Mhe. Naibu Waziri karibu sana.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba kuchukua fursa hii ya kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na uhai kwa sisi sote leo hii kuwa hapa kukutana katika kupitisha bajeti hii muhimu ya uchumi wa nchi yetu, Bajeti ya Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar. Lakini pili nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuniteuwa mimi kuwa Naibu Waziri wa Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, tatu nimshukuru Mhe. Waziri wangu Balozi Amina Salum Ali waziri mzoefu aliyewahi kufanya kazi katika serikali zote mbili Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar *in English* tunasema the *longest served minister,* lakini mheshimiwa nichukuwe fursa hii kukupongeza wewe na Baraza lako Tukufu kwa leo kusoma bajeti yetu na kuonesha kutokutupa vikwazo vya aina yoyote ile na ninaona na najua dhahiri kwamba bajeti yetu leo itapita hasa kwa michango ya wajumbe wengi waliosema kwa heshima ya Mhe. Waziri, kwa heshima ya Naibu Waziri mpya mtoto wa wakwezi na wakulima leo bajeti yetu itavunja rekodi kwa kupita bila ya kupigwa mabuti.

Mhe. Mwenyekiti, kadhalika naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wa Jimbo la Welezo kwa kunichagua mimi kuwa mwakilishi na leo kuwa Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda wizara ambayo ina leta na kusimamia uchumi na maendeo ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, unapozungumza Wizara ya Biashara naomba leo kila mtu atambuwe kwamba Wizara ya Biashara ndio wizara mama inayoleta uchumi wa nchi hii, inayoleta maendeleo ya nchi hii kwa sababu ulimwengu unakoelekea kote unahamasisha biashara. Unapozungumzia kilimo unazungumzia kilimo cha biashara, unapozungumzia utalii unazungumzia utalii wa biashara, unapozungumzia uvuvi unazungumzia uvuvi wa biashara. Unapozungumzia elimu unazungumzia elimu kwa biashara, unapozungumzia michezo, unazungumzia michezo kwa biashara, unajifunza kwamba biashara ndio kila kitu katika maendeleo ya nchi, katika maendeleo hata ya familia, katika maendeleo hata ya mtu mmoja mmoja biashara ndio sahihi ya maendeleo ya taasisi na nchi kwa jumla.

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la Wizara ya Biashara ni kuweka mazingira bora wezeshi ili Zanzibar iweze kufanya biashara ndani ya Zanzibar na nje ya Zanzibar lakini kadhalika biashara ina jukumu la kuhamasisha na kutekeleza Sera ya Viwanda kuifanya Zanzibar iweze kuwa Zanzibar za Viwanda. Mhe. Mwenyekiti, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar

tumedhamiria na uwezo tunao na sababu tunayo ya kuifanya Zanzibar kuwa Zanzibar ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, nitawarudisha kunako historia kidogo watu waangalie historia Zanzibar imekuwa na viwanda kabla ya mapinduzi, Zanzibar imekuwa na viwanda baada ya mapinduzi sasa tunataka kurudisha hadhi na heba ya Zanzibar ya viwanda kama tulivyokuwa nayo zamani.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya mapinduzi Zanzibar ilifungua viwanda vingi na vyote vilifanya kazi na watu walipata ajira walikuwa wengi, mapato mengi ya serikali yalipatikana kutokana na viwanda hivyo na Zanzibar ya viwanda Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar na ukiangalia hii sera imo katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwamba tunataka Tanzania ya viwanda, tunataka Zanzibar ya viwanda, naomba sote leo tuipitishe bajeti hii ili tukajenge viwanda vyetu, ili tukaweke mazingira wezeshi, mazingira bora ya Zanzibar tunayoitaka kuwa Zanzibabar ya viwanda.

Mhe. Mwenyekiti, kama tulivyosema wizara inaongeza waziri mzoefu aliyefanya kazi katika serikali zote mbili na leo wote tumemsifu na mimi mtoto wa mkwezi na mkulima nipo namsaidia ananifundisha kazi, ananielewesha jinsi ya kufanya kazi namshukuru, lakini mheshimiwa sasa naanza kujibu baadhi ya hoja zilizoletwa na Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nitaanza na mfumuko wa bei hasa ukizingatia mwezi mtukufu wa ramadhani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imekuwa na utaratibu wa kutoa msamaha kwa baadhi ya vyakula kama mchele, sukari, unga wa ngano na tende. Lakini wajumbe wengi waliochangia wanofika wajumbe kumi na tatu wote wamezungumzia kwamba msamaha wa kodi haufaidishi wananchi kwa sababu wanalalamika wanasema wafanya biashara bei hazipungui hii ndio hoja mheshimiwa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka niwambie Waheshimiwa Wajumbe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar jinsi gani imekuwa inakuwa inachukuwa jitihada kila uchao wa kuhakikisha inamlinda mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, kuna sheria mbili kuna sheria hii Sheria ya Ushindani Halali na Kumlinda Mtumiaji Sheria namba 5 ya mwaka 2018 inazungumzia jinsi gani itamlinda mtumiaji, lakini kuna Sheria ya Biashara ambayo pia imezungumzia jinsi inavyoweza kumlinda mtumiaji.

Mhe. Mwenyekiti, naomba wajumbe watambue jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar dhidi ya kumlinda mlaji, lakini pia watambue jukumu la Wizara ya Biashara ni kuweka mazingira wezeshi kuwalea wafanya biashara waweze kufanya biashara.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara ina mikono miwili mmoja mkono wa kulea, mmoja mkono wa kuhukumu kwa sababu sheria hizi zote tunazo sisi Wizara ya Biashara.

Mhe. Mwenyekiti, tarehe 15/5/2018 Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar alifanya *Press Conference* alizungumza na Waandishi wa Habari, tarehe 10/5/2018 Wizara ya Biashara kushirikiana na Wizara ya Fedha ilitowa msamaha wa kodi kwa baadhi ya bidhaa kama mchele, sukari, unga wa ngano na tende ili wananchi wake wapate unafuu katika bidhaaa hizo hasa ukizingatia bidhaa hizo zitatumika kwa wingi wakati wa mwezi huu mtukufu wa ramadhani, lakini malalamiko yaliokuwepo kwamba bidhaa hizo wafanya biashara hawajapunguza bei, bei ziko pale pale.

Mhe. Mwenyekiti, Waziri wa Biashara alitoa *Press Conference* alisema naomba kunukuu.

Mhe. Mwenyekiti, Waziri wa Biashara alisema kama kutatokea mtu au mfanyabiashara mwenye kuingiza yule *importer*, muuzaji wa jumla au yule *wholesaler* au muuzaji wa rejareja anakwenda kinyume na maagizo ya serikali narudia anakwenda kinyume na maagizo ya serikali baada ya kutolewa msamaha tulitoa bei elekezi. Bei elekezi zilitolewa katika *Press Conference* ya tarehe 15/5/2018 na imetoa bei elekezi za bidhaa ya mchele, sukari na unga na tukasema tunaomba ushirikiano Mhe. Waziri kasema tunaomba ushirikiano wa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Masheha kama kuna mtu anakwenda kinyume na bei elekezi hizo aripoti kwa mujibu wa taratibu.

Mhe. Mwenyekiti, sheria tunazo Wizara ya Biashara ndio yenye jukumu ya kumlinda na kumuwekea mazingira sahihi mfanyabiashara lakini pia ina jukumu la kumlinda mtumiaji, tuna mikono miwili moja tunalea, mmoja tuna hukumu.

Mhe. Mwenyekiti, mpaka leo hakuna mtu ameripoti mimi naomba kusema na Baraza hili bado nitaendelea kufanya kazi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Rais ameniamini, lakini kama kuna mtu atakwenda kinyume na sheria basi Wizara ya Biashara na Mhe. Waziri kushirikiana na mimi na watendaji wetu tuko tayari kumsulubu, tuko tayari kwenda naye kwa mujibu wa sheria yaani tuko tayari kumuhukumu kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi. Kwa sababu nchi ndio inayoweka sheria na jinsi gani serikali tumeweza kusema inavyowapenda na kuwaenzi wananchi wetu kwa kuwaekea bei elekezi katika mwezi huu mtukufu wa ramadhani.

Mhe. Mwenyekiti, hatuko tayari Wizara ya Biashara kumuona mfanya biashara yoyote anakwenda kinyume na bei elekezi tulizotoa hasa ukizingatia serikali imetoa msamaha kwa baadhi ya bidhaa. Lakini wafanyabiashara tunafahamu kweli wapo baadhi yao si waaminifu wanakwenda kinyume na matamko haya.

Mhe. Mwenyekiti, kupitia leo Mhe. Waziri ametoa *Press Conference* na mimi naomba kusema kama kuna mtu aripoti Masheha tushirikiane, Wakuu wa Wilaya tushirikiane, Wakuu wa Mikoa tushirikiane aturipotie. Kama tulivyosema tuna mikono miwili moja wa kulea, moja wa kumhukumu, tunamchukulia hatua za kisheria mtu yeyote yule ambaye anakwenda kinyume na matakwa ya serikali haendani na sheria, sheria tulizotunga wenyewe lakini yeye hataki kuzifuata kama mwananchi awe mfanyabiashara, awe mwananchi, awe mtu yoyote.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nilihojiwa na waandishi wa habari na nilisema hivi kama mwananchi amekwenda kunako duka na Mzee Ali au Mzee Juma mtaani huko akakuta bei haziko sawa kama tulivyotangaza aende kwa Sheha, akifika kwa Sheha amwambie duka la Mzee Ali sukari imesema iuzwe bei kadhaa lakini Mzee Ali anauza bei hii, ende kwa Sheha akaripoti, Sheha atakwenda kwa Mkuu wa Wilaya, Mkuu wa Wilaya atafika kwetu, sisi tuko kwenye mamlaka ya kumhukumu na sisi ndio twenye mamlaka ya kumlea kama tumeona sheria kaikiuka taratibu zipo sheria tutaichukua.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia pale Wizara aya Biashara tuna utaratibu wa maaofisa wetu kila siku ya mungu wako madukani kuangalia mfumo wa bei. Mhe. Mwenyekiti, kama unavyojua wako wafanyabiashara waliokuwa wako wazuri na wako waliokuwa si waaminifu. Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara inataendelea kufanya jukukumu lake la kuwalea wafanyabiashara ili Zanzibar biashara iweze kufanyika lakini pia itaendelea na jukumu lake la kumlinda mtumiaji ili asije akanyanyaswa na mfanyabiashara kwa kuongezewa bei bila ya sababu ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua mfuko wa bei kuongezeka na kupungua ni jambo la kawaida lakini lazima kuwe na msingi wa kuongeza bei zile. Kwa sasa bei za vyakula elekezi ulizotoa hakuna msingi wa kuengezwa kwa sababu tumetoa bei elekezi, tumetoa msamaha wa kodi kwa wananchi wetu kwa wafanyabiashara lazima wafanyabiashara lazima wananchi wetu wauziwe bidhaa kama tulivyoelekeza kupitia *Press Conference* aliyotoa Mhe. Waziri tarehe 15/5/2018.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hoja hii imezunguzwa na wajumbe karibu kumi na sita ndio hoja iliyokuwa kubwa naomba kusema tushirikiane katika kumleta mtu yoyote yule anaekwenda kinyume na misamaha ya kodi kama tulivyoitoa. Wizara ya Biashara narudia kusema tena tuko tayari na tutamchukulia mtu hatua kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hayo wajumbe wengi wamelalamikia maghala. Maghala, maduka na wamesema wengi sana kwamba Wizara ya Biashara ndio wizara tajiri hapo zamani ilikuwa na maghala mengi, ilikuwa na maduka mengi hata Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) akauliza maghala yako mangapi, maduka yako mangapi.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu kwamba kuna maghala kumi na mbili ambayo yamekodishwa na kuna maduka manne ambayo yamekodishwa. Maduka haya na maghala haya yamekodishwa kwa mujibu wa taratibu ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mujibu wa sheria na taratibu kama zilivyoelekeza kwa mujibu wa sheria katika kukodisha au kutaka kununua mali za serikali, utaratibu huo upo na utaratibu huo umefuatwa na tumekodishwa kwa wastani wa laki moja na nusu mpaka laki sita kwa mwezi lakini kwa kufuata utaratibu na sheria zilizowekwa kwa mujibu wa kukodi au kununua kwa mali za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) na wengine walionesha wasiwasi wao kwamba kuna watu wamekodishwa kwa bei iliyokuwa si ya halali bei ya chini lakini kuna watu wamekodishwa waliokuwa si wazalendo wasiwasi ndio ulokuja watu wanne walikuja na wasiwasi huo.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumwambia Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata) na wengine wasiwasi huo sasa na mimi nimeuchukua umekuwa wangu mimi Naibu Waziri kwamba na mimi nimepata wasiwasi nitalifuatalia kujua hao waliokodishwa wa nani wamekodishwa kwa bei halali, nitaifanya kazi kihaki *llahi taala* kwa sababu ya kulinda maslahi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tukifanya hivyo ndio tunalinda Mapinduzi Matukufu ya Januari 1964.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwambia wajumbe wote kuhusu kukiodishwa kwa maduka hayo, kuhusu bei na waliokodishwa kama wazalendo au si wazalendo hili suala nalichukua na nitalifanyia kazi *kihaki llahi* taala kuhakikisha serikali yetu inaendelea kama tulivyokusudia kwa kuyalinda mapinduzi katika kuwafanyia maendeleo wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hoja ya pili ya tatu ilikuwa hoja ya viwanda wameuliza wajumbe wengi wajumbe kumi na saba wameulizia suala la viwanda na wasiwasi nambari moja ulikuwa Zanzibar ilikuwa na viwanda kabla lakini vimekufa kuna mjumbe akauliza kwa nini vilikufa.

Mhe. Mwenyekiti, unaposoma vitabu, unaposoma *article* mbali mbali zilizoandikwa na wasomi mbali mbali wa Zanzibar na dunia nzima wanasema hivi wanasema naomba ku-*cote* naomba kunukuu.

> "Vwanda vingi vya nchi ya afrika kama Zanzibar vimekufa kutoka na kuwa malighafi *raw material* zilikuwa zinaagizwa kutoka nje".

Ukifanya mfano viwanda vidogo vidogo tulikuwa tuna viwanda vya masufuria, viwanda mbali mbali lakini ukiangalia malighafi zote zilikuwa zinaagizwa kutoka nje.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya tafiti hizo kuziangalia, kuzisoma na namshukuru Mhe. Waziri wangu nilipokwenda pale kama Naibu Waziri alinipa matabu mengi akanambia mheshimiwa kasome utafaidi sana. Sasa nimekuwa siku hizi silali kwa kusoma vitabu, unajifunza kwamba vimekufa kwa sababu ya kuangiza mali ghafi. Sasa naomba kuwatoa wasiwasi Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza laki Tukufu kwamba Sera ya Viwanda kama ilivyoelekeza katika Ilani ya CCM tunaitaka Tanzania ya viwanda, tunaitaka Zanzibar ya viwanda sisi Wizara ya Biashara ndio twenye jukumu tumeipokea na tumeanza kwa kasi kubwa katika kuitekeleza na kuifanyia kazi. Sote mashahidi karibuni tu Mhe. Rais hapa amemteuwa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ha *SMIDA* ambayo itashughulikia masuala ya viwanda vidogo vidogo vya kati kwa Zanzibar.

Lakini kadhalika mheshimiwa ni kweli tunaitaka Zanzibar ya viwanda tumejipanga mheshimiwa ukiangalia faida ya viwanda dunia nzima ni kitu kinachotoa ajira na kinachotoa kodi ya nchi kwa maendeleo ya nchi. Nchi zetu za Ulaya ziliendea baada ya kuleta mapinduzi ya viwanda, mapinduzi ya viwanda nchi kama Uingereza, Marekani, Canada ilileta ajira, ilileta kodi ndio zilizofanya iendelee. Lakini tumuone Mchina jinsi gani anaendelea baada ya kutangaza na yeye mapinduzi ya viwanda, Zanzibar inanunua

vitu vingi kutoka China dunia nzima inanunua vitu kutoka China. China ndio imekuwa the *world workshop* walioona wazungu kwamba vitu vyote vya dunia *almost* asilimia sitini vinazalishwa China na China sasa inaendelea karibuni China itakuwa ni nchi moja kati ya nchi zilizoendelea yote hayo ni kutokana na viwanda walivyonavyo.

Mhe. Mwenyekiti, na Zanzibar ya viwanda tunaweza lakini tuzingatie kwamba tutahakikisha baadhi ya mambo mengi yanayokwenda kwa *raw material* zinatoka. Mhe. Mussa ameeleza tuanzo embe, ameeleza tunazo tungule, kuna mabungo vyote hivyo tunaweza tukavifanya ni bidhaa zinazozalisha watu wengine wakawa wanazalisha wengine wana *process* kwa njia ya viwanda tunauza ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, tutapata ajira, tutapata kodi kwa nchi lakini naomba kusema watu wengi wameongea kuhusu Kiwanda cha Sukari Mahonda. Mhe. Mwenyekiti, naomba kusema Kiwanda cha Sukari Mahonda ni kiwanda chenye historia ya Zanzibar kinakwenda sambamba kabisa kabisa na mapinduzi na matakwa ya Mapinduzi yetu Matukufu.

Mhe. Mwenyekiti, wamekilalamikia kwamba naomba kusema tunafanya kila iwezekanavyo kuhakikisha tunakilinda kiwanda chetu cha sukari Mahonda kwa sababu kinatoa ajira. Katika kulinda viwanda nchi za wenzetu duniani wana taratibu nyingi za kufanya mfano nchi ya Ufaransa huwezi kuingiza maziwa yanayotoka Denmark na Denmark ndio inayotoa maziwa mengi duniani lakini huwezi kuyaingiza Ufaransa kwa nini kwa sababau wameengeza *tarrif* kubwa kwa kulinda viwanda vyao vya ndani. Mhe. Mwenyekiti, na sisi kwa sababu tuna sera ya viwanda kwa hivyo kama una sera ya viwanda ni lazima ulinde viwanda vya ndani.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Biashara kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa sekta hizo tutahakikisha tunalinda viwanda vya ndani kwa kufanya mambo mbali mbali yanayo kwenda na wakati, yanayokwenda na kilimwengu ili na sisi viwanda vyetu viweze kuzalisha tuweze kununua, waweze kuuza ndani nchi na nje ya nchi. Mhe. Mwenyekiti, jukumu la viwanda kwa Zanzibar liko Wizara ya Biashara Mhe. Waziri wangu mimi pomoja na watendaji tumelipokea na tunalifanyia kazi kwa kasi.

Mhe. Mwenyekiti, katika masuala ya viwanda wako waliozungumzia kuhusu mwani. Ni kweli mwani umetoa ajira karibu ya watu 26,000 Zanzibar, wengi wao ni wanawake walioajiriwa katika masuala ya mwani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, wakati nachaguliwa kuwa Naibu Waziri jambo la mwanzo nilimsikia Mhe. Waziri wangu akinambia, "Mhe. Naibu Waziri umechaguliwa hapa lakini hapa tuna mambo mawili kwa matatu, la kwanza tuna *ZSTC* ndio tinga tinga la wizara hii, pili tuna mwani na la tatu Mheshimiwa hapa tuna dagaa".

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuliambia Baraza lako tukufu tangu siku hiyo niliyoambiwa nimetembelea Pemba, Unguja baadhi ya maeneo ya wakulima wa mwani, nimeangalia bei zao, nimezungumza na watu mbali mbali ni kweli bei yao kidogo iko chini, lakini jitihada za wizara tunahakikisha kwamba kwa kushirikiana na *WIPO,* tumeshawaita

wameshatuletea vitabu vyao vya *research* zilizofanywa kuhakikisha Mwenyezi Mungu akitujaalia *Inshaallah* tuwe na kiwanda ambacho kita-*process* mwani Zanzibar. Faida yake nini? Faida yake wako wengine watapata ajira katika kile kiwanda lakini ile bei ya mwani Zanzibar itaongezeka, ili ule mwani uuzwe *processed* mwani kwa nchi nyengine za nje na mwengine tuweze kuutumia hapa Zanzibar. Naomba kuwaambia wananchi kwamba, *issue* ya mwani tunaishughulikia ipasavyo na kuhakikisha kuona wakulima wetu wa mwani wanafaidika na zao hili, hasa ukizingatia kwamba imeajiri kinamama wengi na Rais wa Ghana alisema: "Ukimuwezesha mwanamke umeiwezesha *whole family*". Tuko tayari na tunafanya kazi hiyo kwa umahiri na umakini mkubwa kuhakikisha tunatoka katika sekta hiyo ya mwani na wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo kuna hoja kubwa imezuka ya usumbufu bandarini pale Dar es Salaam baadhi ya watu wanapokwenda na bidhaa zao. Mheshimiwa tarehe 22 mwezi wa Machi Wizara ya Biashara na Viwanda Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Biashara ya Tanzania Bara tulikaa kikao cha pamoja Tanzania kuangalia changamoto zinazoikabili moja ilikuwa ni hii.

Mhe. Mwenyekiti, nakumbuka Mhe. Waziri alisema kwamba usumbufu huu tumeufanyia kazi na tumetoa baadhi ya maelekezo, tumetoa *hotline* mbali mbali za kuhakikisha kwamba mambo hayo tunayafanyia kazi.

Tumesema pia kuhusu suala la maji, bidhaa mbali mbali Mhe. Mohamed Said Mohamed kwamba maji yanayozalishwa Zanzibar hayendi Bara, tukasema kama yana viwango vyote vinavyotakiwa na taasisi za viwango za Zanzibar na taasisi za viwango za Tanzania kwamba suala hilo halina usumbufu na kwa mtu yeyote atakayeweza kuleta usumbufu kwa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Bara kama zimefuata *procedure* zote atupigie simu. Namba za simu zilitolewa naomba kusema kwamba zipo kama kuna mtu atapata usumbufu na amefuata *procedure* zote za kisheria kuhusu bidhaa yake inayozalishwa Zanzibar kwenda Bara kwa mujibu wa kikao cha tarehe 22 kwamba atupigie simu, *hotline* zimetoka tutakwenda naye sambamba mtu huyo kwa sababu atakuwa ni yule adui wa Muungano wetu. Muungano wetu huu umetutoa mbali tupo pazuri na tutaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ukitaka usitake kuna nchi nyingi duniani mfano Gambia na Senegal walitaka kuungana, waliungana wakaita Senegambia lakini hawakuweza, lakini leo tuna miaka 54 ya Muungano wa Tanzania, Tanganyika na Zanzibar tuna kila sababu ya kuulinda, kuudumisha na kuuimarisha Muungano huu. Sasa kama kuna mtu hafuati taratibu Mheshimiwa anausumbua Muungano wetu, anaongeza kero katika Muungano wetu mimi mtoto wa mkwezi na mkulima, Mhe. Waziri wangu na watendaji wa wizara yetu tuko tayari mtu huyo kwenda nae sambamba kwa mujibu wa taratibu na sheria za nchi.

Mhe. Mwenyekiti, kweli unapofika Dar es Salaam kuna wajanja umekwenda na televisheni wanaweza kukutizama sura yako wakataka kukutoza pesa, *sometime* kuna mambo hata si ya kumtoza mtu pesa lakini wanatizama sura yako. Kuna wengine wajanja tu, lakini sio taratibu Mheshimiwa. Kwa maana hiyo, naomba kusema tusichoke kuripoti

mambo kama hayo yanapotokea. Wizara ya Biashara tupo na tuko tayari kuwatumikia wananchi kwa mujibu wa sheria kama sheria zinavyotutaka.

Mhe. Mwenyekiti, nikiacha hayo kuna suala la takwimu lilizungumzwa ambalo liko ukurasa wa nane wa kitabu chetu. Ukiangalia anasema hasa Mhe. Omar Seif Abeid, alisema takwimu za bidhaa zinazoingizwa Zanzibar zilizorikodiwa humu sio sahihi. Kwa sababu anasema kuna bidhaa nyingi zinaingia kwa mujibu wa pesa iliyorikodiwa humu ukurasa wa nane sio sahihi, kwamba ile taasisi ya takwimu hasa bandarini kitengo kile hakiko vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini naomba kumwambia Mheshimiwa na wajumbe wote kwamba hizi ndio takwimu sahihi ambazo tumezileta na tumezipata kutoka taasisi mbali mbali za serikali. Naomba azipokee hizi tulizozileta katika kitabu chetu kitukufu cha Wizara ya Biashara na Viwanda kitabu ambacho kimesifiwa na watu wengi na jinsi walivyomsifu Mhe. Waziri alivyoweza ku-*present* hotuba yake. Lakini naomba kusema, kama kuna tatizo katika takwimu hizi wasiwasi wake nimeuchukua na nitaufanyia kazi. Kwa sababu Mhe. Panya Ali Abdalla mama yangu alisema takwimu ni kitu muhimu katika maendeleo ya nchi, ukiwa na takwimu *wrong* ina maana mipango yako nayo itakwenda *wrong*. Sasa kwa sababu ana wasiwasi na wasiwasi bibi yangu alinambia ndio akili kwa maana na mimi nauchukua ule wasiwasi nitaufanyia kazi, kufanya kitu kwa Kizungu kinaitwa *more verification* katika kujua tunakwendaje. Mhe. Mwenyekiti, hizi ni takwimu sahihi lakini wasiwasi ndio akili na tutasaidia katika kuzifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo Mhe. Simai Mohamed Said alizungumzia kuhusu bidhaa zinazotoka, kwa nini aliuliza yeye Mhe. Simai na wengine...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa muda wako uliobakia kama dakika tano tu kwa hivyo, ujipange muda uutumie vizuri.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Sawa ahsante. Mhe. Simai Mohamed alizungumzia kuhusu bidhaa kama gari na mambo mengine zinazokuja kutoka Dubai, akauliza kwa nini hii *ZBS* haifanyi ikaweka kule kule bandarini? Mhe. Mwenyekiti, kwanza hatuna eneo kule bandarini, lakini kwa mujibu wa sheria za nchi Zanzibar na dunia nzima gari yoyote haiwezi kukaa barabarani bila ya kupata stakabadhi zinazotakiwa. Sheria hiyo ipo kwa maana hiyo gari kama imekuja kutoka Dubai haiwezi kuingia barabarani kama haina *road tax* na *insurance* lazima ikafuate taratibu na taratibu hizo zipo, dunia nzima na hapa Zanzibar zipo, huwezi kuitia gari barabarani kama hujafuata taratibu zipo panahitajika *international road* zipo *guarantee* au unakwenda polisi unasema gari yangu hii wanakupa maelekezo unayafanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo katika mchango wangu nitakwenda *ZSTC*. Wajumbe wengi wa Baraza lako tukufu walielezea kuhusu *ZSTC* Shirika letu ambalo lina jukumu la kununua na kuuza karafuu Zanzibar.

Kwanza naomba kuwapongeza wajumbe wote kwa kuonesha mapenzi ya nchi dhidi ya kushirikiana na sisi Wizara ya Biashara katika kulienzi na kulitunza na kuliendeleza zao kuu la karafuu.

Mhe. Mwenyekiti, dakika zangu zimebakia tatu.....

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae kidogo, sasa nitampisha Mhe. Naibu Spika, ili aweze kuendelea na kika hiki. Mhe. Naibu Spika, karibu sana.

(Hapa Mhe. Naibu Spika alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa Naibu waziri endelea.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, naomba nikushukuru. Naendelea kwa kujibu hoja za Wajumbe mbali mbali kupitia Shirika la *ZSTC*. Mhe. Naibu Spika, napenda kuwapongeza Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwa kulipenda na kulithamini zao letu la karafuu ambalo linaendeshwa na Shirika letu la *ZSTC*.

Shirika hili lina jukumu la kununua na kuuza karafuu. Miongoni mwa majukumu yake wasiwasi wa wajumbe wengi ulikuwa katika vipimo, mikopo, katika mashine ya kukaushia karafuu, halafu pia barabara ya Mgelema ambayo ilizungumzwa na mheshimiwa huyo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa ufafanuzi katika hoja hizo kwamba, kuhusu vipimo *ZSTC* naomba kusema tunanunua karafuu lakini hatununui kwa pishi tunanunua kwa kutumia kilo. Kwa maana hiyo, mwananchi anapokwenda kuuza karafuu kama kazipima kwa pishi ajue kwamba ikifika *ZSTC* wao hawanunui kwa pishi wananunua kwa kilo. Ni kweli kutokana na pishi za leo na za zamani haziko sawa, pishi ya shaba ya kizamani na pishi ya leo unaweza ukazipima karafuu nyumbani pishi kumi lakini ukifika nazo *ZSTC* zikawa pishi tisa na nusu labda hujui kimetokezea nini, lakini naomba kusema *ZSTC* hatununui karafuu kwa pishi tunanunua kwa kilo na nimekwenda mwenyewe nimeona karafuu zinapimwa pale na mwananchi anaitwa amehakikisha anapewa cheti cha ununuzi ndipo anakwenda kulipa.

Nikitoka hapo niende kwenye mikopo. Mikopo haitoshi na haitolewi kwa wakati, naomba kusema kweli naomba watupongeze Wizara ya Biashara Shirika la *ZSTC* kwamba angalau tunatoa mikopo kwa wananchi wetu wanaoshughulikia zao la karafuu. Ni kweli haitoshi tutajitahidi kadiri inavyowezekana tuweze kupata kingi na wao waweze kuwapa kingi. Kuhusu kutolewa kwa wakati tutajitahidi tuweze kutoa kwa wakati, lakini naomba watupongeze kwamba angalau tunaweza kupata mikopo na tunawapa fedha ili kuweza kunusuru zao letu kuu la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, wajumbe wengi walionesha nia ya kwamba karafuu zao zinaharibika wakati wa kipindi cha mvua kwa sababu ya ukosefu wa mashine ya kukaushia. Mheshimiwa hili tumelipokea na naomba kuliambia Baraza lako tukufu hili suala

tunalichukua na tutalifanyia kazi, kwa sababu zao la karafuu ni zao letu kuu tunalipenda sote na tumejidhatiti katika kulienzi na kuliendeleza. Hii mashine ya kukaushia karafuu Mhe. Mussa Ali Mussa na wajumbe wote tunalichukua na tutalifanyia kazi. Mhe. Mussa Ali Mussa alisema twende China tukatafute mashine hii. Mimi naomba kumwambia hili suala tutalichukua tutalifanyia kazi kikamilifu.

Mhe. Naibu Spika, pia walisema kuna baadhi ya mashamba yako Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi walipendekeza Waheshimiwa Wajumbe mashamba yale yahamie *ZSTC* kwa sababu shirika hilo ndio lenye jukumu la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, hili ni wazo na ni pendekezo sisi tumelichukua tutajaribu kufuata utaratibu kama itawezekana basi sisi tuko tayari kuyachukua kwa sababu sisi ndio wenye dhamana ya karafuu hapa Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Mussa pia alisema kwamba barabara ya Mgelema ambayo *ZSTC* Wizara ya Biashara tayari iliitengeneza, lakini amesema imeharibika. Naomba kumwambia nalo tumelichukua tutalifanyia kazi mimi mwenyewe nikienda Pemba *this time* nitakwenda kuitembelea barabara ya Mgelema ili tuweze kuona na kuhakikisha kwamba watu wetu wa Mgelema wanafanya kazi katika kulinusuru na kulienzi zao la karafuu, wanafanya kazi kwa vizuri ili zao hili liweze kuendelea na kumea. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naamini wazi hasa ukizingatia wizara hii inaongozwa na Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali mzoefu, mama yetu, sitotegemea buti hapa leo Ramadhani ya 14 sitoona buti leo hapa. Lakini kadhalika ukiona kwamba jinsi gani Wizara ya Biashara na Viwanda imeweza kusimamia majukumu yake na tunaahidi tutaendelea kuyasimamia.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo machache naomba kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Mheshimiwa ahsante nakushukuru.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwanza kabisa kuwashukuru Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu waliochangia na waliokuwa hawakuchangia na waliochangia kwa maandishi. Wote michango yao imetupa moyo na faraja kubwa sana wizara yetu nawashukuruni sana.

Mhe. Naibu Spika, katika orodha yangu waliochangia jumla ni watu 21, waliochangia kwa maandishi na waliochangia kwa kuhutubia. Kwanza naomba nimtaje Mhe. Mwenyekiti.

1. Mhe. Mussa Ali Mussa
2. Mhe. Ali Suleiman Ali
3. Mhe. Omar Seif Abeid
4. Mhe. Suleiman Makame Ali
5. Mhe. Rashid Makame Shamsi
6. Mhe. Ali Khamis Bakari
7. Mhe. Jaku Hashim Ayoub

8. Mhe. Simai Mohamed Said
9. Mhe. Nassor Salim Ali
10. Mhe. Panya Ali Abdalla
11. Mhe. Suleiman Sarahan Said
12. Mhe. Ahmada Yahya Abdu-Wakil
13. Mhe. Miraji Khamis Mussa
14. Mhe. Shaib Said Ali
15. Mhe. Mohamed Said Mohamed na
16. Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame.

Waliochangia kwa Maandishi ni:

1. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
2. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
3. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf
4. Mhe. Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto
5. Mhe. Said Omar Said

Mhe. Naibu Spika, hao ndio wote waliochangia kama wengine nimewasahau ningeomba kukumbushwa, lakini nadhani hao ndio wote ambao walichangia kwa maandishi na kwa kutoa hotuba.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwanza nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mchango wao wake aliotoa kwa maandishi. Kamati hii naomba nichukue nafasi hii kuishukuru sana, najua pengine katika *process* za kibaraza wanaweza kuwa wajumbe wakabadilika baadae, lakini mpaka sasa hivi tulikuwa na wajumbe hawa wa kamati na Mwenyekiti wetu Mhe. Yussuf Hassan Idd ingawa mgonjwa Mungu ampe nguvu zaidi apone kwa haraka na Makamu Mwenyekiti mama Hamida Abdalla Issa amefanya kazi nzuri, ametusimamia kamati yetu wakati wa bajeti na wenzake wote. Kwa hivyo, naomba niwashukuru wote kwa sababu wametuwezesha, kutushauri, kutufikisha na kutupeleka mbele. Wao wenyewe Waheshimiwa Wajumbe mashahidi wameona tangu tumeanza Baraza hili la Wawakilishi kuanzia mwaka 2016 mpaka hivi sasa wizara inaleta hotuba zake zinaongezeka kwa ubora na viwango nyinyi wenyewe mashahidi.

Hotuba ya safari hii sio ile tuliotoa mwaka jana, sio ile ya mwaka juzi, yote kwa sababu ya michango yao Waheshimiwa ya busara na maelekezo wanayotupa imetufikisha kuleta hotuba iliyokuwa nzuri na kufanya kazi wizarani vile vile kwa bidii.

Katika hoja za kamati ningeomba nijibu kwanza hoja za kamati yetu. Kwanza walisema kwamba fedha zilizotolewa kwa ajili ya viwanda hazitoshi. Mhe. Naibu Spika, katika suala hili la kusema kwamba pesa tulizopewa za kuendeleza viwanda hazitoshi limezungumzwa na wajumbe wengine wapatao wanne mpaka watano na walipendekeza kwamba vifungu viongezwe.

Mhe. Naibu Spika, sisi wenyewe ndani ya wizara yetu tulipokuwa tunaanza kupeleka hoja hii ndani ya serikali tulijenga hoja hizo, tukaongezewa pesa zikafikia hivyo. Kwa maoni yetu sisi tunaona fedha hizo tukipewa tutaweza kufanya kazi kwa mwaka huu wa mwanzo na wakaona matokeo yaliyokuwa mazuri. Tungeomba tuendelee na fedha hizi tulizopewa lakini pia hazikutufunga kuendelea kuzungumza na wahusika mbali mbali kuweza kuweka mipango mizuri kwa ajili ya kujenga viwanda kwa kipindi cha miaka miwili hii iliyobakia. Kwa hivyo, tunaona kwamba fedha hizi turuhusiwe waheshimiwa wakubali zipite tuweze kufanya kazi. Hizi zitatuwezesha kwa mwaka huu mwanzo kuanza kujenga angalau *industrial park* moja lakini na viwanda vyengine ambavyo serikali imetoa ruhusa.

La pili, alizungumzia kuhusu suala la mali maiti. Katika mapato yetu kuna pato moja kama shilingi milioni moja kwa mwaka imetokana na mali maiti na hii tumeshapendekeza, tumeshaomba wizara inayohusika ni Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kihamishwe kifungu hicho katika hicho kitengo chetu sisi cha Wakala wa Biashara, Wasajili wa Biashara na Mali ili kiende katika Wizara ya Katiba na Sheria. Natumai mwaka huu tutaomba tena kwamba ichukuliwe hatua hii, nategemea kwamba Wizara ya Fedha watakubali kukihamisha kitengo hiki.

Jengine alilozungumzia Mhe. Mwenyekiti ni kuhusu suala zima la *PBOC* kwamba *PBOC* ihamishwe, yaani isimamishwe iwe tunafanya ukaguzi huu hapa hapa Zanzibar. Lakini pia alizungumzia kuhusu gari za vipande hili ambalo Naibu Waziri hakulizungumzia. Gari za vipande zinakatazwa na hatua zinachukuliwa kwamba gari zisikatwe kule kwa ujanja zikifika hapa zinahesabiwa kama gari nzima na unalipa kwa mujibu wa utaratibu uliowekwa.

Mhe. Naibu Spika, jengine ni kuhusu mazingira ya biashara. Mazingira ya biashara humu katika kitabu chetu imeoneshwa kwamba haina fedha, kwa sababu utaratibu mzima huu wa mazingira ya biashara bajeti yake imehamishiwa Bodi ya Leseni na vile vile imehamishiwa katika kitengo chetu cha Usajili wa Biashara na Mali.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kama nilivyosema wajumbe wengi wamechangia na Naibu Waziri sehemu kubwa ya majibu ameshatoa, lakini nitajaribu kujibu majibu katika *cluster* yake kwa pamoja ili tuweze kupunguza muda na tuweze kupata ufafanuzi uliokuwa wa kina.

Mhe. Naibu Spika, kwanza suala lililozungumzwa ni la maeneo tengefu, kuna wajumbe walitaka kujua maeneo tengefu hayo yako wapi na utaratibu gani ambao tunaufuata. Mimi ningetaka kwanza kuwaomba Waheshimiwa Wajumbe watukubalie kuwa safari hii tunajaribu kubadilisha sera na mwelekeo wa viwanda. Huko nyuma mwelekeo wa viwanda tulikuwa tunategemea viwanda ambavyo vitakuja hapa, viwanda ambavyo vitaweza kupunguza kununua bidhaa zetu kutoka nje. Lakini pia kwa kutumia mali ghafi kutoka nje. Muelekeo wa safari hii wa viwanda ambao ni muelekeo endelevu na muelekeo ambao utakaotupa faida kubwa sana kwa nchi yetu ya Zanzibar ni kujenga viwanda kutizama hali halisi ya mali asili iliyoko Zanzibar. Lakini viwanda ambavyo

vitaweza kuajiri watoto wetu wengi, lakini viwanda ambavyo vitatoa mali au *product* ambazo tutaweza kuziuza sio tu Zanzibar peke yake na nchi za nje ikiwemo Ulaya, China, Marekani na nchi za Ghuba.

Huo ndio muelekeo wetu na kama mnavyojua sasa hivi kuna masoko ambayo yapo kwa mfano kuna soko la *SADC* ambalo ni kubwa kuna soko la *AGOA* ambalo ni kubwa kuna soko la Ulaya ambalo nalo ni kubwa. Lakini kuna soko la nchi za jirani hapa za nchi za ghuba ambazo sisi na ndugu zetu wa damu ambao wanataka bidhaa kutoka Zanzibar. Huo ndio muelekeo wetu tunaokwenda nao katika sera nzima ambayo tunaitekeleza ya kufufua na kujenga viwanda vipya.

Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, tunapozungumzia suala zima la maeneo tengefu ya viwanda na hii imetoka na matukio ya sasa tuliyoyafanya na tulisoma tunaanzisha *SMIDA* kama ni kutuo kikubwa cha kushajihisha wajasiriamali na wenyewe viwanda wadogo wadogo wakati na vikubwa ni kwamba sasa hivi tutakuwa tumependekeza kuwa maeneo tengefu kila wilaya. Mpaka sasa hivi maeneo ambayo tumeshakabidhiwa ardhi tumeshaoneshwa ardhi kwanza tumeoneshwa ardhi eneo la Tunguu, kuna eneo tumeshaoneshwa ardhi tumeenda kukaguzwa kwa mujibu wa mipango miji ambayo serikali na Wizara ya Ardhi imepanga.

Vile vile kuna eneo tumeambiwa lipo sehemu ya Mkokotoni tunatakiwa twende tukaoneshwe na tukabidhiwe. Kuna eneo huku upande wa Magharibi karibu na *Airport* tumekwenda tumeoneshwa ni eneo ambalo nalo tunaweza kufanya hayo maeneo ya viwanda kwa ajili ya *Industry Park* ambazo tumezitaja katika bajeti yetu.

Lakini bado kuna maeneo mengine Wizara ya Ardhi inayashughulikia mpaka wapime na watutayarishie kabisa stakabadhi zote ndio tutajua kama maeneo haya yako sehemu gani. Lakini tumesema kwa maeneo matatu ya mwaka huu tumeshayaona. Pemba kuna eneo ukichukuwa kama lile la *SMIDA* hapo Kizimbani ni eneo ambalo tutaweza kuweka viwanda pale vya kushajihisha wajasiriamali.

Lakini pia kuna maeneo mawili ambayo tumeshapewa na serikali. Eneo moja ni la kiwanda cha Pujini cha Matunda kuna Wajumbe hasa nadhani Mhe. Mussa Ali Mussa amezungumza kiwanda cha Pujini tumepewa na serikali tukakisimamia na kukufanyia kazi kitasaidia mazao yote ya kilimo yanayotokana na upande ule wa Pemba. Kuna kiwanda chengine cha Ushindikaji ambacho kipo hapa Kizimbani nacho pia tumekabidhiwa rasmi na serikali tutakifanyika kazi.

Lakini kama nilivyosema mwanzo hapa hii haikutufunga kuendelea kufanya utafiti katika maeneo mengine. Kuna eneo la Shengejuu Pemba lile eneo la chumvi nalo ni eneo vile vile tengefu kwa ajili masuala la chumvi na hii ni mikatabata unatayarishwa baina ya muekezaji na wananchi wanaolima chumvi ambao ni kiasi ya vikundi 36 viko pale.

Kwa hiyo, ningeomba niseme tu Waheshimiwa Wajumbe msiwe na wasiwasi kwa bajeti tulilopewa tutaweza kuyapima maeneo haya kuyafanyia ramani na kuanza kutayarisha

vile vile tafiti mbali mbali ambazo za kiinjinia za kuweza kujenga maeneo haya. Tayari tushafanya tafiti za awali na michoro tunayo tutaendelea na kazi hii.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nataka nizungumzie ni kuhusu suala la soko na utaratibu mzima wa masoko. Ningeomba nizungumzie masoko ya ndani na masoko ya nje. Ni kweli nakubaliana na Wajumbe kwamba soko ni jambo muhimu sana huwezi kuwa na biashara bila ya kuwa na soko. Lakini soko linaweza kuwa ndani ya nchi na vile vile soko linaweza kuwa nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, tatizo tulilokuwa nalo hapa Zanzibar ni kubwa kwa sababu wananchi wetu wafanyabiashara bado hawajaweza kutumia masoko ya nje. Lakini pia mpaka masoko ya ndani kama changamoto hiyo iliyoko kuuza vitu Tanzania Bara lakini pia masoko ya kuuza humu humu ndani ya nchi, hayo nayo ni matatizo. Kwa hiyo, soko ni jambo muhimu sana ili tuweze kutumia haya masoko lazima tuwatayarishe wafanyabiashara wetu kuongeza uzalishaji ni moja ya jambo kubwa kwa sababu wakati mwengine masoko yapo lakini uzalishaji wa bidhaa zile hakuna wa kutosha.

Kwa mfano tunatakiwa tuuze sisi bidhaa za viungo, lakini bidhaa za viungo Zanzibar tumerudi nyuma huo ni mfano mmoja ambao tunataka tuhimizane Wizara ya Kilimo isimamie vizuri zaidi tugawane majukumu tuweze kusimamia kuhakikisha kwamba mazao haya ya viungo kwa mfano mmoja yanapatikana ya kutosha. Lakini soko lipo mimi sitaki sasa hivi kuzungumzia habari ya soko nje masoko yapo. Kwa mfano tumepata soko la mafuta ya makonyo tani elfu mbili hatuna uwezo huo wa kuzalisha, kuna soko la mafuta ya mkaratusi tani elfu mmoja hatuna uwezo huo wa kuzalisha, siri ni nini? Siri kubwa ni kuongeza uzalishaji wa vitu hivyo kwa hivyo masoko yapo.

Lakini upande wa pili wa masoko ni masoko ya ndani humu ndani ya nchi yetu, soko la Zanzibar pia tunatakiwa tuwe na bidhaa ambazo zinakidhi ubora, bidhaa ambazo zimetengenezwa vizuri na vifungashio vizuri, bidhaa ambazo zinatambulikana kwa wananchi na zilizokuwa hazina madhara kwa afya. Kwa hiyo, bado tuongeze uzalishaji katika maeneo haya.

Lakini pia niwaombe wananchi na Waheshimiwa hapa tutumie bidhaa za Zanzibar, kama mtu anaenda dukani kununua *Tomato saurce* anunue *Tomato saurce* ya Indonesia anunue ya Tanzania ya Zanzibar zipo hatununui. Kwa hiyo, Mheshimiwa tupende kilicho chetu ndio maana tukasema *Made in Zanzibar Products* lazima tuzikubali tununue kilicho chetu ili tuweze kuongeza hilo soko.

Lakini pia kwa upande wa soko la Bara tumefanya utafiti ndogo tu, tumegundua kuwa kuna bidhaa nyingi mbali ya hizi ambazo za viwanda ambazo zilikuwa zina usumbufu mkubwa ambao tumeshakaa tumekubaliana na tumepeana majukumu. Sasa hivi kama wamekuwa na utaratibu mzuri una vibali vyote wame-*register* kampuni yako Zanzibar ama *ZFPA* umepita *ZBS*, umepita *Chamber of Commerce* huna sababu ya kuzuiliwa mizigo yako Bara.

Lakini tufate taratibu na sisi wizara yetu tutaendelea kuwaelimisha wajasiriamali, mwaka jana tumewaelimisha wajasiriamali zaidi ya 50 na vikundi zaidi ya 50 tumevipa elimu na kuwaelimisha. Kitu tulichofanya sisi kupitia *trade market* na kupitia chombo kile cha Ulaya tumeona kwamba kuna haja ya kutayarisha vikaratasi vya ufafanuzi. Kwa sababu ni kweli watu wetu Zanzibar hawaelewi taratibu za kuuza nje, hawaelewi taratibu za kuuza ndani. Kwa hiyo, utaratibu tumefanya tutatoa mafunzo na tutatoa vipeperushi ili kila mmoja na mfanyabiashara aweze kujua hatua gani zinatakiwa azifanye.

Soko la ndani Mheshimiwa Idara ya Masoko hapo zamani kama mnavyojua ilikuwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Sasa hivi Wizara ya Biashara na Viwanda, masoko haikuondoka maana kuna watu wanakanganyika sasa hivi hapa. Masoko haikuondoka kwa sababu masoko ni sehemu ya Idara ya Biashara.

Kwa hivyo, tunachotakiwa tushafanya utafiti na tushafanya utaratibu mzima wa kuona tutapanua zaidi suala zima la masoko yakiwemo masoko ya Jumapili, masoko ya wakati wa sherehe maalum kwa mfano kama matamasha na masoko vile vile yalioko nje ya nchi hayo yamo ndani ya idara yetu ya masoko. Kiasi gani tutawashajihisha wananchi wetu waweze kutumia masoko hayo ni hiyo kazi ambayo tunaifanya mwaka huu kwenye bajeti tutafanya kazi hiyo.

Masoko ya Jumapili yalikuwepo hapa Zanzibar pia na Pemba yalikuwepo lakini yakaonekana baada ya kuongezeka yanafifia. Kila Jumapili watu wakienda wanakuta bidhaa zinakuwa zina upungufu au watu wengine wanaotakiwa wakauze wanapungua. Lakini tumeona iko haja ya kufufua masoko ya pamoja na masoko ya Jumapili.

Mhe. Mwenyekiti, niseme suala zima hili la biashara sisi na Bara, kwa sababu sasa hivi kama mnavyojua Bara biashara nyingi za Zanzibar zinakwenda lakini hazionekani kunako takwimu na hili tumeligundua ni jambo ambalo ni udhaifu uliomo ndani katika utaratibu wetu, tunaufanyia kazi. Kwa mfano tumeambiwa huko kwamba zao la tikiti kuna miaka nyuma tikiti peke yake tuliweza kuuza Bara kwa taarifa za wenyewe wenye Kamati yao ya Matikiti kama bilioni nane zilipelekwa Bara za matikiti. Mimi naambiwa juzi juzi hapa kwa mwezi mmoja masusu ya tungule yamepelekwa Bara ishirini elfu, lakini takwimu zake hazipo hazijawekwa vizuri. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba niseme kwamba kuna kazi kubwa tunatakiwa tufanye wizara yangu, Wizara ya Mawasiliano na Wizara ya Fedha na Mipango na Wizara ya Kilimo tukae pamoja tuweke utaratibu mwengine tafauti wa kuweza kujua kwamba kwanza tubadilishe mauzo yetu. Hivi leo tunauza vitu hivi hatutumii kilo, tunauza kwa mafungu. Jamani kwa mafungu mtaweza kuweka *statistic* zipi? (*Makofi*)

Kwa hiyo, mwaka huu tunataka kufanya utaratibu bidhaa zetu zote hapa Zanzibar zimetumie utaratibu wa *metric* kama unauza samaki uuze kwa kilo, kama unauza tungule uuze kwa kilo, unauza mbatata uuze kwa kilo. Hayo yatatuwezesha kuweka takwimu zilizokuwa sahihi tutakaa kuonana na wenzetu wa Wizara ya Biashara kumaliza hilo.

Jengine la ujumla Mhe. Mwenyekiti, ni kuhusu hapo hapo kunako biashara. Hii hotuba yetu tumefanya kwa makusudi kukuonesheni kwamba tunao uwezo wa kufanya biashara nje ya Zanzibar, nje ya Bara. Humu takwimu zilizooneshwa ni sahihi lakini pia zinaonesha kwamba tunaweza kuuza bidhaa kupeleka Kenya kupeleka Uganda na nchi nyengine.Hii takwimu ilikuwa imeonesha Uganda peke yake kwa sababu ndio takwimu ambazo tumezipata katika vyombo vyetu ambavyo tumeenda kuchukuwa hizi hesabu.

Lakini pia Kenya kuna biashara lakini sasa tatizo la Kenya biashara za Kenya sio za kudumu kwa sababu biashara za Kenya mara nyingi zinakuja Zanzibar Pemba halafu zinarudi tena kule kule. Kwa hiyo, takwimu zake za Kenya haziko *reliable* ndio maana hatukuzionesha huku, lakini za Uganda ziko *reliable.* Lakini inaonesha kwamba tuna uwezo wa kufanya kazi huko na tukaweza kupata fedha. Kwa mfano Afrika ya Kusini tumeonesha humu tumeuza sehemu nyingi kwa nini wafanyabishara wetu wasilazimishwe, wasisaidiwe, wasipewe nguvu na *incentive* ili waweze kuuza nje. Lakini tunaangalia hapo hapo Bara tu kwa sababu Bara kuna taratibu zake ambazo tunazisimamia safari hii ili tuweze kupeleka bidhaa nyingi zaidi kule Bara lakini vile vile bidhaa nyingi zaidi nje ya Tanzania Bara.

Jambo jengine ninalotaka kulizungumzia ni masuala ya *branding, branding* imezungumzwa na Wajumbe wengi lakini zaidi Mhe. Simai Mohamed Said alikuwa anazungumzia suala la Zanzibar. Mhe. Simai Mohamed Said jina la Zanzibar hatujaweza kwenda kulirikodi kuliwekea *partent* kwa sababu lazima unapokuwa na *brand name* lazima ukali-*register*, ndio maana wajanja wanatumia jina la Zanzibar. Sisi tumeanza ku-*register* kwa sababu tulianza kwenye utaratibu wa karafuu tulianza kuzi-*register* za Zanzibaar. Lakini pia kwa sababu katika huu utaratibu mradi wa *made in Zanzibar* tutaendelea mbele zaidi.

Wamekuja wataalamu wa *WIPO* tumezungumza nao na wametwambia kwamba watatusaidia katika suala zima lote hili kuangalia Zanzibar nzima inakuwa ni *brand*. Kwa sasa hivi Zanzibar kwa huku nje sio *brand* ni *brand* ambayo tunataka tuitayarishe sisi Zanzibar kuna wajanja wanaitumia. Kwa hiyo, ni kweli kuna haja na kazi kubwa ya kufanya ili Zanzibar yenyewe iwe ni *brand*. Kwa hiyo, kila kinachotoka Zanzibar kikitoka Zanzibar kionekane kwamba hii ni *brand* ya Zanzibar na inayokubalika. Hiyo kazi tunaifanya katika hatua ya pili la *branding*.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala la viwanda vya zamani, hili ameshajibu Mhe. Naibu Waziri. Lakini nataka nitoe ufafanuzi zaidi kwa viwanda viwili kwa upande wa *Cotex* hili jambo tumelizungumza serikalini tumefikia mahala pazuri. Mwenyewe kiwanda cha *Cotex* yuko tayari kuzungumza na sisi aidha aliuze lile eneo tulichukuwe tufute ile leseni yake, tulichukuwe tulifanyie matumizi mengine au kama kuna muekezaji kwa mfano juzi kuna muekezaji wa kutengeneza madengrizi tukamwambia kwamba yeye atakubali kwenda kuchukuwa *Cotex* kaenda akasema kwa yeye kikubwa zaidi, haitaji kwa sasa hivi. Kwa hiyo, tunaangalia katika mambo mawili zaidi aidha tukichukuwe iwe sehemu ya eneo tengefu kwa hapa Mjini Zanzibar au la pili tukichukuwa aje muwekezaji tuweze kumkabidhi.

Kiwanda cha soda Mhe. Naibu Spika, nimeshatembelea si mara moja si mara mbili. Tatizo kuu kiwanda cha Soda kwamba bado wana ushindani na watu wa soda wa nje. Soda inatoka Dubai kwa mfano Kibati kile Dubai kile cha Soda shilingi elfu moja. Lakini soda yake hawezi kushindana na kiwanda kilichotoka nje. Kwa hiyo, cha kufanya sasa hivi sisi na Wizara ya Fedha nafikiri mimi bajeti hii itakapokuja maana tulitoa hoja kwamba tulinde viwanda vyetu. Njia moja pekee ya kulinda vyetu ni lazima tutizame suala zima la kodi. Lakini pia ukishaweka kodi haina maana kwamba watafuata kwa sababu kuna mpenyo kule Bandarini. Kwa hiyo, kuna *smugly* nyingi utakuta soda zinatiwa kunako magari, kwenye mambo mengine mengine tusimamie. Tukisimamia uzuri bandarini tutaweza kulinda viwanja vyetu. (*Makofi*)

Jengine Mhe. Naibu Spika, suala lililozungumzwa kwa ujumla alizungumza Mhe. Miraji Khamis Mussa kuhusu uchumi hasa *deep sea fishing* yaani uvuvi wa Bahari Kuu. Mhe. Naibu Spika, alitaka kujua sisi tumejiandaa vipi. Natagemea kesho Mhe. Waziri wa Kilimo ataeleza kwa upande kwa sababu tunafanyakazi pamoja sisi na wenzetu wa Wizara ya Kilimo. Katika suala zima la uvuvi kuna kitu kinaitwa *blue economy*, kwa hiyo ndani ya mkakati wetu wa MKUZA tumezungumzia *Blue economy* kwamba sio tu kuzungumzia *deep sea fishing* yaani Uvuvi wa Bahari Kuu peke yake lakini kuzungumzia masuala yote yanayohusu bahari na vilivyomo baharini kuvivua kuvifanyia kazi, kuvisindika, kuvikausha na kuviuza.

Mhe. Naibu Spika, katika mantiki hiyo basi Uvuvi wa Bahari Kuu ni sehemu ya kufanya kazi hiyo. Kama mtavyojua Shirika la *ZAFICO* limeshaanza na jitihada mbali mbali zimeshaanza kuchukuliwa Waziri wa Kilimo atakuja kueleza kesho sisi kama wabia kama *ZSTC* na vyombo vyengine ni wabia za Shirika la *ZAFICO* na kuna mtaalamu aliekuja maalum kwa ajili ya *ZAFICO* na amewapata mapendekezo mazuri sana wameyafanyia kazi. Niseme suala zima la Uvuvi wa Bahari sisi wenyewe kama serikali tutafanya kazi hiyo, lakini pia tunawapa leseni Kampuni binafsi kutoka nje kwa ajili ya shughuli za Uvuvi wa Bahari Kuu.

Sasa Bahari Kuu kuna mambo yanatakiwa yafanywe kuwe na mahali vyombo viweke nanga, soko liwepo kunatakiwa na mahali pa barafu kuweka wale samaki na mambo mengi. Kutakuwa na vyombo ambavyo vitafika katika Bahari Kuu hasa kwa ajili ya wavuvi wananchi, haya mambo ni mradi mkubwa. Tumekaa juzi sisi na wenzetu wa *ZAFICO* tumetayarisha waraka, waraka huo unakwenda *UNIDO* ili kuangalia sehemu kubwa ya mradi huu wa Uvuvi wa Bahari Kuu unajumuisha na vitu vyengine vingi, sio unakuwa una boti una meli lakini huna mahali pa kuwaweka samaki, huna mahali pa kuweza kutengeneza samaki. Kwa mfano juzi kampuni moja ya China imesema watatuletea kiwanda cha samaki na sisi wenyewe tumeanza jitihada ya kuwaleta wawekezaji ambao watawekeza katika sekta ya samaki. Kwa hiyo, hili la uvuvi wa Bahari Kuu linafanyiwa kazi kubwa sana na serikali yetu, chini ya uongozi wa mwenyewe Rais Dr. Ali Mohamed Shein.

Jengine ni uvuvi mdogo mdogo, uvuvi mdogo mdogo pia kuna mradi ambao wanashughulikia hawa wezetu wa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kuwapatia vijana hawa vyombo vitakaowawesha kuvua kule, kwa mfamo Mhe. Rais alipokwenda Comoro

alikuta Kampuni kule ya Comoro ambayo inashughulika na mambo ya uvuvi waliweza kutengeneza maboti na kuwawezesha vijana kwenda kuvua katika bahari ambayo kubwa kidogo. Kwa hiyo, hili nalo vile vile kupitia serikali Wizara ya Kilimo Sekta ya Uvuvi wanalifanyia kazi. Watalizungumza wenyewe kesho kwenye bajeti yao.

Lakini jengine ambalo nataka niliongeze katika utaratibu mzima wa kuangalia biashara hii ya *blue economy* uchumi wa bahari. Kuna suala zima la ufugaji wa viumbe vya bahari, huko Pemba kuna sehemu nyingi na watu wengi wamepata mafunzo kwa ajili ya ufugaji wa samaki, ufugaji wa kamba, ufugaji wa pweza, ufugaji wa *prawns* wamefundishwa vijana wengi kuna vikundi vilivyokwenda mpaka China kujifundisha.

Kwa hiyo, jambo linatakiwa sasa hivi kuwasogeza ndio kazi ambao tunaifanya sisi katika utaratibu mzima wa viwanda, tutafanya kazi hii kuwawezesha vijana hawa waweze kufuga na waweze kupata soko, soko lipo Wachina wamekuja hapa tumewasimisha tukawaambia kwanza msije kununua kwa sababu hatujaweza kuwa na vijana madhubuti.

Lakini pia suala zima la viwango na kuweza kutoa vyeti vilivyokuwa vinakidhi haja. Hilo nalo limo katika Bajeti ya Viwango *ZBS*, kwa mfano *laboratory* ya vyakula tuweze kama mtu anafanya biashara hii ya kuuza samaki au pweza au mfano majongoo ya pwani nje lazima apewe hati ile inayothitisha kama imepitia katika vyombo vya viwango.

Jengine katika hili la uvuvi Mhe. Naibu Spika, ni ukulima wa baharini. Ukulima wa baharini hili ni jambo tumepewa na wataalamu wa *UNIDO* tumezungumza pamoja sisi na Wizara ya Kilimo hatujui ukulima wa bahari nyie wengine hamjui ukulima wa bahari. Lakini tunaambiwa kunakokaa mwani na wananchi wa nchi za nje wanalima kule kule wanalima majongoo ya pwani, wanalima chaza wale wakubwa, wanalima mpaka hawa wadogo wadogo *prawns* na kadhalika. Kwa hilo nalo ukulima wa baharini nalo tunalifanyia kazi ili sekta nzima hii ya *blue economy* iwe imefanyiwa kazi.

Mhe. Naibu Spika, nilitaka nitoe kwa ujumla sasa nije katika yale mambo ambayo Mheshimiwa amekuwa hajaweza kuyazungumza. Mhe. Naibu Waziri amezungumza sana na mengi mazuri lakini nitaongezea yale ambayo yameachwa.

Mhe. Naibu Spika, labda niseme tu kuhusu suala la *value chain* alizungumza Mhe. Miraji Khamis Mussa akataka kujua suala zima la *value chain*. Mhe. Naibu Spika, kama niliposema pale mwanzo huko ndiko tunakokwenda. Kwa sababu tulivyozungumza *value chain* hatuzungumzii kiwanda kimoja na maisha natoa mfano wa *ZSTC*. *ZSTC* kama kama tutazungumza *value chain* kama ndio kiwanda mama na mimi napenda kukiita *ZSTC* kama nyangumi wa viwanda hapa Zanzibar. (*Makofi*)

ZSTC kwa mfano huo sasa hivi utanunua mafuta mfano ya mchaichai au mafuta ya mkaratusi ambayo wananchi mtakuwa mnaweza kutengeneza wenyewe kuna vikundi kule Pemba hata Unguja wakipewa nyenzo wakipewa na vile vyombo vya kutengenezea mafuta wataweza kutengeneza *semi refined* ambayo haijakamilika. Baada ya hapo watauza *ZSTC* na *ZSTC* kwa sababu ya uwezo waliokuwa nao watasafisha zaidi

watafunga vizuri zaidi wataweza kuuza nje huo ni mfano mmoja wa mnyororo wa thamani.

Lakini tunaweza kusema mifano mingi sana kwa mfano kiwanda cha nguo, kiwanda cha nguo ndio kama kitakuja Unguja tutafungua wananchi kama wanchukua nguo vitambaa wanauza wananchi watafungua viwanda vyao vidogo vidogo au koponi za kushona wakashona wakauza nje. Kwa hivyo tunapozungumzia mnyororo wa thamani kama inakuwa unaunganisha jitihada mbali mbali za wananchi na huko ndio tunakokwenda sisi kwa vile vile kama nilivyosema wa Mhe. wetu Rais wetu mpenzi Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein.(*makofi*)

Jengine niseme kwamba katika hii sekta ya utaratibu wote wa viwanda lazima uweze kujiuliza kwamba alisema Mhe. nadhani ndie Mussa kwamba hakuna usimamizi au mjumbe mwengine yumo humu katika *list* yangu kwamba hakuna usimamizi. Lakini naomba nimtowe wasiwasi kwamba huko nyuma inaweza kuwa kwa sababu sio Zanzibar tu mashirika mengi haya viwanda yalikufa kwa sababu mambo mapya haya usimamizi watu wetu walikuwa hawana utaalamu wa kutosha na mali ghafi.

Lakini sasa hivi tunafikiria kwanza kuwashirikisha wenzetu wa *private sector* kwa kuendesha viwanda hivi, *private sector* wanao uwezo huo na vile vile hili suala faida linamsumbua sana kwa hivyo watasimimia lakini pia tumesema hebu tutazame mabaraza ya vijana na wenzetu wa halmashauri kama watapewa utaalamu wa kusimamia viwanda hivi tumeona sehemu nyengine za Bara wanaweza kusimamia ukawa usimamizi nzuri zaidi lakini pia SMIDA, moja ya jukumu la SMIDA ni kuona kwamba wanasimamia na kuwaelekeza na kuwalea hivi viwanda vyetu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika haya yote Mhe. yatakuwa yameenda vizuri.

Sehemu nyengine Mhe. Naibu Spika, nije nijibu suala Mhe. Jaku ambalo hili ni peke yake Mhe. Jaku alizungumzia utaratibu huu wa usafirishaji wa fedha, Mhe. Naibu Spika kweli kumetokea kesi kama mbili tatu hapa Zanzibar lakini tunapokuwa tunasafirisha pesa kuna utaratibu ambao upo kisheria na ningeomba wafanyabiashara wa Zanzibar wafuatate utaratibu huu wa kisheria.

Kuna sheria Mhe. Naibu Spika inayozuia *money laundering* sheria hii namba 9 ya mwaka 2009 lakini pia kuna kanuni 70 ya mwaka 2013 ambayo inazuia *money laundering* lakini hata katika *level* ya umoja wa kimataifa tatizo lilioko kubwa nchi za kiafrika fedha zetu zinatoka zinapelekwa nje au pesa za dawa zinazungushwa humu ndani, kwa hivyo ni matatizo makubwa mpaka Umoja wa Mataifa mpaka Afrika *new* wanasimamia hata Afrika Mashariki wanasimamia.

Kwa hivyo, sheria hizi zimewekwa utaratibu wa kisheria jambo ambalo limekosekana wewe mwisho wako kuleta pesa zako za kigeni ni dola 10,000 kama una pesa zaidi ya dola 10,000 hujakatazwa lakini lazima useme ujaze katika makaratasi, huwezi kutoka na dola kama 100,000 kule katika mfuko wako umetia unaondoka nazo hiyo kinyume na sheria kwa sababu sio tu sisi Zanzibar, Bara lakini dunia nzima. Mimi najua dunia nzima ukisafiri na pesa zaidi ya dola 10,000 unajiingiza mwenyewe kwenye matatizo.

Naomba nikuhakikishieni kwamba wizara ya fedha ina jukumu la kutayarisha hizo karatasi za kutoa za kuweza ku-*declarer* yaani za kueleza kwa sababu unatakiwa ukifika pale *air port* unatoka unaeleza na ukirudi kama unaingia na pesa unaeleza. Kama mimi natoka na pesa dola zangu 50,000/- au 100,000/- hizo karatasi ndio ambazo bado hazijatengenezwa. Kwa hivyo nimeshahakikishiwa kwamba karibu baada ya bajeti karatasi hizi zitatengenezwa ili wananchi waweze kuondoka na utaratibu ambao mzuri.

Mhe. Naibu Spika, nije katika hoja ya Mhe. Dimwa za ziada Mhe. Dimwa aligusia katika vifungu ukichukia R01 usimimizi wa Mamlaka ya Utoaji wa Leseni katika bajeti ya 2017 hadhi 2018 wizara imeanza na mamlaka 25 jumla za mamlaka 45. Kwa hivyo usimamizi kwa mwaka huu 2018/2021 usimamizi wa mamlaka 45 za utoaji wa leseni ndio zilizopo mpaka za SMZ 27 serikali za Mitaa 11 na SMT ziko 7. Tatizo hili Mheshimiwa ni nyeti kwa sababu kwa nini tukaambiwa tuaangalie kwanini ikaundwa bodi ya leseni. Kwa sababu ilionekana kule nyumba kuna vyombo vingi vinatoa leseni vinatoa mambo mengi.

Kwa hivyo serikali ikasema ili kuweza kuimarisha biashara na kurahisisha biashara basi tuangalie vile vile utaratibu mzima wa kufanya biashara ndio maana ikaundwa bodi ya leseni na kazi hii nzuri wameshaanza kufanya na wanaendelea, kuna vikao vingi washafanya na kuna mapendekezo yatakwenda serikalini kwa baadhi ya hivi vyombo vinagongana ili viweze kuwa utaratibu mtu akienda mahali kununua leseni kumoja basi awasilishe na kwengine kote ambako wanatakiwa awasilishe ile leseni.

Lengine Mhe. Naibu Spika, kuhusu Mhe. Dimwa alizungumzia kunako kifungu kuhusu tafiti akataka kujua tafiti tunazozifanya kwa mwaka huu ningeomba nimtajie tafiti kwa mwaka huu, 2018/2019 ni bidhaa kutoka soka la *Agoa Made in Zanzibar Product* mambo haya ya kuondosha vikwazo vilokuwa sio vya biashara na utaratibu wa kupata fedha *finance agriculture project* miradi ya kilimo, utafiti wa matokeo ya mfumo wa utoaji leseni, suala zima la mradi ule wa maji Zanzibar na suala la mwani ndio tafiti tunazimaliza zimeshaanza lakini hasa tafiti kubwa zitakuja baada ya muda na tafiti nyengine ndogo ndogo.

Kwa upande wa sera Mhe. Naibu Spika, tunamalizia sera ya *industry of policy* sera ya viwanda, tunamalizia sera ya biashara, tunamalizia sera ya PP yaani mahusiano ya wafanyabiashara na sekta binafsi na sekta ya serikali.

Mhe. Naibu Spika, suala la Mhe. Dimwa na wengine walizungumza suala zima la sukari na hili limeshajibiwa vizuri, nataka nikuhakikisheni waheshimiwa wajumbe kwamba suala la sukari chini ya uongozi wa Mhe. Rais wetu tumelisimamia vizuri na karibu maamuzi yatatoka ukizingatia maslahi ya nchi lakini pia kuzingatia maslahi ya kiwanda chetu na maslahi ya wafanyabiashara ambao wanatakana na wao wapate riski ya kuendeleza biashara zao.

Kwa hivyo, suala hili matarajio yangu baada ya bajeti tarehe mosi Julai kama tutakuwa na kikao cha serikali kumalizia hoja za kiwanda cha sukari tutakuwa na maamuzi mazuri

na kiwanda chetu kitaweza vile vile kulindwa kwa nguvu zote za Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, alizungumziwa Mhe. Dimwa kuhusu *incentive* gani ambazo tunazitoa Mhe. Naibu Spika, *incentive* zinazotolewa na ZIPA ni nzuri sana incentive za Zanzibar kwa ajili uwekezaji ni nzuri sana lakini pamoja na hayo tumeona kuna haja yakuzipitia. Kwa hivyo Wizara ya Fedha na sisi tunawasaidia kwa upande wa watu viwanda tunazipitia zote ili tuweze kuwa na kitu ambacho kitaweza kutufikisha pazuri na tutawashaijisha wawekezaji wengi kuja hapa kwetu kuwekeza.

Mhe. Naibu Spika, juzi nimetoka China jambo ambalo nilisistiziwa kule China na hili namjibu Mhe. Dkt. Mwinyihaji kwamba kuna nchi inafanya vizuri kuwaleta wawekezaji kutoka China na nchi hiyo ni Ethiopia Mhe. Naibu Spika. Mimi Ethiopia nimefanya kazi na ninajua nimeshatembelea lakini hii ambayo ni eneo tengefu ni kubwa Afrika nzima na limefanywa na Wachina na sisi tumeufanya mkataba na kampuni moja ya kichina ya kuweza kutushajisha wawekezaji kuja Zanzibar. Nimeambiwa mambo mawili lakwanza niloambiwa tembelea Ethiopia ukaone jinsi Ethiopia walivyoweza kupata viwanda kwa muda mfupi sana kutoka China.

Na jambo hili nilizungumza na watu UNIDO Na pia nimezungumza na serikali nimepewa baraka za kwenda lakini tunangoja bajeti ishe na kujiandaa kubwa Waheshimiwa Wajumbe sitaki kwenda Ethiopia nikarudi na wawekazaji mfano China wanataka ardhi, ardhi haijapangwa vizuri, wanataka mambo mengi mengi ukiritimba unakuwa mwingi mpaka tumalize masuala haya ndio maana nikasema tumeshaoneshwa maeneo ya ardhi ya viwanda na mengine tutaoneshwa zaidi ili mtu anapotoka kutoka kule anakuja tunamuonesha kitu cha uhakika kipindi kifupi anaanza kuekeza.

Vile vile la pili tuliloambiwa, tukaambiwa angalieni utaratibu wa vivutio walivyofanya China ambavyo Ethiopia wamevikopia mikishavijua hivyo, mtakuwa rahisi na nyinyi vile vile kufanya kama Ethiopia bahati nzuri tushapata taarifa zote ya vivutio vya wachina ambao katika huo utaratibu mfumo mpya ambao tunaupitia tutangalia yale ambayo yana maslahi na Zanzibar, lakini niseme tena Zanzibar vivutio vyetu ni vizuri juzi tu tumetoa hapa utaratibu zima wa vivutio kwa miradi ambayo inaitwa miradi muhimu ya kitaifa.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Dkt. Mwinyihaji alizungumzia kuhusu kilimo cha hai tofauti ya kilimo hai na kilimo cha kawaida watu wengi hawaelewi nilitaka niliseme hili watu wengi hawaelewi. Kwa kweli sehemu kubwa ya Zanzibar tunatumia kilimo hai, kama ukisema kilimo hai cha kawaida sehemu kubwa ya Zanzibar tunatumia kilimo hai lakini hakiendi bila ya kuona tuna vyeti vinavyotakiwa kwa hivyo ndio maana hawa wakulima wa karafuu ambao wanalima karafuu kwa kilimo hao ndio watu ambao wamepata *certificate* zote wanaangaliwa wanakaguliwa na wanafanya kazi vizuri .

Mhe. Naibu nikisema ndani mtacheka hapa watu wanaambiwa karafuu walikuja Wajapani fulani, Wajapani walipokuja wakapelekwa Pemba Mtambwe, wakapelekwa Konde kwa Mhe. Omar Seif kule wakakuta mahali kinyesi cha ng’ombe na karafuu ziko

karibu hapo hapo, wakasema hii haiwezi kuwa *organic* kwa nini? Kwa sababu *organic* wanakula watu kwa hivyo vitu kama vile unapokausha karafuu, unapokausha vitu vyako uwe umevifungia haviingii vumbi havingii upepo na vitu kama kinyesi cha wanyama na kadhalika kila kitu kinakuwa safi, mimi nimekwenda Ujerumani hivi juzi tumeoneshwa vitu vingi vya *organic.* Sasa hivi kila jambo watu wanapenda vitu hai, kwa hivyo kama hutumii madawa unatumia mbolea mfano mbolea ya kinyesi cha ng'ombe au vitu vyengine ambavyo havidhuru afya ya mtu. Kwa hivyo kwa msingi huo ndio inakuwa hai na sisi mwaka huu tunawataalamu tumeshakutana na wataalamu tunatayarisha sera ya kilimo hai, lakini pia sio sera tu kuwasimia na kuwaongoza wananchi wa Zanzibar waweze kulima kilimo hai kina manufaa makubwa Mhe. Naibu Spika, na sio kigumu hata kidogo, lakini hapa Unguja tunae Dkt. Mwatima anasomesha vikundi mara kwa mara tunakwenda na ningewaomba Waheshimiwa wenzangu Wawakilishi muwe mnaangalia kule kwa Dkt Mwatima anatoa *course* hizi.

Mhe. wangu Mhe. Omar Seif Abeid yeye yuko kule anawaona watu wake yeye ni mkulima nambari *one* na yeye angie kilimo hai, pesa nzuri ziko huko Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo katika kutoa majibu nimejaribu kutumia muda mfupi ili tuweze kumaliza vizuri na tuweze kwenda vizuri.

Suala *Online registration* bajeti sio kidogo bajeti yao inatosha kwa sababu kazi nyingi washafanya vifaa vishamaliza kuwekwa wako wataalamu na wataalamu hao jamani suala la maslahi sinayo mimi Wizara ya Biashara peke yangu, maslahi ya wataalamu wote yanasimiwa na Idara Kuu ya Utumishi. Kwa hivyo na Utumishi inaangalia maslahi ya kila mtaalamu kwa hivyo musiwe na wasiwasi maslahi ya wataalamu hawa na wao vile vile yanaangaliwa kwa mujibu wa sheria za utumishi na kwa mujibu wa utaratibu ambao tumejiwekea, kwa hivyo msiwe na wasi wasi mkubwa.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho kabisa kabla sijapigwa mabuti nalo hili kalzungumza Mhe. Jaku kuhusu gharama za kusafirisha vitu kutoka bandarani Bara kwa mfano mafuta, ni kweli kule Bara kama vitu vinatoka Burundi, Congo, dola tatu lakini kutoka Zanzibar dola kumi na vile vile kuna tatizo moja la kuweka mizigo yetu kule Bara ukiweka mizigo watu wanaruhusiwa siku saba. Lakini Wanzibari siku tatu wanatakiwa waondoshe hili lilizungumzwa na kweli tumezunguza na tumekaa, kuna mjumbe hapa alisema kwamba hakuna kweli nadhani Mhe. Dimwa hapana tumezungumza kwa ukweli kabisa kabisa. Tumekubaliana mpaka leo hatujasikia malalamiko ya watu tumeweka *hotline* mbili moja Ofisi ya Makamu wa Pili moja Ofisi ya Makamu wa Rais wa Tanzania kama wanaopata matatizo kama haya watuletee. Hadi leo hakuna mfanyabishara ambaye ametuletea ninayo kesi moja tu na hii kesi ni kwa sababu ya masuala ya sukari. Kwa hivyo tumefanya tumekaa kwa dhati kabisa lakini jengine niseme juzi nimemuona Waziri wa Afya akifungua mkutano wa chombo cha Mamlaka ya Chakula na Vipodozi, wamekaa pamoja watu hawa Zanzibar na Tanzania Bara wamesaini mkataba, wameweka utaratibu mzuri, jamani wakati mwengine tusiwalaumu msilaumu sana.

Hitilafu za kimuungano za kibiashara mimi niseme si mambo ya ajabu nchi zote kunakuwa na hitilafu hizo aidha nchi kwa nchi, nchi yake na jirani yake yatokea hayo. Lakini sisi kwa taratibu tulizojiwekea mambo ya muungano tumekaa tumekubaliana

iliyobalia ni kamati mbili tu. Kamati hizo waliomba wenzetu wa Bara na wenzetu wa SMZ hapa sisi tukasema sawa na sisi tunabajeti, tukasema basi tungoje basi bajeti zishe ili masuala kama haya ya bandari ya gharama hizi yamesema yazungumzwe mamlaka ya bandari kule Bara na huku Zanzibar. Lakini tukasema Mamlaka ya bandari tutaweza kushirikiana na sisi kuweza kulizungmza suala hili.

Kwa hivyo nayo haya Mhe. Naibu Spika, yatakwenda tuwe na subira yatamalizika haya. Lakini niseme vizuri wafanyabiashara wa Zanzibar watizame pia nchi nyengine na sisi mwaka huu tafiti mmeziona hizi, tunataka kufanya kuweza kuhakikisha kwamba tunaweza kuingia maeneo mengine ya kibiashara. Lugha ya Kiswahili humu naomba Waheshimiwa wangu mtusamehe kwa sababu nina wataalamu wataalamu washazozea lugha kitaalamu kukondoesha, sijui lugha gani nyengine hizi lugha kitaalamu. Kwa hivyo mtusamehe maana kukondoesha ni kuzitia pamoja mambo ambayo yako nje unayaingiza pamoja mtusaheme kwa lugha. Sisi tutajitahisi kwamba hata sisi kwenye vikao vikubwa tunapokaa huko kwenye serikali tunakosolewa pia tunaambiwa wote sisi serikali kwamba lugha tumieni lugha fasihi ya Zanzibar na tumepata kamusi juzi tunashukuru kwamba sasa hivi tutakuwa na lugha iliyokuwa nzuri zaidi.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, ningependelea kusema sana lakini naogopa kupigiwa kengele kwa hivyo naomba niishie hapa Mhe. Naibu Spika kama kuna masuala mengine ambayo sikuweza kuyajibu yote Mhe. Naibu Spika, tuombe tu kwamba tuyafanyia kazi. Lakini niseme kwamba wizara yetu tulivyoikuta miaka ile na sasa hivi tofauti, tunaomba mtupe moyo zaidi kama mlivyoptupa moyo kwa sababu kujenga viwanda si jambo la siku moja na vile vile kusimamia viwanda si jambo la siku moja ni jambo ambalo linatakiwa mipango madhuti na ushirikishaji wa wote wote ambao wanahusika.

Tumeshakaa mpaka na watu wa Tawala za Mikoa Mhe. Naibu Spika, kwa sababu unapokuwa na sehemu unataka kujenga kwa mfano kama hichi cha Kizimbani tumesema kiwanda kile tuangalie tuanze japo tungule. Lakini suala linakuja tungule hizo mnazo kwa hivyo lazima muangalie mambo yote unapokuwa utatoa maamuzi ungalie mambo yote kwanza upatikanaji wa hivo vitu soko lake la ndani na la nje nani anatakaesimamia kiwanda hicho nani watakaoshiriki kufanya kazi hizo mambo yote tumeshaanza kazi na tushaanza kuzungumza na wizara zinazohusika kwa ajili ya kukuza viwanda.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi naomba mtupitishie bajeti yetu mia juu ya mia na mwenye suala lolote lile aje atakaribishwa ofisini kwetu kupatiwa maelezo ya ziada ili tuweze kufanya kazi. Kwa sababu sasa hivi tukimaliza kazi hii tunatakiwa tuje kunako mawilaya kwa hivyo msitukawilishe kuja kwenye mawilaya tumejindaa tunataka kuja kwenye Wilaya kila wilaya, tunataka kila Wilaya waweze kamati yao ya halmashauri au kamati yao ya maendeleo watwambie viwanda gani wanaweza kusimamia na sisi tuhangaike kutafuta viwanda.

Kuna watu wanakuja mwezi Julai, kuna watu wanakuja mwezi agosti, kuna watu wanakuja mwezi Novemba hawa wote ni wawekezaji ambao wako tayari kufanya kazi na wananchi wa Zanzibar na hasa wakiwepo vijana na kinamama na wazee nao wastaafu mnaweza kufanya kazi ya viwanda mkafanya mazao ya kitalii yakaweza kuuzwa, kwa

hivyo naomba kama niposema pale mwanzo mtuunge mkono, mtupitishie bajeti yetu mia juu mia Mhe. Naibu Spika, nawashukuruni sana kwa miaka yote ambayo mumetusapoti sisi na sisi tuko tayari kwa maagizo mutakayotupa tuendeleza kufanya kazi yenu Mhe. Naibu Spika naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda sasa niwauleze wajumbe wale wanaokubaliana na hoja wanyooshe mikono, wanaokataa wanaokubali wameshinda. MheWaziri.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda : Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Baraza lako tukufu limejadili na kukubali Hutuba ya Bajeti ya wizara yangu Wizara ya Biashara na Viwanda, sasa naomba baraza lako tukufu likae kama kamati ya matumizi ili kuvipitisha vifungu vya matumizi vya wizara yangu Mhe. Naibu Spika naomba kutoa hoja.

KAMATI YA MATUMIZI

FUNGU R01 - WIZARA YA BIASHARA NA VIWANDA

Kifungu R0104	Idara ya Biashara na Ukuzaji Masoko	1,213,061,000
Kifungu R0106	Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali	300,000,000
Jumla Kuu		**1,513,061,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

Kifungu PR0101	Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Biashara	2,617,636,000
Kifungu PR0102	Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali	3,831,400,000

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, nikushukuru kwa kuniona. Kwanza niweke *hansard* sawa katika fungu lile la mwanzo la Uratibu wa Wizara na Biashara, nimeuachia huru mshahara wa Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye kifungu kidogo cha SR01022 Maendeleo ya Wajasiriamali. Mhe. Mwenyekiti, mwaka jana 2017/2018 zilitengwa shilingi milioni 267,594,000. Lakini safari hii zimetengwa shilingi milioni 166,109,000. Nilikuwa nataka kuuliza tu nipate ufafanuzi, hizi shughuli za ujasiriamali zimefikia wapi zinakwenda au basi hatutaki tena kuwasaidia wajasiriamali mbona pesa kidogo.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, swali la Mhe. Mohamed Said ni zuri sana kwa sababu ndio tunaowahudumia sasa hivi wajasiriamali. Lakini naomba mkumbuke kwamba tumepitisha *SMIDA*, kwa hivyo sehemu kubwa ya kuwasimamia wajasiriamali uko katika huu wakala wa *SMIDA* ambao umepatiwa hapa pesa bilioni 2,000,000,000 ukijumlisha na hizi nyengine za viwanda jumla bilioni 3,881,000,000.

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa sababu suala zima la wajasiriamali hatuwezi kwamba kuwaachia *SMIDA* peke yao, kuna utafiti unatakiwa ufanywe na kuna mafunzo tunatakiwa tuyafanye. Kwa hivyo, tumebakisha fedha hizi kwa ajili ya kuwafanyia mafunzo na zaidi kwa mfano, suala la chumvi, kuna *association* ya chumvi ambayo ndio inayosimamia Kiwanda kile cha Chumvi wanatakiwa na wao wawekwe vizuri *management* yao na nini. Kwa hivyo, hizi fedha zimewekwa kwa ajili ya kazi kama hizo ambazo ni ziada ambazo *SMIDA* wanachukua watazifanya. Kwa hivyo, fedha za wajasiriamali zipo na *SMIDA* wameshaanza kazi, sasa hivi tutamalizia kuweka bodi ya wakurugenzi. Kama nilivyosema katika hotuba yangu kujenga maeneo na kuanza kazi, lakini pesa zao hawa zimehamishiwa *SMIDA*.

Mhe. Mohamed Said Mohamed: Mhe. Mwenyekiti, tuendelee.

Kifungu PR0102	Programu Kuu ya Maendeleo ya Viwanda na Ujasiriamali	3,831,400,000
Kifungu PR0103		

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya mama yangu Mhe. Amina Salum Waziri wa Biashara na Viwanda. Lakini jana nilizungumzia kuhusu suala la wafanyabiashara kule Pemba. Katika ukuzaji wa biashara nilizungumzia kwamba Pemba wana dhiki sana ya kuchukua biashara zao kutoka hapa kupeleka Pemba, na kuna eneo tayari limetengwa maalum kwa ajili ya kushushia makontena. Pale bandarini Mkoani kama unakwendea Makombeni, tuliwahi hata kuswali swala ya Iddi Mhe. Haji Omar Kheir anakumbuka, Swala ya Iddi El Hajj anakumbuka.

Mhe. Mwenyekiti, sasa nataka kujua Mhe. Waziri na siku ile katika majibu ya kamati hapa ripoti ya kamati alikiri kwamba ni kweli. Nataka nijuwe kwa sababu hili halikupata majibu, kwa hivyo nataka nijuwe kuna mpango gani wa kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wa Pemba nao hawakati tamaa katika kukuza biashara zao. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli leo alivyochangia nilimfahamu vizuri hoja yake. Kwanza kwamba kuna thamani kuwe na utaratibu mali zinazokwenda Pemba au Zanzibar zikifika Mombasa zinakwenda kulipiwa, wanafungua makontena mizigo inatolewa kule inapelekwa Pemba. Sasa utaratibu huu kwa agizo la *TRA* umezuiliwa. Kwa hivyo, mizigo yote ambayo inakuja Pemba na Unguja ni lazima iletwe moja kwa moja, ama Bandari ya Dar es Salaam au Bandari ya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hivyo, kuna wafanyabiashara hili jambo likawa limezungumzwa sana. Sisi Wizara ya Biashara na Viwanda pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango tulilifuatilia sana. Lakini mwisho wakakubali *TRA* na *KRA* kwamba kwa wale ambao mizigo yao ilikuwa imeshakwama kule waje walipie hapa Zanzibar au wakalipie Dar es Salaam. Wengi wao walilipia kwa mizigo yao mingi imeweza kutolewa.

Lakini jambo la pili analozungumza kwamba hili eneo mawasiliano wameliweka kwa ajili ya makontena hakuna kizuizi kwa sababu kama bidhaa imekuja mpaka Zanzibar inapelekwa Pemba, basi wataweza kutumia hili eneo kwa ajili ya kupeleka bidhaa zao na kuweza kuzishusha. Lakini kusema kutoka Mombasa kuja moja kwa moja Pemba, hili jambo limepigiwa marufuku, kwa nini? Kwa sababu imeonekana kwamba kuna sehemu kubwa ya upotevu wa mapato na tukubali sisi wote kwamba tunataka mapato yakusanywe.

Mhe. Mwenyekiti, ingawa sisi kama Wizara ya Biashara na Viwanda tulipewa taarifa kwa kipindi cha mwaka jana, kwamba biashara za Pemba zinategemea zaidi Tanga na Mombasa. Kwa hivyo, katika moja ya tafiti tunazozifanya kuona ni kiasi gani tutaweza kurahisisha biashara Pemba zikiwemo za vyakula na vitu vingine. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Mjumbe hili jambo tunalifanyia kazi zaidi, ili tuweze kuona yale maeneo ambayo yamewekwa na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji liweze kujaa makontena ili wafanyabiashara wa Pemba waweze kutumia pale. Lakini kusema kutokea Mombasa sio rahisi kwa sababu marufuku haya yako mpaka sasa hivi. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza namshukuru sana Mhe. Waziri Amina Salum kwa kukiri hilo na akaliona. Lakini Mhe. Mwenyekiti, kuna wafanyabiashara kule Pemba ambao tayari wameshalipia *ZRB* na wameshalipia *TRA*, hiyo mizigo iliyozuiliwa huko Mombasa mpaka leo hii iko.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nataka nijue kwamba ni lini itaanza hii *process* ya kushusha makontena pale, kwa sababu wafanyabiashara Pemba kuna wengine wanatimiza hadi makontena 20, kwa hivyo meli inapita Pemba inakuja Unguja. Kwa hivyo, mimi nataka nijue tu kwamba ni lini itaanza. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba hili suala lipo, lakini mimi na wenzangu wa mawasiliano tutalifanyia kazi hili ili kuweza kuona mizigo inafika pale. Lakini ni jambo ambalo tumelipokea na litafanyiwa kazi, lakini kwa kutoka Mombasa kuja pale haiwezekani, lakini kama ni kati ya Zanzibar na Pemba kwa hiyo serikali imesikia na italifanyia kazi.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, kwa vile Mhe. Waziri, amekubali na Mhe. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji basi *Inshaallah* tutaona. Ahsante.

Kifungu PR0103	Programu Kuu ya Utunzaji na Uendelezaji wa Biashara	2,331,464,000

Kifungu PR0104	Programu Kuu ya Viwango na Tathmini ya Ubora	2,583,300,000
Jumla Kuu		**11,363,800,000**

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vimepitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya Mabadiliko yoyote)

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda: Mhe. Naibu Spika, ilivyokua Kamati ya Matumizi imejadili na kupitisha makadirio ya fedha ya wizara yangu bila ya mabadiliko, Sssa naomba kutoa hoja kwamba Baraza liyakubali makadirio yao. Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naafiki.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, wale wanaokubaliana na hoja ya Mhe. Waziri wanyooshe mikono, wanaokataa. Wanaokubali wameshinda. *(Makofi)*

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kwanza nichukuwe fursa hii kumpongeza Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda, kwa kupitisha bajeti yake lakini vile vile kwa kuweza kujibu hoja vizuri na kwa ufasaha sana.

Mhe. Waziri pamoja na Naibu Waziri hongereni, nawatakieni kila la heri katika utekelezaji sasa wa bajeti hii ya mwaka 2017/2018. Lakini niwapongeze na Waheshimiwa Wajumbe, kwa michango yao mbali mbali pamoja na utulivu waliouonesha katika kupitisha bajeti hii.

Waheshimiwa Wajumbe, kwa kuwa shughuli zetu za leo zimemalizika, kwa hivyo sina budi kuakhirisha kikao chetu hadi kesho saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 7:49 mchana Baraza liliahirishwa mpaka tarehe 31/05/2018 saa 3:00 za asubuhi)